**13 JUNI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Arobaini na Saba – Tarehe 13 Juni, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa Mwaka 2023 *(The Public Private Partnership (Amendment) Bill, 2023)*.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ubia Baina ya

Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa Mwaka 2023 [*The Public Private Partnership (Amendment) Bill, 2023]*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:**

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023)*.

**MHE. ABEID R. IGHONDO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023)*.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaanza na maswali, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Bonnah kwa niaba yake Mheshimiwa Chumi.

Na. 601

### Mkakati wa kuhakikisha vijana wanapata ajira

**MHE. COSATO D. CHUMI K.n.y. MHE. BONNAH L. KAMOLI** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kushirikiana na Sekta Binafsi kuhakikisha vijana wanaohitimu wanapata ajira?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mbunge wa Segerea, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha vijana wanaohitimu wanapata ajira, Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi imejipanga kufanya yafuatayo:-

(i) Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuwezesha Sekta Binafsi kuwekeza kwenye sekta zinazoweza kuzalisha fursa nyingi za ajira na hivyo kuwezesha vijana wengi wahitimu kupata fursa za ajira;

(ii) Kuendelea kutekeleza programu ya mafunzo ya uzoefu wa kazi *(Internship)* kwa vijana wahitimu wa ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo ili kuwawezesha vijana husika kuwa na ujuzi unaohitajika na waajiri wa Sekta Binafsi wa ndani na nje ya nchi;

(iii) Serikali inaendelea kufanya majadiliano na Nchi za kimkakati kwa lengo la kuwezesha kuwa na Hati za Mashirikiano ya Uwili *(Bilateral Agreements)* ili kuwezesha Watanzania kunufaika na fursa za ajira zinazotokana na utangamano wa kikanda pamoja na ushirikiano wa kidiplomasia;

(iv) Serikali kupitia Wizara ya Kilimo inaendelea kutekeleza Programu ya kuwezesha vijana kushiriki katika Kilimo Biashara *(Building a Better Tomorrow Youth Initiative for Agribusiness – BBTYIA);*

(v) Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi inaendelea kutekeleza programu ya mafunzo ya vitendo (Atamizi) kwa wahitimu wa fani za uvuvi na ukuzaji viumbe maji; na

(vi) Serikali kupitia Wizara ya Madini imeendelea kuwezesha wachimbaji wadogo wa madini kwa kuwatengea maeneo pamoja na kufanya utafiti ili kuwa na uhakika wa kupata madini, kuanzisha vituo zaidi ya 93 na Ofisi za masoko 42 za kuuzia madani na hii inawapa fursa za ajira, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kwa kuwa Jiji la Dar es Salaam linauhitaji sana wa bidhaa za mbogamboga, je Serikali iko tayari kuwasaidia vijana wa Jimbo la Ilala kwa Mheshimiwa Bonnah kuwa na kitu kinaitwa *urban farming* na hivyo kuwawezesha kulima mazao ya mbogamboga ili kuliwezesha Jiji la Dar es Salaam kujitosheleza kwa bidhaa hiyo na wao kujipatia kipato?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa mazingira ya Dar es Salaam hayafanani sana na Jimbo la Mafinga Mjini. Je, Wizara na Serikali iko tayari kuwasaidia vijana wa Jimbo la Mafinga kuwapa mafunzo mahususi kwa ajili ya kutengeneza bidhaa za mazao ya misitu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bonnah Kamoli yaliyoulizwa na Mheshimiwa Cosato Chumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, kama Serikali tuko tayari kuweza kuwasaidia vijana waweze kuona kwa kushirikiana na Halmashauri tutaangalia kama suala la *urban farming* linawezekana kulingana na upatikanaji wa eneo kwenye hilo eneo, lakini pia Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia maagizo ya

Mheshimiwa Waziri Mkuu ilishaagiza kila Halmashauri iweze kutenga maeneo kwa ajili ya vijana kufanya kilimo. Kwa hiyo tutaliangalia hilo na tunalizingatia ili kuweza kuhakikisha ombi hilo tunaenda kulitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, lakini kabla ya hilo kuna *program* pia ya Vitalu Nyumba ambayo tumekuwa tukiitekeleza katika Halmashauri zote nchini zaidi ya 180. Tutaangalia na kuweza kuhakiki kama *lot* ya pili pia tutazidi kwenda kutoa vifaa na mafunzo ili waweze kunufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ambalo ameliuliza Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na Mafinga. Kwa sura ileile hili tumelichukua na tutalizingatia, tutashirikiana na Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kuona tunatengeneza mazingira mazuri ya vijana wetu kupata ajira,, ahsante.

**NAIBU SPIKA**: Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kapinga, kwa niaba yake Mheshimiwa Shangazi.

Na. 602

**Hitaji la walimu wa hesabu na fizikia katika elimu msingi na kidato cha tano na sita**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI K.n.y. MHE. JUDITH S. KAPINGA** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani kuhakikisha uwepo wa walimu wa kutosha wa masomo ya hesabu na fizikia katika elimu msingi hadi kidato cha tano na sita?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)**, alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuajiri walimu wapya wa masomo ya sayansi ili kukabiliana na upungufu uliopo ambapo kwa mwaka 2022/2023, tayari walimu 13,130 wameshapangiwa vituo vya kazi wakiwemo walimu wa masomo ya hesabu na fizikia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Serikali, lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kwa kuwa bado kuna idadi kubwa sana ya Walimu wa Masomo ya Sayansi ambao bado hawajapata ajira na Serikali ilikuwa inaendelea kuajiri kidogo kidogo.

Je, ni upi mkakati wa Serikali sasa kuhakikisha kwamba angalau inaongeza wigo wa ajira angalau kuchukua Walimu wote walioko katika soko ambao kwa sasa wako tu hawana shughuli za kufanya?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa suala zima la sayansi pia linaendana na uwepo maabara na wananchi nchi nzima maeneo yote wamejenga sana maboma mengi ya maabara, lakini kulikuwa na kasi ndogo ya ukamilishaji wa miradi hiyo ya Maabara. Je, Serikali ina mpango gani mahususi kuhakikisha kwamba ndani ya kipindi kifupi maboma yote yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi yanakamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza yaliyoulizwa na

Mheshimiwa Shangazi kwa niaba ya Mheshimiwa Kapinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hii idadi ya Walimu ambao bado hawajapata ajira hawa wa sayansi, nimtoe mashaka Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita itaendelea kutoa kipaumbele katika kuziba mapengo na kuajiri Walimu wengi zaidi kwa sababu kama walivyoona, Wabunge wote ni mashahidi, Serikali hii imejenga miundombinu mingi sana kwenye suala zima la elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa Walimu 13,130 ni kwenye mwaka wa fedha huu ambao tunaumaliza, kwa maana ilikuwa 2022/2023 na vilevile Serikali imetenga bajeti kwa ajili ya 2023/2024 na pale ambapo fedha zitaruhusu, basi Serikali itaendelea kuajiri Walimu wengi zaidi na kuwapeleka katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye swali lake la pili la uwepo wa maabara. Ni kweli Serikali iliweka kipaumbele katika ujenzi wa maabara katika maeneo mbalimbali hapa nchini kwa kupeleka shilingi milioni 30, 30 katika shule nyingi sana hapa nchini kwa ajili ya ujenzi wa maabara hizi. Baada ya ujenzi huu kukamilika sasa Serikali iko katika harakati za kutafuta fedha kwa ajili ya kupeleka vifaa vya maabara hizi. Mara baada ya vifaa hivyo kufika kwenye maabara hizi, vilevile tutaangalia tena namna gani ya kupata fedha kuendeleza ujenzi wa maabara zingine kote nchini.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Monni.

Na. 603

**Hitaji la madaktari na watumishi Kituo cha Afya Mrijo - Chemba**

**MHE. MOHAMED L. MONNI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaongeza madaktari na watumishi wa kada nyingine katika Kituo cha Afya Mrijo chenye Daktari na Nesi mmoja?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI),** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, Mbunge wa Jimbo la Chemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ilipata kibali cha ajira na kuajiri Watumishi wa Kada ya Afya 7,340 ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Chemba ilipatiwa Watumishi 87. Kati ya hao, Watumishi wawili walipelekwa kwenye Kituo cha Afya Mrijo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imeajiri Watumishi wa Kada za Afya 8,000, ambapo Halmashauri ya Wilaya Chemba nayo imepatiwa Watumishi wa Afya ambao watapelekwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Monni.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Swali la kwanza; Hospitali ya Wilaya ya Chemba tayari imefungwa mashine za *x-ray* na *ultra-sound* lakini hakuna mtaalam hata mmoja. Naomba kujua ni lini Serikali itapeleka wataalam hao ili mashine hizo zifanye kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Kituo hicho hicho cha Afya cha Mrijo kinahudumia Kata nne zikiwemo Kata za Wilaya ya Kiteto. Naomba kujua ni lini sasa watapeleka gari la wagonjwa ili liweze kuhudumia kituo hicho?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mohamed Lujio Monni, Mbunge wa Chemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza hili la wataalam wa mionzi katika Hospitali ya Wilaya. Nimtoe mashaka Mheshimiwa Monni, Serikali inaendelea kutafuta wataalam hawa hata katika ajira ambazo zilikuwa zimetangazwa na Serikali katika upungufu ambao tulipata kwa kutokuwa na watu walioomba nafasi, ni nafasi kama hizi za wataalam wa mionzi, lakini Serikali itaendelea kuweka jitihada kubwa kwa ajili ya kuajiri wataalam hawa ili Hospitali ya Wilaya ya Chemba nayo iweze kupata watumishi watakaosaidia katika kutumia mashine hizi za *x-ray* na nyinginezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye swali lake la pili la Kituo cha Afya Kata ya Mrijo ambacho kinahudumia kata nne kama alivyosema Mheshimiwa Monni. Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imewekeza fedha nyingi katika sekta hii ya afya vilevile na tayari fedha imeshatolewa kwa ajili ya ununuzi wa magari ya kubebea wagonjwa ambapo kila halmashauri hapa nchini ikiwepo Halmashauri ya Wilaya ya Chemba itapata magari mawili kwa ajili ya kubebea wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haikuishia hapo, Mheshimiwa Rais bado aliona kuna umuhimu wa kupata magari kwa ajili ya *supervision,* kwa ajili ya watalaam wetu kutembelea zahanati zetu na vituo vya afya ambavyo vipo katika Halmashauri hizi, kwa hiyo pia halmashauri hizi zitapata angalau gari moja kwa ajili ya *supervision*.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Mbunda.

Na. 604

**Ukarabati wa madarasa, nyumba za walimu na vyoo**

**MHE. JONAS W. MBUNDA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha za ukarabati wa madarasa, nyumba za Walimu na vyoo katika Shule za Msingi, Jimbo la Mbinga Mjini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI),** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Jimbo la Mbinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya tathmini ya hali ya uchakavu wa miundombinu katika Shule za Msingi Nchini na kubaini uwepo wa miundombinu inayohitaji ukarabati mkubwa, ukarabati mdogo, kubomoa na kujenga upya na isiyohitaji ukarabati. Kwa kuanzia mwaka wa fedha 2023/2024 kipaumbele kitakuwa ujenzi wa vyumba vya madarasa na shule mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hali ya uchakavu kwa nyumba za Walimu, ni jukumu la Halmashauri kufanya tathmini ya gharama zinazohitajika kukarabati nyumba za Walimu zilizopo kwenye maeneo yao na kuzitengea bajeti ili zikarabatiwe. Nitumie fursa hii kuwaelekeza Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kufanya tathmini ya ukarabati wa nyumba za Walimu na kuchukua hatua stahiki.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunda.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Naomba

nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kwa jinsi inavyoweka mikakati mizuri ya kufanya ukarabati wa miundombinu katika shule zetu za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Mbinga Mjini lina Kata 19 na Kata nane ziko mjini, Kata 11 ziko vijijini lakini bado kuna changamoto kubwa sana ya Walimu katika eneo hili la Jimbo la Mbinga Mjini. Katika mgao wa Walimu ambao wameajiriwa hivi karibuni Jimbo la Mbinga Mjini halijapata Mwalimu hata mmoja. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba inamaliza changamoto hii katika Jimbo la Mbinga Mjini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI kumwelekeza Katibu Tawala, Mkoa wa Ruvuma kuhakikisha anafanya msawazo ndani ya Mkoa wake kwa maeneo ambayo yana upungufu wa watumishi. Kuna maeneo ambayo yatakuwa na watumishi au Walimu wengi zaidi na yale ambayo bado hayajapata watumishi, basi Katibu Tawala wa Mkoa aweze kuhakikisha anapeleka watumishi ikiwemo katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunda la Mbinga Mjini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chaya, jiandae Mheshimiwa Flatei.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Katika Jimbo la Manyoni Mashariki, Shule ya Msingi ya Iseke, Makanda na Sasagila ni kongwe sana. Je, nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba wanapeleka madarasa kwenye hizi shule kongwe? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu

Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya, Mbunge wa Manyoni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hili lini Serikali itapeleka fedha katika shule hizi kongwe. Tayari Serikali kupitia mradi wa *BOOST* imetenga zaidi ya bilioni 230 kote nchini kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa shule kongwe hapa nchini na shule mpya katika halmashauri mbalimbali ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni. Hizi shule za Iseke, Makanda na Sasajira nazo tutazifanyia tathmini kuona uhitaji uliopo na baada ya hapo tutaziweka katika mipango yetu kwa ajili ya ofisi kutoa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante ameshakuelewa, Mheshimiwa Flatei, jiandae Mheshimiwa Songe.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Moja ya sababu za kushuka kwa ufaulu katika maeneo ya vijijini hasa Mbulu Vijijini ni kukosekana kwa nyumba za walimu na sisi tumejenga maboma yamefikia hatua mbalimbali.

Je, ni lini uko tayari kupeleka fedha katika majengo hayo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Flatei la nyumba hizi za walimu zilizojengwa kwa nguvu za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, inafanya tathmini ya maboma yote ya nyumba za walimu ambayo yamejengwa kwa nguvu za wananchi na pale tathmini hii itakapokamilika basi itawasilishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI na tutaiwekea katika mipango yetu kwa ajili ya utafutaji wa fedha ya ukamilishaji wa nyumba hizi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Songe.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu lakini pia na swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Jimbo la Busega wamejenga maboma ya madarasa 69 na nyumba za walimu 11. Je, Serikali sasa iko tayari kupelekea fedha kwa ajili ya kumalizia maboma ya wananchi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala hili la maboma kama nilivyotoka kusema hapa awali, tayari kuna timu kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa maelekezo yake Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Angellah Kairuki ambayo inafanya tathmini kujua maboma ya nyumba za walimu lakini vilevile maboma ya madarasa, pale tutakapopata idadi kamili kutoka kwenye Halmashauri hizi ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Busega tukaa na kutafuta fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma haya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shekilindi, jiandae Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule ya Msingi Mshizii, Mategho na Mavului zina hali mbaya sana. Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kupeleka pesa kwa ajili ya ukarabati wa shule hizo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kumuelekeza Afisa Elimu wa Mkoa wa Tanga kufika katika Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto

na kufanya tathmini katika shule ambayo ameitaja Mheshimiwa Shekilindi na tathmini hiyo ikikamilika basi wawasilishe Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili tuweze kuona namna gani tunatafuta fedha katika mwaka wa fedha unaofuata kwa ajili ya ujenzi wa maboma hayo katika shule hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule ya Sekondari Mpandapanda katika Wilaya ya Rungwe, Kata ya Kiwila ina wanafunzi wengi sana lakini ina idadi ndogo sana ya matundu ya vyoo. Ni lini Serikali itaongeza nguvu kuweza kujenga vyoo kwa ajili ya kuweza kuwasaidia wanafunzi hao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la matundu ya vyoo katika shule hii ya Mpandapanda Wilayani Rungwe, ni Mkurugenzi wa Halmashauri sasa nae aweze kuangalia katika mapato yake ya ndani, atenge fedha kwa ajili ya kujenga matundu ya vyoo katika shule hii ambayo ina upungufu wa matundu hayo ya vyoo. Vilevile tutakaa na Mheshimiwa Mbunge tuweze kupata taarifa zaidi ya shule hii nakuona namna gani Serikali Kuu inaweza ikachangia.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Dkt. Mathayo.

Na. 605

**Ukosefu wa wahudumu wa afya na vifaatiba**

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID** aliuliza:-

Je, nini mpango wa kuajiri waganga, watumishi wa afya na kupeleka vifaatiba kwenye zahanati na vituo vya afya nchini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutoa vibali vya ajira kwa watumishi wa kada ya afya ili kupunguza uhaba wa watumishi uliopo. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Ofisi ya Rais, TAMISEMI, iliajiri watumishi 7,732. Aidha, katika mwaka wa fedha 2022/2023 tayari Serikali imeajiri watumishi 5,319 wa kada za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Serikali imetenga shilingi bilioni 69.95 kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba. Kati ya hizo, shilingi bilioni 7.1 ni kwa ajili ya hospitali 71 za Halmashauri, shilingi bilioni 47.7 ni kwa ajili ya vituo vya afya 159 na shilingi bilioni 15 ni kwa ajili ya zahanati 300. Hadi kufikia mwezi Aprili 2023 jumla ya shilingi bilioni 58.85 zilikuwa tayari zimetolewa na Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya vifaatiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 116.92 kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mathayo.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru sana Serikali kwa kuendelea kujenga vituo vya afya na vingine vile zamani kukarabatiwa lakini ningependa kujua ni lini Serikali sasa itapeleka vifaatiba vya kutosha katika Vituo vya Afya vya Hedaru, Kisiwani, Makanya, Ruvu na Shengena?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; zahanati nyingi katika Jimbo la Same Magharibi hususan katika Tarafa ya Mwembembaga, Chemesuji na Same, zahanati zimekamilika lakini hazina watumishi. Je, ni lini Serikali sasa itapeleka watumishi wa kutosha na waganga katika zahanati hizo ili wananchi waweze kupata huduma?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Dkt. David Mathayo David.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuhusu upatikanaji wa vifaatiba katika Jimbo la Same Magharibi. Niseme tu kwamba Serikali tayari imetenga shilingi milioni 300 kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba katika vituo vya afya vilivyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Same. Vilevile, shilingi milioni 100 kwa ajili ya zahanati zilizokuwepo katika Halmashauri ya Wilaya ya Same katika Mwaka wa Fedha wa 2023/2024. Hivyo nimtoe mashaka Mheshimiwa Mbunge kwamba pale ambapo tutaanza utekelezaji wa bajeti mpya kwenye mwaka wa fedha unaokuja, tutaweka kipaumbele hizi fedha ziweze kwenda haraka kwa ajili ya ununuzi wa vifaa hivi tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili la zahanati hizi kukosa watumishi kule Halmashauri ya Wilaya ya Same. Serikali imeajiri watumishi wa afya zaidi ya 8,070 katika mwaka huu wa fedha ambao tupo na tunaenda kuumalizia. Tutaangalia ni wangapi ambao wamepangiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Same ili zahanati hizi nazo Mkurugenzi nae aweze kufanya *allocation* ya hawa watumishi wapya watakaokwenda kwenye zahanati alizozitaja Mheshimiwa Mathayo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Asia.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Tunaishukuru Serikali kwa kujenga vituo vya afya katika

Mkoa wa Manyara. Je, ni lini sasa Serikali itapeleka wataalam wa kutosha pamoja na vifaatiba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni *commitment* ya Serikali hii ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha kwamba ina wataalam wa kutosha wa afya, ndiyo maana hivi karibuni Serikali ilitoa ajira 8,070 kwa wataalamu wa afya kote nchini na Mkoa wa Manyara nao wamepata mgao wao wa wataalam hawa wa afya.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali lingine, Mheshimiwa Zaytun Swai.

Na. 606

**Ujenzi wa Shule ya Wasichana Arusha**

**MHE. ZAYTUN S. SWAI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga Shule ya Wasichana Arusha ambayo ilipangwa kujengwa katika Kata ya Enkikret - Longido?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia mradi wa kuboresha elimu ya sekondari imedhamiria kujenga shule za sekondari 26 za bweni za wasichana wanaosoma masomo ya sayansi kidato cha kwanza mpaka cha sita ambapo kila mkoa utajengewa shule moja. Ujenzi wa shule za bweni za wasichana za Mikoa unafanyika kwa awamu. Katika Awamu ya kwanza ya ujenzi Mikoa 10 imenufaika ambapo kiasi cha shilingi bilioni 30 zilitolewa

kwa ajili ya ujenzi wa shule hizo na ujenzi upo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kuwa ujenzi wa Shule ya Mkoa wa Arusha utafanyika katika awamu inayofuata hivyo ombi lake lipo kwenye utaratibu wa utekelezaji, wakati wowote fedha zitakapokuwa tayari, zitapelekwa Halmashauri husika kwa ajili ya kuanza ujenzi huo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Swai.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri lakini wananchi wa Longido wana hamu sana na shule hii, hadi sasa wako tayari kujitolea kwa nguvu kazi zao wenyewe ili basi kuendeleza shule hii. Je, Serikali haioni haja kuwapa kipaumbele wananchi hawa ambao wako *site* tayari? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa Serikali ya CCM ina malengo mema ya kuzalisha wahitimu mahiri wa masomo ya sayansi na wananchi wa Kata ya Kikatiti katika Wilaya ya Meru wamejitolea ujenzi wa maabara katika Shule ya Ngyeku Sekondari. Je, Serikali itawasaidiia wananchi hawa kumaliza maabara hii lini? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zaytun Swai.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze yeye mwenyewe Mheshimiwa Mbunge kwa maana amekuwa mstari wa mbele katika ufuatiliaji wa fedha hizi kuweza kupelekwa katika Mkoa wa Arusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la kwanza, Serikali kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi ilianza na *phase one* ya shule 10 za mwanzo ambapo bilioni 30 zilitumika, kwa sasa katika mwaka huu wa fedha ambao tupo 2022/2023 tunaenda kwenye *phase two* ambapo *disbursement* ya shule tisa, fedha za shule tisa, itafanyika muda si mrefu ikiwemo ya Shule ya Arusha ambayo wao wenyewe wamepanga kuijenga kule Longido.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili, kama nilivyosema hapo awali kwenye majibu mengine, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI, inafanya tathmini kwa ajili ya maboma haya yakiwemo haya ambayo yapo kule kwenye Kata ya Kikatiti katika Shule hii ya Ngyeku kwa ajili ya kuona ni uhitaji wa fedha kiasi gani ambao tunao ili baadaye tuweze kukaa na wenzetu wa Wizara ya Fedha na kuomba fedha hizi kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma haya.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha.

Na. 607

**Ujenzi wa barabara ya mchepuko ya Tanga – Horohoro - Chongoleani**

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE** aliuliza:-

Je lini Serikali itajenga barabara ya mchepuko kutoka barabara ya Tanga - Horohoro - Chongoleani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii inachepuka kutoka barabara ya Tanga - Horohoro kuelekea eneo ambalo kutajengwa bohari kubwa *(depot)* ya kupokelea mafuta ghafi kutoka Hoima nchini Uganda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mradi huu wa bomba la mafuta na ujenzi wa bohari kwa ajili ya upokeaji wa mafuta unaofanywa na Kampuni ya *EACOP* ambao ndiyo wasimamizi wa mradi huu, waliomba kibali cha kuimarisha barabara ya Chongoleani kwa viwango ambavyo vitaweza kuhimili uzito wa magari na mitambo itakayokuwa inapitishwa katika barabara hii kwa kipindi chote cha ujenzi wa mradi hadi utakapokamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo kutokana na hali hiyo kwa sasa barabara hii inahudumiwa na *EACOP* kupitia Mkandarasi walieingia naye mkataba kwa kipindi chote cha mradi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwanaisha.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, barabara ile ni ya changarawe na magari yenye uzito mkubwa ndiyo yanapita kuelekea kule kwenye matanki ya mafuta yanapojengwa na gharama ya kurudishia changarawe imekuwa ni kila baada ya miezi miwili ambayo inapelekea …

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa uliza swali lako.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** …inapelekea *maintenance cost* kuwa kubwa. Je, hamuoni haja kuishauri *EACOP* barabara ile ijengwe kwa kiwango cha lami kupunguza *maintenance cost* na kuweza kutumika baada ya mradi kukamilika? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la *Engineer* Ulenge, kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi kwamba barabara hii tayari baada ya utiwaji saini wa mkataba wa bomba la mafuta la Hoima tayari imehama kutoka *TARURA* na sasa inawahudumiwa na wao wenyewe *EACOP*. Tayari wameshaingia mkataba na mkandarasi wa kwao ambaye ataihudumia mpaka pale mradi huu utakapokamilika. Tunapokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na tutaufanyia kazi kupitia wenzetu wa *TARURA*, kuweza kukaa na wenzetu wale wa *EACOP* kuona ni namna gani wanaweza kuanza walau taratibu kui - *upgrade* barabara hii lakini haya yote yanategemeana na uwepo wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ahsante. Tunaendelea Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi.

Na. 608

**Tathmini ya hewa ya ukaa**

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha kikundi maalum kuweza kutathmini hewa ukaa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mbunge Viti Maalum kutoka Mkoa wa Kusini Pemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tayari imeshaweka mipango thabiti ya kusimamia na kutathimini hewa ukaa. Ofisi ya Makamu wa Rais, imetoa Mamlaka kwa Kituo cha Uratibu na Usimamizi wa Kaboni *(NCMC)* kilichopo Chuo Kikuu cha Sokoine

*(SUA)* kwa ajili kuratibu, kutathmini na kutoa utaalam wa masuala yote yanayohusu gesijoto na biashara ya hewa ukaa nchini. Aidha, katika kuhakikisha biashara ya hewa ukaa inakuwa biashara rasmi hapa nchini, Ofisi ya Makamu wa Rais, imeandaa kanuni na mwongozo wa kusimamia na kudhibiti biashara ya kaboni za mwaka 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais inaendelea kushirikiana na wadau wengine kwa kuhakikisha kwamba masuala haya ya hewa ukaa yanaeleweka kwa kila mdau na Watanzania wote kwa ujumla. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maryam.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tayari Wizara imeshatunga katika kanuni na miongozo ya biashara ya hewa ukaa. Je, ni jitihada gani ya Wizara katika kutoa uelewa wa biashara hii kwa jamii hasa wanawake? *(Makofi)*

Swali langu la pili, je, Zanzibar inanufaika vipi kutokana na fedha inayotokana na faida ya biashara hii ya hewa ya ukaa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, najibu maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Maryam pamoja na Wabunge wote kwa kuwa na hamu sana ya kutaka kujua faida na fursa mbalimbali ambazo zinapatikana kwenye biashara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar sasa muda wowote inakwenda kuanza kunufaika kutoka na biashara hii, tulichokuwa sasa tunakisubiria ni kwanza tunasubiri tumalize utafiti. Zanzibar tunayo misitu kwa upande wa Pemba tunao Msitu wa Ngezi lakini kwa upande wa Unguja tunao Msitu wa Jozani na kama unavyojua kwamba biashara hii inavunwa kwenye misitu hasa misitu ya asili. Kwa hiyo, tutakapokamilisha utafiti wetu Zanzibar inakwenda kunufaika kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa tulisema wacha tuendelee kutoa taaluma kwa wananchi hasa kwa upande wa Zanzibar, tumeshaanza kushirikiana idara ya mazingira tumeanza kutoa taaluma, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tumeanza kuwapa taaluma. Kwa hiyo, muda wowote kuanzia sasa Zanzibar inakwenda kuanza kunufaika na biashara hii ya hewa ukaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa jitihada ambazo zimechukuliwa ni kwamba, tumeunda kikosi kazi na kikosi kazi hichi kimekuwa kinashirikiana na TAMISEMI katika kuzunguka nchi yote kuhakikisha kwamba tunawafundisha wananchi. Tayari tumeshaanza kwenye baadhi ya Halmashauri za Mkoa wa Tabora, Simiyu, Katavi, Manyara na maeneo mengine. Kwa hiyo, taaluma hii tutahakikisha kwamba inaenea kote na juzi tulikuwa na Kamati za Wabunge kuwapa taaluma hii ya biashara ya hewa ukaa. Nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Mchungahela.

Na. 609

**Kuporomoka kwa bei ya korosho 2022/2023**

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA** aliuliza:-

Je, baada ya kuporomoka kwa bei ya korosho katika msimu wa 2022/2023 Serikali imechukua hatua gani kuhakikisha hali hiyo haijirudii?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Lulindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya korosho Nchini hutegemea mwenendo wa bei katika Soko la Dunia. Mabadiliko ya mwenendo wa bei katika masoko hayo huchochewa na kiasi cha korosho kinachozalishwa Duniani na mahitaji kwa wakati husika. Kwa wastani katika msimu wa mwaka 2022/2023 bei ilishuka kutoka shilingi 2,150 hadi shilingi 1,850 kwa kilo kwa korosho daraja la kwanza na shilingi 1,595 hadi shilingi 1,332 kwa korosho daraja la pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imeendelea na jitihada za kuimarisha bei ya korosho nchini kwa kufufua viwanda vya kubangua korosho pamoja na kuanzisha viwanda vipya. Vilevile, Serikali itaanzisha kongani la viwanda vya kubangua korosho ili kuongeza thamani ya korosho na kuuza moja kwa moja katika nchi walaji badala ya kuuza korosho ghafi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Issa.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu lakini ninayo maswali mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Lulindi ni mzalishaji mkubwa wa malighafi hya hivyo viwanda wanavyoahidi kuvijenga. Je, Serikali itajenga viwanda vingapi kwenye Jimbo la Lulindi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha korosho, zao hili pekee yake ndiyo linalochangia mfuko wa kilimo. Je, Serikali haioni sababu ya kutumia kiasi cha pesa zilizoko katika mfuko huu kwa ajili ya kutengenezea bima ya bei ya korosho? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza nataka nikiri ni kweli eneo la Lulindi ni kati ya wazalishaji wakubwa wa korosho. Kwa kutambua hilo Serikali pamoja na sekta binafsi itaendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kubangua korosho katika eneo hili la Lulindi ili wakulima wengi zaidi waweze kunufaika na hatua hii ya uchakataji wa korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kuhusu bima, tumeshafanya mazungumzo na Shirika la Bima la Taifa kwa ajili ya kuhakikisha ya kwamba wanaingia katika zao hili la korosho ili tuweze kumlinda mkulima pale bei inapoporomoka. Hivi sasa tupo katika hatua nzuri na baadhi ya maeneo tumeanza majaribio naamini itawafikia wakulima wengi zaidi na itakuwa ni mkombozi mkubwa kwa wakulima wa korosho nchini Tanzania.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Abubakari Asenga.

Na. 610

**Mradi wa Umwagiliaji wa Kisawasawa – Kilombero**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha mradi wa Umwagiliaji wa Kisawasawa – Kilombero?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, skimu ya umwagiliaji Kisawasawa ipo katika Kata ya Kisawasawa, Tarafa ya Mang'ula Wilaya ya Kilombero. Skimu hiyo ipo umbali wa kilometa 43 kutoka Mji wa Ifakara kupitia barabara ya Ifakara - Mikumi. Skimu ya Kisawasawa ina eneo linalofaa kwa umwagiliaji lenye ukubwa wa hekta 500.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Kilimo kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imetenga fedha za kwa ajili ya kufanya mapitio ya usanifu ili kupata gharama halisi za uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asenga.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Naishukuru Serikali kwa kututengea fedha kwa ajili ya mradi huu. Kwa kuwa Mkurugenzi wa Umwagiliaji aliahidi kwenda yeye mwenyewe, nataka kujua: Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, atamwelekeza lini aende kutembelea mwenyewe mradi huu wa Kisawasawa kwa sababu aliahidi wakati wa Bunge hapa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa Kijiji cha Lungongole Tarafa ya Ifakara nako wana eneo linalofaa kwa umwagiliaji hasa wakati wa kiangazi: Je, ukimwagiza aende Kisawasawa, uko tayari kumwagiza aende na Lungongole ili tathmini pia ianze? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nitamwelekeza Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kufika Kilombero mapema kadiri iwezekanavyo. Kuhusu eneo lake la pili, bahati nzuri tulisaini mkataba hapa wa kuajiri Washauri Waelekezi kwa ajili ya kuyapitia mabonde yote nchini likiwemo Bonde la Ifakara - Idete. Kwa hiyo, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tunayo Kampuni pale ya *Clemence* na *Vibe International Company Limited* wako tayari na wako 13% ya kufanya usanifu katika eneo hilo. Kwa hiyo, mradi huo pia utajumuishwa katika skimu ambayo itatengenezwa hapo katika Bonde la Ifakara.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Minza. Hayupo. Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Anatropia.

Na. 611

**Pato la Taifa linalochangiwa na Mkoa wa Kagera**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST** aliuliza:-

Je, Mkoa wa Kagera unachangia kiasi gani kwenye Pato la Taifa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya *National Accounts for Tanzania Mainland* inayoandaliwa na kusambazwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, hadi kufikia mwaka 2021 Mkoa wa Kagera ulichangia 2.6% ya pato la Taifa ikilinganishwa na 2.5% ya pato la Taifa kwa mwaka 2020, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mkoa wa Kagera anaosema unachangia 2.6% ni mkoa ambao una rutuba ya kutosha, unazalisha kahawa ya kutosha na pia una ardhi ya kutosha: Je, huo mkoa kuchangia kwenye pato la Taifa 2.6% haioni kwamba ni kushindwa kwa Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Mkoa wa Kagera umezungukwa na nchi mbalimbali ikiwepo Rwanda, Burundi na

maeneo mengine: Nini mkakati wa kuusaidia au kusaidia kuvutia wawekezaji katika huu mkoa ili uweze kuzalisha vya kutosha na hasa katika viwanda ili uongeze pato la Taifa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Anatropia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali haijashindwa na ushahidi wa hilo, Serikali imeweka mazingira wezeshi ili wananchi wenyewe wafanye shughuli zao za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Serikali imefanya mikakati mbalimbali na hatua mbalimbali. Hivi leo tunaona sekta za uzalishaji ndiyo ambapo Serikali imeweka nguvu zaidi ya kuwekeza mfano kama kilimo cha umwagiliaji, mifugo na uvuvi, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Kavejuru, Mbunge wa Buhigwe.

Na. 612

**Ujenzi wa Kituo cha Forodha Manyovu**

**MHE. KAVEJURU E. FELIX** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Forodha cha Manyovu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, Mbunge wa Buhigwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekamilisha usanifu wa kituo cha huduma za pamoja mpakani *(One Stop Boarder Post)* cha Manyovu kilichopo Mkoani Kigoma na ujenzi upo kwenye taratibu za awali za kumpata mkandarasi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kavejuru.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Je, lini Serikali italipa fidia kwa wananchi wanaopisha ujenzi wa kituo hicho cha forodha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Fedha na Mipango yupo tayari kuambatana nami twende Manyovu baada ya Bunge hili ili akaongee na wananchi hao wanaopisha ujenzi wa kituo hicho cha forodha? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Felix kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze hilo la pili. Niko tayari kuambatana naye kwenda sehemu husika na kuongea na wananchi kule. Swali lake la kwanza, Serikali iko katika hatua za uchambuzi wa fidia hiyo ya wananchi. Namwomba tu Mheshimiwa Mbunge awe na subira. Mara tu taratibu zitakapokamilika, basi wananchi watapata haki yao.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Hasunga.

Na. 613

**Hitaji la Mahakama ya Mkoa – Songwe**

**MHE. JAPHET N. HASUNGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatenga fedha na kuanza ujenzi wa Mahakama ya Mkoa wa Songwe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Songwe ulianza katika mwaka wa fedha 2021/2022, na jengo hilo lilijengwa eneo la Vwawa Wilayani Mbozi na lilikamilika Julai, 2022. Aidha, Jengo lilianza kutumika Agosti, 2022 na kuzinduliwa rasmi na Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania mwezi Novemba, 2022 ambapo alizindua kwa pamoja na majengo ya Mahakama za Hakimu Mkazi katika Mikoa ya Lindi na Katavi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hasunga.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza naishukuru Serikali kwa kutenga fedha na kukamilisha hilo jengo.

Je, ni kwa kiwango gani jengo hili limekuwa jumuifu kwa maana ya kuwa na Mahakama ya Mwanzo, Mahakama ya Wilaya na Mahakama ya Mkoa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa kuna msongamano mkubwa sana katika Gereza la Ilembo pale

Vwawa: Je, ni kwa kiwango gani jengo hili sasa litasaidia kuhakikisha kwamba kesi nyingi ambazo zimesongamana katika Mahakama zitaweza kwisha? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Naomba kujibu maswali mawili sasa ya Mheshimiwa Japhet, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza anataka kufahamu kama hili jengo litakuwa linajumuisha na Mahakama nyingine. Nimwarifu kwamba, katika mpango wetu wa Mahakama, miongoni mwa mikoa ambayo tunajenga majengo ambayo yatajumuisha Mahakama zote, ni pamoja na Mkoa wake. Kwa hiyo, hili limezingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, anataka kufahamu kama sasa kesi zitakwenda kwa kasi. Ni dhahiri kwamba kesi zitakwenda kwa kasi kwa sababu jengo hili baada ya kukamilika, *efficiency* ya Waheshimiwa Mahakimu wetu itaongezeka. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Regina.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama katika Wilaya ya Kiteto na Wilaya ya Hanang' Mkoani Manyara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Regina Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama yetu ina mpango wa kujenga majengo yote ya Mahakama za Wilaya na za Mwanzo katika mikoa yote Tanzania. Katika mwaka wa fedha wa

2024/2025 tuna mpango wa kujenga Hanang' pamoja na Kiteto. Kwa hiyo, Mahakama hizi ziko kwenye mpango. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea Wizara ya Maliasili na Utalii Mheshimiwa Massare.

Na. 614

**Kuvuna Tembo katika Pori la Wanyama la Rungwa, Muhesi na Kizigo**

**MHE. YAHAYA O. MASSARE** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani kuvuna/kuwahamisha Tembo kutoka katika Pori la Rungwa, Muhesi na Kizigo ambao wanaingia katika Vijiji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakiri kuwepo kwa changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu wakiwemo tembo. Kwa sasa Serikali inaendelea kutekeleza Mkakati wa Udhibiti Wanyamapori Wakali na Waharibifu wa Mwaka 2020/2024. Wizara inaendelea kufanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni kutoa elimu juu ya kujikinga na wanyamapori wakali na waharibifu; pili, kujenga vituo vya askari wanyamapori ili kusogeza huduma karibu na wananchi; na zaidi ya hapo ni kufunga mikanda *(GPS collars)* tembo kwa kuanzisha timu maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuwashirikisha wananchi kwa kutoa mafunzo kwa askari wa vijiji ili kuongeza nguvu ya kudhibiti tembo katika maeneo ya wananchi, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Massare.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa kuwa wanyama hawa wamekuwa wanashambulia watu na tatizo ni upungufu wa Askari: Je, ni lini Serikali itaongeza askari katika Kituo cha Doroto ambacho ni Makao Makuu ya *Game Reserve* ya Muhesi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kuna waathirika wengi wamevamiwa, wengine wameuawa, mashamba yao yameliwa na tembo, au wanyama wakali wameuawa: Je, ni lini mtalipa watu wetu hawa katika Jimbo langu katika Halmashauri ya Itigi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, najibu maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tunakiri kwamba kuna upungufu wa askari ambao wanatakiwa walinde kwenye maeneo haya. Nimwambie tu Mheshimiwa kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, ndani ya mwezi huu tutahakikisha kwamba tunapeleka Askari katika kituo cha Doroto ili kuhakikisha kwamba shughuli za ulinzi wa wananchi dhidi ya wanyama wakali zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie tu kwamba tayari Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan imeshaachia kiasi cha shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wote walioathirika na athari za wanyamapori wakiwemo tembo wanapatiwa fidia zao na kupatiwa malipo yao, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Malleko.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Kumekuwa na ongezeko kubwa sana la nyani na ngedere ambao wamekuwa ni waharibifu sana kwa mazao ya wananchi: Je, Serikali haioni sababu ya kuwahamisha au kuwauza nje ya nchi ili kujipatia fedha za kigeni? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya miongoni mwa wanyamapori ambao tunawatumia sana kwa shughuli zetu za utalii na kivutio cha watalii kwa ajili ya kuingiza mapato katika nchi yetu ni hao kima na wengine. Hata ukiangalia kwa mfano kwa upande wa Zanzibar, kule kuna wale kima ambao nadhani dunia nzima wanapatikana tu Zanzibar. Kwa hiyo, kwa kusema kwamba tuwachukue tuwasafirishe nadhani hili tulichukue tuende tukalifanyie kazi tukafikirie zaidi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Wizara ya Ujenzi Mheshimiwa Kawawa.

Na. 615

**Ujenzi wa Reli ya Kusini**

**MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza:-

Je, mpango wa ujenzi wa Reli ya Kusini umefikia wapi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali kwa ajili ya ujenzi wa Reli ya *Standard Gauge* ya Mtwara - *Mbamba Bay* na matawi yake ya kuelekea Liganga na Mchuchuma. Aidha, taarifa hiyo ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali, ilionyesha kuwa mradi huu unaweza pia kutekelezwa kwa uratibu wa ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi *(Public Private Partnership - PPP)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua iliyofikiwa kwa sasa ni kumwajiri Mshauri wa Kifedha *(Transaction Adviser)* ili aweze kufanya mapitio ya Upembuzi uliokamilika mwaka 2016 kwa lengo la kuandaa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa mwekezaji kwa utaratibu wa ubia *(PPP – Public Private Partnership)*, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kawawa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Mkoa wa Ruvuma umejaliwa kuwa na makaa mengi sana na inasemekana kwamba makaa yaliyopo yanaweza kuchimbwa kwa miaka isiyopungua 80; na sasa Liganga Mchuchuma imefunguka: Je, kwa nini Serikali isitafute mwekezaji kwa mfumo wa *BOT* (Jenga, Endesha na Kabidhi) kwa *base* ya makaa ya mawe yaliyopo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa kwa sasa kumekuwa na usafirishaji wa makaa ya mawe kwa malori mengi sana, malori 250 kwa siku na tani 360,000 kwa mwezi na kumekuwa na malalamiko ya wananchi kwamba Mkoa wa Ruvuma na Mtwara tunafaidikaje: Je, Serikali inaweza kuja na taarifa rasmi, yaani tani ngapi mpaka sasa hivi zimeshasafirishwa na Mkoa wa Ruvuma umepata nini; na Taifa linapata nini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda kujibu maswali

mawili ya Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia suala hili la ujenzi wa reli katika ushoroba huu wa Mtwara. Ni kweli kwamba tayari Serikali tumeshaanza ku-*engage* ubia kwa maana ya *PPP* na kuna nchi zaidi ya tano ambazo zimeonesha nia ya kuwekeza, kwa maana ya kuna nchi ya Marekani, Afrika Kusini makampuni kutoka katika hizo nchi, Morocco, Italy, Croatia pamoja na Canada, kwa maana ya kwamba makampuni haya yapo tayari kushirikiana na Serikali katika kujenga reli hii kwa mfumo wa ubia.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kuhusu manufaa na kuja na taarifa rasmi hapa Bungeni, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote wa Mikoa ya Mtwara, Lindi pamoja na Njombe kwamba Serikali ipo tayari kuja na taarifa ya manufaa ya uwepo wa makaa ya mawe katika maeneo hayo tangu tulipoanza kuchimba mpaka sasa. Kwa kupitia pia wenzetu wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara pamoja na Wizara ya Fedha tutashirikiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha, Shilingi bilioni 15 kwa kuanza malipo na fidia kwa maeneo haya la Liganga na Mchuchuma na tayari wameanza kutoa elimu katika maeneo haya. Ni jambo la kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Njau.

Na. 616

**Kupeleka fedha za ujenzi wa Balozi**

**MHE. FELISTA D. NJAU** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kuhakikisha fedha za ujenzi wa Balozi za Tanzania zinapelekwa ili kupunguza gharama kubwa ya kodi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felista Njau, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, inatekeleza mpango mkakati wa miaka 15 wa kujenga, kununua na kukarabati majengo balozini kwa kipindi cha mwaka 2017/2018 hadi 2031/2032.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Mwaka 2017/2018 na 2022/2023 Serikali imeweza kupeleka kiasi cha shilingi 10,357,785,067kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa majengo katika Balozi zetu nje ya nchi ili kuyaweka katika hali nzuri na hivyo kuipunguzia Serikali gharama kubwa ya kupanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali imekamilisha uchambuzi na utekelezaji wa mpango huo na kuandaa mkakati wa utekelezaji ambapo jumla ya miradi 14 ya kipaumbele imeainishwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano cha mwaka 2022/2023 hadi 2026/2027 kupitia fedha za Serikali pamoja na ubia na sekta binafsi. Aidha, Serikali itaendelea kupeleka fedha za ujenzi na ukarabati wa majengo katika Balozi zetu kwa kadri hali ya upatikanaji wa fedha itakavyoruhusu, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya

nyongeza. Kwa kuwa ujenzi wa balozi zetu nje ya nchi inachukua gharama kubwa ukilinganisha na hapa kwetu, lakini kikubwa kabisa bajeti ambayo tunaiweka kila mwaka haiwezi kuakisi ujenzi wa majengo hayo kutokana na kwamba itachukua muda mrefu na hatuwezi kuona tija: Serikali haioni sasa ni bora kuchukua mkopo katika taasisi za fedha nje au ndani ya nchi ili kujenga majengo hayo kwa mara moja ili kuleta tija? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Ujenzi wa balozi zetu unaleta tija kwenye Sekta ya Utalii, Biashara na Uwekezaji na huweza kuiletea Serikali pato la Taifa: Serikali haioni sasa ni bora kuainisha balozi za kimkakati ambazo zitaanza kujengwa mara moja ili kuletea Serikali yetu tija? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuanza na suala la kwanza, haya pia ni maelekezo mahususi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati wa uzinduzi wa makao makuu ya Benki ya *CRDB* mwaka 2022 kwa jinsi ni namna gani itumie taasisi binafsi na taasisi za fedha katika kuendeleza majengo yetu ubalozini. Hivi sasa tayari Serikali imeanza mazungumzo na Benki za *CRDB* na *NMB* pia na mifuko ya hifadhi ya jamii kama vile *PSSSF, WCF* na *ICCF* ili kuona vipi tunaweza kushirikiana katika suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la pili la kuainisha balozi za kimkakati. Huu ni ushauri mzuri sana wa Mheshimiwa Mbunge na tayari Serikali imeshaanza kutekeleza mkakati huo na kwa kuanzia tutaanzia na Ubalozi wa Nairobi, New York, Washington pamoja na Ubalozi wetu wa London, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri nilipata bahati kuwa kwenye Kamati hiyo miaka 17, masuala kushirikisha *Public Sector* yamezungumzwa zaidi ya miaka 10 na kamati lakini mpaka leo hakuna kinachoendelea. Pamoja tumekwenda Rwanda kuna

kiwanja kikubwa, kuna nchi jirani na mamlaka ya bandari yake Rwanda, sisi hatuna. Hebu ongezeni na *TPA* hapo, watu wa bandari waombeni na wao washirikiane na mabenki kufungua Ofisi ya Balozi na wao wapate ofisi yao mle ndani, ni jambo dogo tu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa.

**NAIBU SPIKA:** Hili nalo mnataka vilevile liende huko juu, limalizeni wenyewe. Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Khenani.

Na. 617

**Kukosa usafiri kwa vyombo vya ulinzi na usalama – Ziwa Tanganyika**

**MHE. AIDA J. KHENANI** aliuliza:-

Je, kwa nini Vyombo vya Ulinzi na Usalama vilivyopo mpakani mwa Ziwa Tanganyika havina Usafiri wa uhakika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Nkasi Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua mahitaji ya vyombo vya usafiri vya uhakika katika kudhibiti uhalifu maeneo ya mpakani mwa ziwa Tanganyika. Kwa dhamira ya kuimarisha upatikanaji wa usafiri, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetoa fedha kiasi cha shilingi bilioni 15 kwa ajili ya kununulia magari na pikipiki ambapo mchakato unaendelea. Pindi yatakapofika, pikipiki na magari hayo yatagawiwa wilaya zote zikiwemo zilizopo mpakani mwa ziwa Tanganyika. Pia katika

bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 4.5 za kununulia boti 10 kwa ajili ya doria baharini na kwenye maziwa. Baada ya kununuliwa, boti hizo zitagawiwa kwenye maeneo yenye changamoto za uhalifu ikiwemo Ziwa Tanganyika, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khenani.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali, pamoja na majibu ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri unajua kwamba kumekuwa na changamoto sana ya uvamizi kwa wavuvi kuchukuliwa vifaa vyao ikiwemo injini pamoja na fedha na tunaposema boti tunazungumzia *speed* boti kwa ajili ya kuendana na wale wahalifu wanaotoka nje za jirani. Je, Serikali haioni kuna haja sasa ya kuwapa *speed* boti kwa maana ya *fiber* askari polisi ili waweze kuwalinda wananchi wetu na kupambana na wale wahalifu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili Askari Polisi wa Nkasi wanapata changamoto kubwa sana kulingana na jiografia. Ni lini mtawapa gari pamoja na mafuta ya kutosha siyo kama hivi wanavyofanya sasa hivi ili waweze kuwajibika katika majukumu yao? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kwamba wakati mwingine wananchi wetu wanaathiriwa na majambazi hawa wanaopita maeneo ya ziwani kwa sababu wanakuwa na vifaa bora zaidi kuliko walivyokuwanavyo vijana wetu wa Jeshi la Polisi kwenye maeneo hayo. Kwa kulitambua hilo ndio maana nimeeleza katika boti tutakazonunua ni *fiber* zinazokwenda mwendokasi ili kukabiliana na hao majambazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vijana wetu ambao wanahitaji magari, nimesema yatakapotoka tutawagawia na Wilaya yako ya Nkasi itanufaika na pamoja na Jimbo la mwenzio Nkasi Kusini ambaye ni Mjumbe wa Kamati yetu ya NUU wote tutahakikisha kwamba tunapata magari. Baada ya kupata magari hayo katika mwaka ujao pia tutaongezea vitendea kazi vingine zikiwemo pikipiki ili kuimarisha uwezo wa vijana wetu wa doria kwa magari na madoria kwa pikipiki, nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mmetulia, maswali yamekwisha na sasa ni muda wa kutangaza wageni wetu.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, wageni waliopo Jukwaa la Spika; wWageni 28 wa Mheshimiwa Naibu Spika; Viongozi wa Chama cha Mapinduzi na Jumuiya zake kutoka Kata ya Kariakoo, Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mgeni wa Mheshimiwa Nape Nnauye, Waziri wa Habari Mawasilianao na Teknolojia ya Habari Naibu Katibu Mkuu wa Wizara Habari Mawasilianao na Teknolojia ya Habari, Ndugu Selestine Kakere, karibu. *(Makofi)*

Wageni wawili Mheshimiwa Jumanne Sagini, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambaye ni mke wake Ndugu Mariam Sagini na mtoto wake Ndugu Leyla Sagini, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni 60 wa Mheshimiwa Angellah Kairuki, wanafunzi viongozi wa mabaraza na klabu za watoto kutoka Shule za Arusha na Dar es Salaam wameambatana na Maafisa kutoka TAMISEMI ngazi ya Mkoa na Halmashauri pamoja na mdau wa *SOS Children Village* Jijini Arusha, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 61 wa Mheshimiwa Jumanne Sagini, Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM, Kamati ya Siasa, Kamati ya Ulinzi na Usalama kutoka Butiama, Mkoa wa Mara, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mgeni wa Mheshimiwa Zahor Haji kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni saba wa Mheshimiwa Simon Songe kutoka Busega Mkoa wa Simiyu, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 62 wa Mheshimiwa Regina Qwaray Viongozi wa UWT na Madiwani Viti Maalum kutoka Kiteto, Mkoa wa Manyara. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Cecil Mwambe, walimu wa Shule Msingi Wilaya ya Masasi kutoka Mtwara, karibuni. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Ally Jumbe wawekezaji kutoka Norway na Tanzania, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Condester Sichalwe; walimu wake kutoka Jimbo la Momba. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Michael Kembaki kutoka Wilaya ya Liwale, Mkoa wa Lindi, karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni sita wa Mheshimiwa Salum Shaafi wafanyabiashara wa Kariakoo kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni 29 wa Mheshimiwa Flatei Massay; walimu wa Shule ya Msingi Yamay kutoka Mbulu Vijijini wakiongozwa na Mheshimiwa Diwani wa Kata ya Changilii, karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 90 na walimu 10 kutoka Shule ya Sekondari Ntyuka ya Jijini Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Wanafunzi 75 na walimu watano kutoka Shule ya Sekondari *Ihsan Islamic* ya Jijini Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Katibu.

**13 JUNI, 2023**

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR - KATIBU MEZANI:**

**MUSWADA WA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa Mwaka 2023 *(The Public Private Partnership (Amendment) Bill, 2023)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa sasa namwita Mtoa Hoja Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa Mwaka 2023 *(The Public Private Partnership (Amendment) Bill, 2023)* pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Daniel Sillo Mbunge wa Babati Vijijini kwa kujadili kwa kina na kutoa ushauri kwa ajili ya kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Muswada huu umezingatia kwa kiasi kikubwa ushauri na mapendekezo mazuri ya kamati na wadau mbalimbali kwa ujumla ambao kwa nyakati tofauti walitoa ushauri wao. Aidha nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wataalam wake, wataalam wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuanda Muswada huu pamoja na marekebisho yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la marekebisho yanayopendekezwa katika muswada huu ni kutatua changamoto mbalimbali zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti yaliyomo katika Sheria ya Ubia baina ya

Sektaya Umma na Sekta Binafsi Sura namba 103, ambazo zimekuwa zikisababisha kuwepo kwa ushiriki hafifu wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa utaratibu wa ubia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na Sheria ya kutotoa haki kwa Wabia kutoka sekta binafsi kuwasilisha migogoro kwenye mahakama za kimataifa kwa utatuzi. Sheria ya kutoainisha aina ya misaada ya kifedha ya *public funding* itakayoidhinishwa kupitia Sheria ya Mikopo, Dhamana, Misaada Sura namba 134 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya *PPP*. Sheria ya kutoruhusu Mamlaka za Serikali kufanya ununuzi wa moja kwa moja kwa mbia kutoka sekta binafsi kwa ajili ya kutekeleza miradi iliyoibuliwa na mamlaka hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya kutoweka masharti kwa mwekezaji kutoka sekta binafsi aliyeshinda zabuni ya kutekeleza mradi wa *PPP* kuunda kampuni maalum ya mradi wa *PPP*. Sheria ya kuzuia vivutio vya kikodi vinavyotolewa chini ya Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Sura 38 kutolewa kwa wawekezaji wa miradi ya *PPP*…

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa naomba utulivu ndani ya Bunge.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria iliyopo inaongeza gharama kwa mwekezaji kutoka Sekta Binafsi anayeibua mradi kwa kuweka masharti ya dhamana ya kiasi kisichozidi asilimia tatu pamoja na 0.1% ya gharama za mradi. Sheria imeweka utaratibu mrefu wa maandalizi ya miradi unaochelewesha kuanza kwa utekelezaji wa miradi ya *PPP* na sheria kutokuwa na kifungu kinachoipa nguvu Sheria ya *PPP* kuwa Sheria Kiongozi katika masuala ya *PPP*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maelezo yote yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge. Muswada huu umegawanyika sehemu mbili kama ifuatavyo:-

Sehemu ya kwanza ikisomwa pamoja na Jedwali la Marekebisho yenye Ibara ya 1 na 2 inahusu masharti ya utangulizi

yanayoyojumuisha jina la Sheria. Aidha, kifungu kipya cha pili kimeongezwa ili kuyafanya masharti ya Sheria hii yatumike bila kuathiri makubaliano yanayoweka utaratibu maalum wa uendelezaji wa miradi ya kimkakati pale ambapo makubaliano hayo yatakuwa yamepata ridhaa ya Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili yenye Ibara ya 2 hadi 16 inapendekeza kufanya marekebisho yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 2 ikisomwa pamoja na Jedwali la Marekebisho inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 3 ili kutoa tafsiri ya maneno mbalimbali yatakayotumika kwenye Sheria hii. Ibara ya 3 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 4 cha Sheria ili kuondoa masharti kwa Mamlaka za Serikali kuwasilisha andiko ama dhana *(Concept Note)* pamoja na kuboresha utaratibu wa uwasilishaji wa maandiko ya miradi ya Ubia kwenye Kituo cha Ubia. Ibara za 4, 5, 7, 8, 9, 13, 14, na 16 zinapendekeza kurekebisha vifungu vya 5, 7, 9, 13, 23, 23A na 28 ili kuondoa mapungufu ya kiuandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 6 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 7B ili kutoa tafsiri ya maneno "*public funding*". Ibara ya 9 ikisomwa pamoja na Jedwali la Marekebisho inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 15 kwa lengo la kuzipa Mamlaka za Serikali uwezo wa kufanya ununuzi wa moja kwa moja wa wabia kwa miradi inayoibuliwa na Mamlaka hizo pamoja na vigezo vitakavyotumiwa na Waziri mwenye dhamana na masuala ya *PPP* kusamehe hatua ya ununuzi wa mbia vimeainishwa. Ibara ya 10 inapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 18A ili kuweka masharti kwa wawekezaji kutoka Sekta Binafsi wanaoshinda zabuni za kutekeleza mradi wa PPP kuanzisha kampuni maalum ya mradi mahsusi kwa ajili ya utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 11 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 21 kwa kufuta kifungu kidogo cha (2) ili kuruhusu vivutio vya kikodi vinavyotolewa chini ya Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Sura 38 kutolewa kwa wawekezaji wanaotekeleza miradi ya *PPP*. Ibara ya 12 inapendekeza kufuta

na kuandika upya kifungu cha 22 ili kuwezesha utatuzi wa migogoro kufanyika kwa kuzingatia makubaliano ya kimkataba. Ibara ya 16 inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 28A ili kuifanya Sheria hii kuwa na nguvu endapo utatokea ukinzani na Sheria zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, naomba Bunge lako tukufu lijadili Muswada huu na hatimaye kuuridhia kuwa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijamaliza nitumie fursa hii kuipongeza sana Timu ya Yanga kwa kutwa kombe la tatu msimu huu pale Tanga hapo jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**MAELEZO YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO, MHESHIMIWA DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MUSWADA WA MAREKEBISHO YA SHERIA YA UBIA BAINA YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI, WA MWAKA 2023 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**UTANGULIZI**

1. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa mwaka 2023 (The Public Private Partnership (Amendment) Bill, 2023) pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili.

2. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake **Mheshimiwa Daniel Sillo, (Mbunge wa Babati Vijijini)** kwa kuujadili kwa kina na kutoa ushauri kwa ajili ya kuuboresha Muswada huu.

3. **Mheshimiwa Spika**, napenda kulihakikishia Bunge lako tukufu kwamba, Muswada huu umezingatia kwa kiasi kikubwa ushauri na mapendekezo mazuri ya Kamati na wadau mbalimbali kwa ujumla ambao kwa nyakati tofauti walitoa ushauri wao. Aidha, nitoe shukran zangu kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wataalam wake, wataalam wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuandaa Muswada huu pamoja na marekebisho yake.

4. **Mheshimiwa Spika**, lengo la marekebisho yanayopendekezwa katika Muswada huu ni kutatua changamoto mbalimbali zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti yaliyomo katika Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Sura 103, ambazo zimekuwa zikisababisha kuwepo kwa ushiriki hafifu wa Sekta Binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa utaratibu wa ubia.

5. **Mheshimiwa Spika**, baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na: -

i. Sheria kutotoa haki kwa wabia kutoka Sekta Binafsi kuwasilisha migogoro kwenye mahakama za kimataifa kwa utatuzi;

ii. Sheria kutoanisha aina ya misaada ya kifedha (public funding) itakayoidhinishwa kupitia Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya PPP;

iii. Sheria kutoruhusu Mamlaka za Serikali kufanya ununuzi wa moja kwa moja wa mbia kutoka Sekta Binafsi kwa ajili ya kutekeleza miradi inayoibuliwa na mamlaka hizo;

iv. Sheria kutoweka masharti kwa Mwekezaji kutoka Sekta Binafsi aliyeshinda zabuni ya kutekeleza mradi wa PPP kuunda Kampuni Maalum ya Mradi wa PPP;

v. Sheria kuzuia vivutio vya kikodi vinavyotolewa chini ya Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Sura 38 kutolewa kwa wawekezaji wa miradi ya PPP;

vi. Sheria iliyopo inaongeza gharama kwa mwekezaji kutoka Sekta Binafsi anayeibua mradi *(Unsolicited proposal)* kwa kuweka masharti ya dhamana ya kiasi kisichozidi asilimia tatu (3%) pamoja na 0.1% ya gharama za mradi;

vii. Sheria imeweka utaratibu mrefu wa maandalizi ya miradi unaochelewesha kuanza kwa utekelezaji wa miradi ya PPP; na

viii. Sheria kutokuwa na Kifungu kinachoipa nguvu Sheria ya PPP kuwa Sheria Kiongozi katika masuala ya PPP.

6. **Mheshimiwa Spika**, Muswada huu unakusudia kurekebisha Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Sura 103 ili pamoja na mambo mengine kuiwezesha Sekta Binafsi kushiriki kikamilifu katika kutekeleza miradi ya maendeleo kwa utaratibu wa PPP; kuimarika kwa huduma za jamii kutokana na ubunifu, teknolojia na ujuzi kutoka Sekta Binafsi; na kupungua kwa muda wa maandalizi ya miradi na hivyo kuharakisha utekelezaji wa miradi ya PPP.

7. **Mheshimiwa Spika**, Muswada huu kwa kiwango kikubwa umezingatia ushauri na mapendekezo ya wadau mbalimbali wakiwemo Sekta ya Umma, Sekta Binafsi na Wadau wa Maendeleo.

**MAUDHUI YA MUSWADA**

8. **Mheshimiwa Spika**, Muswada huu umegawanyika katika sehemu mbili kama ifuatavyo: -

**Sehemu ya Kwanza** ikisomwa pamoja na Jedwali la Marekebisho yenye Ibara ya 1 na 2 inahusu masharti ya utangulizi yanayoyojumuisha jina la Sheria. Aidha, kifungu kipya cha pili kimeongezwa ili kuyafanya masharti ya Sheria hii

yatumike bila kuathiri makubaliano yanayoweka utaratibu maalum wa uendelezaji wa miradi ya kimkakati pale ambapo makubaliano hayo yatakuwa yamepata ridhaa ya Baraza la Mawaziri.

**Sehemu ya Pili** yenye Ibara ya 2 hadi 16 inapendekeza kufanya marekebisho yafuatayo:

(a) **Ibara ya 2** ikisomwa pamoja na Jedwali la Marekebisho inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 3 ili kutoa tafsiri ya maneno mbalimbali yatakayotumika kwenye Sheria hii;

(b) **Ibara ya 3** inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 4 cha Sheria ili kuondoa masharti kwa Mamlaka za Serikali kuwasilisha Andiko Dhana (Concept Note) pamoja na kuboresha utaratibu wa uwasilishaji wa maandiko ya miradi ya Ubia kwenye Kituo cha Ubia. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza muda wa maandalizi ya miradi ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi na kuondoa changamoto mbalimbali zilizokuwa zikijitokeza wakati wa uwasilishaji wa maandiko ya miradi ya ubia kwa kuzingatia utaratibu uliobainishwa kwenye Sheria ya Bajeti;

(c) **Ibara za 4, 5, 7, 8, 9, 13, 14, na 16 zinapendekeza kurekebisha vifungu vya 5, 7, 9, 13, 23, 23A na 28** ili kuondoa mapungufu ya kiuandishi. Lengo la marekebisho haya ni kuvifanya vifungu husika viweze kutafsiriwa kwa urahisi na kuleta maana iliyokusudiwa;

(d) **Ibara ya 6** inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 7B ili kutoa tafsiri ya maneno “public funding”. Lengo la marekebisho haya ni kuainisha misaada ya kifedha itakayosaidia utekelezaji wa miradi ya ubia;

(e) **Ibara ya 9** ikisomwa pamoja na Jedwali la Marekebisho inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 15 kwa lengo la kuzipa Mamlaka za Serikali uwezo wa kufanya ununuzi wa moja kwa moja wa Wabia kwa miradi inayoibuliwa na

Mamlaka hizo ambapo vigezo vitakavyotumiwa na Waziri mwenye dhamana na masuala ya PPP kusamehe hatua ya ununuzi wa Mbia vimeainishwa. Vilevile, Ibara hii inapendekeza kubainisha hatua inayofuata baada ya kutolewa msamaha kuwa ni kuanza majadiliano ya masharti ya mkataba pamoja na kumpa mamlaka Waziri kuainisha muda wa kuanza majadiliano kupitia kanuni. Aidha, marekebisho hayo yanakusudia kuondoa masharti kwa Mwekezaji wa Sekta Binafsi kutoa dhamana ya kiwango kisichozidi asilimia 3 ya gharama za mradi. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza muda wa kupata Wabia katika hatua ya ununuzi wa Wabia na kuvutia Sekta Binafsi kuibua na kuandaa miradi ya Ubia.

(f) **Ibara ya 10** inapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 18A ili kuweka masharti kwa wawekezaji kutoka Sekta Binafsi wanaoshinda zabuni za kutekeleza mradi wa PPP kuanzisha kampuni maalum ya mradi mahsusi kwa ajili ya utekelezaji wa mradi. Marekebisho haya yanakusudia kutenganisha majukumu ya Mbia yasiyohusiana na mradi wa PPP. Aidha, inapendekezwa kuwa Mamlaka ya Serikali inaweza kuwa mwanahisa katika kampuni hiyo kwa sharti la kuchangia hisa zisizozidi asilimia 25 ya hisa za kampuni ili kuwezesha sehemu kubwa ya hisa za kampuni kutoka wa Sekta Binafsi. Kabla ya uamuzi wa Mamlaka ya Serikali kuwa mwanahisa kwenye Kampuni hiyo, inapendekezwa mamlaka hiyo iwe na uwezo wa kifedha;

(g) **Ibara ya 11** inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 21 kwa kufuta kifungu kidogo cha (2) ili kuruhusu vivutio vya kikodi vinavyotolewa chini ya Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Sura 38 kutolewa kwa wawekezaji wanaotekeleza miradi ya PPP;

(h) **Ibara ya 12** inapendekeza kufuta na kuandika upya kifungu cha 22 ili kuwezesha utatuzi wa migogoro kufanyika kwa kuzingatia makubaliano ya kimkataba. Lengo la marekebisho haya ni kutoa haki kwa wabia kuamua utaratibu wa kufuata wakati wa utatuzi wa migogoro

inayoweza kutokea wakati wa utekelezaji wa mikataba ya PPP; na

(i) **Ibara ya 16** inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 28A ili kuifanya Sheria hii kuwa na nguvu endapo utatokea ukinzani na Sheria nyingine katika masuala ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa mgongano wa kisheria wakati wa kutafsiri masharti yanayohusiana na miradi ya PPP.

**HITIMISHO**

9. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo haya, naomba Bunge lako tukufu lijadili Muswada huu na hatimaye kuuridhia kuwa sheria.

10. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri tumia muda wako vizuri kwa maslahi ya Bunge. Hoja imeungwa mkono, sasa namwita Mwenyekiti Kamati ya Bajeti.

Waheshimiwa Wabunge, naomba vilevile kumtangaza Mheshimiwa Gerson Msigwa, Msemaji Mkuu wa Serikali tunaye Bungeni hapa. *(Makofi)*

**MHE. JONAS W. MBUNDA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na kwa mujibu wa kanuni ya 99(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bajeti kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi *(The Public Private Partnership)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ilikutana na Serikali kuanzia tarehe 2 hadi tarehe 10 Juni, 2023 ili kuchambua na kujadili kuhusu mapendekezo ya Muswada huu ambao unakusudia kufanya marekebisho kwenye Sheria ya

Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi Sura namba 103 ya mwaka 2010 kama ulivyorekebishwa mwaka 2014, 2018, 2020 na 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati iliupitia Muswada huu kifungu kwa kifungu kwa madhumuni ya kujielimisha maudhui ya kila kifungu na kupendekeza marekebisho katika maeneo ambayo yalihitaji maboresho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati ilifanya majadiliano ya kina na Waziri wa Fedha na Mipango, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kamishna wa *PPP* pamoja na wataalam kutoka Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Aidha, pia ilikutana na wadau mbalimbali kwa ajili ya kupokea mapendekezo na maoni kuhusu Muswada huu kabla ya kuanza majadiliano na Serikali. Wadau walioshiriki ni pamoja na *The Tanganyika Law Society,* Baraza la Maaskofu Tanzania, Haki Rasilimali, *Seka & Associate Advocates,* Baraza la Wakristu Tanzania, Baraza la Habari Tanzania, Tanzania *Chamber of Commerce and Agriculture* pamoja na maoni binafsi yaliyowasilishwa kwa njia ya barua pepe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu una dhamira ya kufuta baadhi ya vifungu, kuongeza vifungu vipya ukiwa na lengo la kutatua changamoto mbalimbali zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti yaliyomo katika Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi ambazo zimekuwa zikisababisha sekta binafsi kutokushiriki katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa utaratibu wa ubia.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa inayowasilishwa mbele yako ni muhtasari wa maeneo yaliyokuwa na utata na yalihitaji marekebisho kutoka kwa Serikali. maeneo hayo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, namba moja, Ibara ya 2 mpya ya Muswada inayofanya marekebisho katika kifungu kidogo cha (2).

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho haya yanakusudia kufuta kifungu cha 2(2) cha Sheria ya Ubia ili kuweka sharti la kutokutumia masharti ya Sheria hii kwa miradi ya kimkakati ambayo imeridhiwa na Baraza la Mawaziri na Wawekezaji au Mwekezaji ambaye ana mikataba na Serikali. Lengo ni kutocheleweshautekelezaji wa miradi ya kimkakati yenye manufaa ya kitaifa pindi mwekezaji anapopatikana. Marekebisho hayo awali hayakuwa kwenye muswada uliyosomwa Bungeni. Hata hivyo yamejumuishwa kwenye jedwali la marekebisho lililowasilishwa kwenye Kamati na Waziri wa Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilishauri Serikali kutoa Tafsiri ya maneno, Mradi wa Kimkakati *(Strategic Project)* pamoja na kuweka sharti la mikataba yote itakayoingiwa na Serikali kupitiwa na kuridhiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Lengo la marekebisho hayo ni kuhakikisha kwamba miradi ambayo haitalazimika kupitia utaratibu wa Sheria hii inakuwa ni ile ya kimkakati na ambayo mikataba yake imeridhiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya kamati kama ilivyoonekana kwenye jedwali la marekebisho,

Mheshimiwa Naibu Spika, namba mbili; Ibara ya 3 ya Muswada inayofanya marekebisho katika Kifungu cha 3 cha Sheria hii ili kutoa tafsiri ya maneno "*Public Sector a Model Agreement*" pamoja na maneno "*Special Purpose Vehicle*".

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya mabadiliko katika tafsiri ya maneno '*Public Sector*' ili kujumuisha Sekretarieti za Mikoa kwenye jukumu la kuibua, kuandaa na kusimamia miradi ya ubia. Hatua hii itasaidia kuhamasisha Sekretarieti za Mikoa kutekeleza miradi kwa njia ya ubia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho mengine ni pamoja na kubadilisha neno "*a model agreement*" na badala yake litumike "*Standard Documents*" itakayokuwa imepitishwa na kuridhiwa na Mamlaka ya Ununuzi *PPRA*. Hatua hii inaenda kuondoa mkanganyiko utakaoweza kujitokeza na kuwepo na aina nyingi na tofauti za "*a model agreement*".

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko mengine yaliyopendekezwa katika kifungu hicho ni kutoa tafsiri ya maneno kampuni maalumu ya kutekeleza miradi *"special purpose vehicle"*. Tafsiri iliyokuwa imependekezwa na Serikali haikubainisha kwamba vihatarishi vya mradi kwa upande wa Serikali vitabebwa sawa na hisa ambazo Serikali inamiliki katika kampuni hiyo. Baada ya majadiliano Serikali ilikubali kufanya mabadiliko ya tafsiri ya maneno hayo kama ilivyopendekezwa na Kamati. Mabadiliko hayo ni kama inavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, namba tatu; Ibara ya 6 Muswada inayofanya Marekebisho katika Kifungu cha 7B ina lengo la kutoa tafsiri ya maneno ya "*public funding*." Marekebisho haya yanalenga kuainisha misaada ya kifedha itakayotolewa na Serikali kusaidia utekelezaji wa miradi ya ubia. Lengo ni kuweka wazi aina ya vivutio vya kifedha vitakavyotolewa na Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ubia.

Mheshimiwa Naibu Spika, namba nne; Ibara ya 9 ya Muswada inapendekeza lengo la sheria kuruhusu miradi ya *PPP* kupata vivutio vya kikodi vinavyotolewa chini ya Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Sura 38 kutolewa kwa wawekezaji wa miradi ya *PPP*. Sheria ilivyo hivi sasa ilikuwa hairuhusu miradi inayotekelezwa na *PPP* kupata vivutio vya kikodi kama ilivyokuwa kwa wawekezaji wengine wanao tekeleza miradi nchini. Kifungu hiki kilikuwa hakileti usawa kwa wawekezaji. Hivyo, mabadiliko haya yanaenda kutoa fursa kwa wawekezaji wa miradi ya *PPP* nao kufurahia vivutio vya kodi kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Uwekezaji Tanzania Sura 38. Ikumbukwe kivutio cha kikodi ni moja ya kivutio kikubwa na cha msingi katika utekelezaji wa miradi, hasa ile miradi mikubwa. Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa kulitambua hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, namba tano; Ibara ya 9 ya muswada inapendekeza kuondoa sharti la dhamana ya kiasi kisichozidi asilimia tatu kwa muwekezaji anayeibua mradi *(unsolicited proposal)*. Kifungu cha 15(3) na cha (4) cha sheria ilivyo hivi sasa kilikuwa na lengo kuondoa wawekezaji wababaishaji. Hata hivyo, utekelezaji wake umeonyesha kwamba

kinaongeza gharama kwa wawekezaji. Hivyo, Kamati ilikubaliana na mapendekezo ya Serikali na ikapendekeza kwamba pamoja na kuondoa vifungu hivyo kuna haja ya kuweka sharti kwa wawekezaji kutekeleza mradi katika muda uliopangwa ili kuondoa wawekezaji wababaishaji. Serikali ilikubali mapendekezo hayo ya kamati na imefanya marekebisho kupitia jedwali la marekebisho ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namba sita; Ibara ya 9 inafanya mabadiliko kwenye kifungu cha 15 ili kuweka masharti ya kumpata mbia wa kutekeleza miradi iliyoandaliwa na Mamlaka za Serikali bila kupitia ushindani ili kufupisha muda. Kamati ilijadiliana na Serikali na kukubaliana kwamba kabla Waziri mwenye dhamana hajafanya maamuzi ya kutoa msamaha kwa mradi kutopitia mchakato wa kumpata mbia kwa njia ya ushindani apate ushauri wa Kamati ya usimamizi *(PPP Steering Committee)* endapo mradi huo unastahili kutopitia ushindani. Serikali ilikubali mapendekezo hayo ya kamati kama inavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, namba saba; Ibara ya 10 Inaongeza kifungu cha 18A ili kuweka sharti kwa Muwekezaji aliyeshinda zabuni kuunda Kampuni Maalum ya Mradi wa *PPP* "*special purpose vehicle.*" Marekebisho hayo yana lengo la kuepusha uhamisho wa mali na madeni kutoka kampuni mama na kuyahamishia kwenye mapato yanayotokana na mradi wa *PPP*. Uanzishwaji wa kampuni hii utasaidia kutenganisha na kulinda faida na hasara za kampuni hii dhidi ya vihatarishi vya kifedha endapo muwekezaji anaetekeleza mradi ana kampuni zaidi ya moja. Aidha, hatua hii ina lengo la kulinda maslahi ya nchi kwenye mradi husika ikiwa ni pamoja na kulipa mapato stahiki ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, namba nane; Ibara ya 12 inafanya mabadiliko katika kifungu cha 22(1) ili kuweka utaratibu wa wabia katika utatuzi wa migogoro. Serikali imekusudia kufanya mabadiliko katika kifungu cha 22 cha Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kwa kukifuta na kukiandika upya. Lengo la mabadiliko hayo ni kuruhusu migogoro kupelekwa na

kutatuliwa katika vyombo vya usuluhishi vya kimataifa endapo njia ya awali ya kusuluhisha kupitia majadiliano haitofikiwa. Kifungu kilivyokuwa awali kilikuwa kinalazimisha wabia kutatua migogoro kwa kutumia Mahakama na Sheria za Nchi. Hatua hii ilikwamisha wawekezaji wengi kutoka nje kutekeleza miradi kwa njia ya ubia. Hivyo, kuwekwa kwa kifungu hiki ni hatua nzuri ili kuhakikisha kwamba Sekta Binafsi inashiriki kikamilifu katika miradi ya ubia na pindi kunapokuwa na migogoro itaamuliwa katika Mahakama na vyombo vya usuluhishi ambapo mbia anaona haki itatendeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Masuala mengine yaliyojadiliwa katika Kamati wakati wa kupitisha Muswada wa Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, namba moja, utekelezaji wa Masharti ya Kifungu cha 4(6) cha Sheria ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Kifungu cha 4(6) kinataka maafisa masuuli wa Wizara, Idara na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwasilisha maandiko yenye tathmini ya awali *(Pre-Feasibility Study)* kwa Waziri wa Fedha na Mipango ili ijumuishe kwenye mpango wa maendeleo wa mwaka. Masharti hayo pamoja na kuwepo katika uhai wote wa Sheria hii hadi hivi sasa yamekuwa hayazingatiwi na Maafisa Masuhuli. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuweka utaratibu wa kikanuni utakao awalazimisha Maafisa Masuhuli kufanya hivyo. Hatua hii itaongeza ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo yenye sura ya kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, namba mbili; kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya Mfuko wa Kuchochea Miradi ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi *(PPP Facilitation Fund)*. Kifungu cha 10 (a) cha Sheria ya Ubia kinataka kuanzishwa kwa mfuko wa uwekezaji wa Miradi ya *PPP*. Aidha, Kifungu cha 10 (b) (ii) kinabainisha majukumu ya mfuko huo pamoja na mengine kuwa ni kuwezesha uandaaji wa miradi ya *PPP*. Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kwamba mfuko huo haujaweza kutengewa fedha za kutosha ili kuchochea miradi ya Ubia. Katika

mwaka wa fedha 2023/2024 mfuko huu umetengewa shilingi bilioni 2.8 kati ya maombi ya shilingi bilioni 10 zilizokuwa zimeombwa. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha mfuko huu una fedha za kutosha ili miradi iandaliwe na kutekelezwa kwa mfumo wa ubia. Vilevile, Wizara, Idara, Wakala na Mamlaka za Serikali za Mitaa zianzishe utaratibu wa kutenga kiasi cha fedha katika bajeti zao ambazo zitasaidia kutekeleza hatua za awali za maandalizi ya miradi ya ubia.

Mheshimiwa Naibu Spika, namba tatu; mtazamo hasi kuhusu dhana ya utekelezaji wa miradi kwa njia ya ubia. Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kwamba kuna changamoto ya mtazamo hasi katika kutekeleza miradi yenye sura ya kibiashara kwa njia ya ubia. Mfano ujenzi wa stendi za mabasi, masoko ya wafanyabiashara na miradi ya umwagiliaji. Mtazamo huu unatokana na ukweli kwamba Wizara, Idara na Mamlaka za Serikali zinapendelea zaidi kutumia fedha za umma kuliko kuwashirikisha Sekta Binafsi. Aidha, mtazamo huu haupo kwa Watumishi wa umma tu hata baadhi ya Wananchi kunapokuwa na ushirikishwaji wa Sekta Binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo hudhani kwamba wanaibiwa. Hivyo, kuna ulazima wa kutoa elimu ili kubadili mtazamo wa sekta ya umma ili kuona matunda ya utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo yake wakati wa utendaji kazi wa kamati. Aidha, napenda kumshukuru wewe binafsi Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika, kwa kuendelea kumsaidia Spika, kuliongoza vyema Bunge lako Tukufu. Vilevile namshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao walioutoa kwa Kamati wakati wa kuchambua Muswada huu. Napenda kumshukuru Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango Dkt. Natu Mwamba, Kamishna wa *PPP* Ndg. David Kafulila na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati kipindi chote cha kuchambua Muswada huu. Kamati pia

inawashukuru wadau wote kwa maoni yao kuhusu Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwapongeza Wajumbe wa Kamati kwa umahiri, wakiongozwa na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb), Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua (Mb), Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa umahiri na ushirikiano wao katika kuchambua Muswada huu na kuweza kuuboresha hadi kufikia hatua hii. Naomba majina ya Wajumbe hao yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee nimshukuru pia Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Mwihambi, *ndc*. kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndg. Michael Kadebe akishirikiana na Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Emmanuel Rhobi, Makatibu wa Kamati pamoja na Wanasheria wa Ofisi ya Bunge kwa kuipatia Kamati ushauri wa kitaalam na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MAONI YA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA MAREKEBISHO YA SHERIA YA UBIA BAINA YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI SURA 103 – KAMA YALIVYOWASLISHWA MEZANI**

---

**1.0. UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (The Public Private Partnership (Amendment Bill) 2023).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ilikutana na Serikali kuanzia tarehe 2 hadi 10 Juni, 2023 ili kuchambua na kujadiliana kuhusu mapendekezo ya Muswada

huu ambao unakusudia kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi Sura 103 ya Mwaka 2010 kama ulivyorekebishwa mwaka 2014, 2018, 2020 na 2021. Kamati iliupitia muswada huu kifungu kwa kifungu kwa madhumuni ya kujielelimisha maudhui ya kila kifungu na kupendekeza marekebisho katika maeneo ambayo yalihitaji maboresho.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya majadiliano ya kina na Waziri wa Fedha na Mipango, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kamishna wa PPP pamoja na Wataalam kutoka Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, Kamati pia ilikutana na wadau mbalimbali kwa ajili ya kupokea mapendekezo na maoni kuhusu Muswada huu kabla ya kuanza majadiliano na Serikali. Wadau walioshiriki ni pamoja na The Tanganyika Law Society (TLS), Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC), Haki Rasilimali, Seka and Associate Advocates, Baraza la Wakristu Tanzania (CCT), Baraza la Habari Tanzania (Medica Council of Tanzania-MCT), Tanzania Chamber of Commerce and Agriculture (TCCIA), pamoja na maoni binafsi yaliyowasilishwa kwa njia ya barua pepe.

## 2.0. MADHUMUNI YA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika,** Muswada huu unadhamiria kufuta baadhi ya vifungu na kuongeza vifungu vipya, ukiwa na lengo la kutatua changamoto mbalimbali zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti yaliyomo katika Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, ambazo zimekuwa zikisababisha Sekta Binafsi kutokushiriki katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa utaratibu wa ubia.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ninayowasilisha mbele yako ni Muhtasari wa maeneo yaliyokuwa na utata na yalihitaji marekebisho toka kwa Serikali. Maeneo hayo ni kama ifuatavyo:-

### 2.1. Ibara ya 2 mpya ya Muswada inayofanya Marekebisho katika Kifungu cha 2 kifungu kidogo cha 2.

**Mheshimiwa Spika,** marekebisho haya yanakusudia kufuta kifungu cha 2 kifungu kidogo cha 2 cha Sheria ya Ubia ili kuweka sharti la

kutokutumia masharti ya Sheria hii kwa miradi ya kimkakati ambayo imeridhiwa na Baraza la Mawaziri na wawekezaji/muwekezaji ambaye ana mikataba na Serikali. Lengo ni kutokuchelewesha utekelezaji wa miradi ya kimkakati yenye manufaa ya kitaifa pindi muwekezaji anapopatikana. Marekebisho hayo awali hayakuwa kwenye muswada uliosomwa Bungeni, hata hivyo yamejumuishwa kwenye jedwali la marekebisho lililowasilishwa kwenye Kamati na Waziri wa Fedha na Mipango.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliishauri Serikali kutoa Tafsiri ya maneno Mradi wa Kimkakati '*Strategic Project'* pamoja na kuweka sharti la mikataba yote itakayoingia na Serikali kupitiwa na kuridhiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Lengo la marekebisho hayo ni kuhakikisha kwamba miradi ambayo haitalazimika kupitia utaratibu wa Sheria hii inakuwa ni ile ya kimkakati na ambayo mikataba yake imeridhiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati kama yanavyoonekana kwenye jedwali la Marekebisho.

**2.2. Ibara ya 3 ya Muswada inayofanya Marekebisho katika Kifungu cha 3 cha Sheria ili kutoa tafsiri ya maneno "Public Sector", "A Model Agreement" pamoja na maneno "Special Purpose Vehicle" (SPV)**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imefanya mabadiliko katika tafsiri ya maneno 'Public Sector' ili kujumuisha Sekretarieti za Mikoa (*Regional Secretariat*) kwenye jukumu la kuibua, kuandaa na kusimamia miradi ya ubia. Hatua hii itasaidia kuhamasisha Sekretarieti za Mikoa kutekeleza miradi kwa njia ya ubia.

**Mheshimiwa Spika,** marekebisho mengine ni pamoja na kubadilisha neno 'A Model Agreement' na badala yake litumike 'Standard Documents' itakayokuwa imepitishwa na kuridhiwa na Mamlaka ya Ununuzi PPRA. Hatua hii inaenda kuondoa mkanganyiko utakaoweza kujitokeza kutoka na kuwepo na aina nyingi na tofauti za 'A Model Agreement'.

**Mheshimiwa Spika,** mabadiliko mengine yaliyopendekezwa katika kifungu hicho ni kutoa tafsiri ya maneno kampuni maalumu ya

kutekeleza miradi "Special Purpose Vehicle". Tafsiri iliyokuwa imependekezwa na Serikali haikubainisha kwamba vihatarishi vya mradi kwa upande wa Serikali vitabebwa sawa na hisa ambazo Serikali inamiliki katika kampuni hiyo. Baada ya majadiliano Serikali ilikubali kufanya mabadiliko ya tafsiri ya maneno hayo kama ilivyopendekezwa na Kamati. Mabadiliko hayo ni kama inavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho.

**2.3. Ibara ya 6 ya Muswada inayofanya Marekebisho katika Kifungu cha 7B ina lengo la kutoa tafsiri ya maneno ya "Public Funding"**

**Mheshimiwa Spika**, marekebisho hayo yanalenga kuainisha misaada ya kifedha itakayotolewa na Serikali kusaidia utekelezaji wa miradi ya ubia. Lengo ni kuweka wazi aina ya vivutio vya kifedha vitakavyotolewa na Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ubia.

**2.4. Ibara ya 9 ya Muswada inapendekeza lengo la Sheria kuruhusu miradi ya PPP kupata vivutio vya kikodi vinavyotolewa chini ya Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Sura 38 kutolewa kwa wawekezaji wa miradi ya PPP**

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ilivyo hivi sasa ilikuwa hairuhusu miradi inayotekelezwa na PPP kupata vivutio vya kikodi kama ilivyokuwa kwa wawekezaji wengine wanaotekeleza miradi nchini. Kifungu hiki kilikuwa hakileti usawa kwa wawekezaji, mabadiliko haya yanaenda kutoa fursa kwa wawekezaji wa miradi ya PPP nao kufurahia vivutio vya kodi kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Uwekezaji Tanzania Sura 38. Ikumbukwe vivutio vya kikodi ni moja ya kivutio kikubwa na cha msingi katika utekelezaji wa miradi hasa ile miradi mikubwa. Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa kulitambua hili.

**2.5. Ibara ya 9 ya muswada inapendekeza kuondoa sharti la dhamana ya kiasi kisichozidi asilimia tatu (3%) kwa muwekezaji anayeibua mradi (Unsolicited proposal).**

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 15 kifungu kidogo cha 3 na cha 4 cha sheria ilivyo hivi sasa kilikuwa na lengo kuondoa wawekezaji wababaishaji. Hata hivyo, utekelezaji wake umeonyesha kwamba kinaongeza gharama kwa wawekezaji. Hivyo, Kamati ilikubaliana

na mapendekezo ya Serikali na ikapendekeza kwamba pamoja na kuondoa vifungu hivyo kuna haja ya kuweka sharti kwa wawekezaji kutekeleza mradi katika muda uliopangwa ili kuondoa wawekezaji wababaishaji. Serikali ilikubali mapendekezo hayo ya kamati na imefanya marekebisho kupitia Jedwali la marekebisho ya Serikali.

**2.6. Ibara ya 9 inafanya mabadiliko kwenye kifungu cha 15 ili kuweka masharti ya kumpata mbia wa kutekeleza miradi iliyoandaliwa na Mamlaka za Serikali bila kupitia ushindani ili kufupisha muda.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijadiliana na Serikali na kukubaliana kwamba kabla Waziri mwenye dhamana hajafanya maamuzi ya kutoa msamaha kwa mradi kutopitia mchakato wa kumpata mbia kwa njia ya ushindani apate ushauri wa Kamati ya usimamizi "PPP Steering Committee" endapo mradi huo unastahili kutopitia ushindani. Serikali ilikubali mapendekezo hayo ya kamati kama inavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho.

**2.7. Ibara ya 10 Inaongeza kifungu cha 18A ili kuweka sharti kwa Muwekezaji aliyeshinda zabuni kuunda Kampuni Maalum ya Mradi wa PPP " Special Purpose Vehicle"**

**Mheshimiwa Spika,** marekebisho hayo yana lengo la kuepusha uhamisho wa mali na madeni kutoka kampuni mama na kuyahamishia kwenye mapato yanayotokana na mradi wa PPP. Uanzishwaji wa kampuni hii utasaidia kutenganisha na kulinda faida na hasara za kampuni hii dhidi ya vihatarishi vya kifedha endapo muwekezaji anaetekeleza mradi ana kampuni zaidi ya moja. Aidha, hatua hii ina lengo la kulinda maslahi ya nchi kwenye mradi husika ikiwa ni pamoja na kulipa mapato stahiki ya Serikali.

**2.8. Ibara ya 12 inafanya mabadiliko katika kifungu cha 22(1) ili kuweka utaratibu wa wabia katika utatuzi wa migogoro.**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imekusudia kufanya mabadiliko katika kifungu cha 22 cha Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kwa kukifuta na kukiandika upya. Lengo la mabadiliko hayo ni kuruhusu migogoro kupelekwa na kutatuliwa katika vyombo vya usuluhishi vya kimataifa endapo njia ya awali

ya kusuluhisha kupitia majadiliano haitofanikiwa. Kifungu kilivyokuwa awali kilikuwa kinalazimisha wabia kutatua migogoro kwa kutumia Mahakama na Sheria za nchini. Hatua hii ilikwamisha wawekezaji wengi kutoka nje kutekeleza miradi kwa njia ya ubia. Hivyo, kuwekwa kwa kifungu hiki ni hatua nzuri ili kuhakikisha kwamba Sekta Binafsi inashiriki kikamilifu katika miradi ya ubia na pindi kunapokuwa na migogoro itaamuliwa katika Mahakama na vyombo vya usuluhishi ambapo mbia anaona haki itatendeka.

## 3.0. MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA UBIA BAINA YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI

**Mheshimiwa Spika,** masuala mengine yaliyojadiliwa katika Kamati wakati wa kupitisha Muswada wa Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ni kama ifuatavyo:-

### 3.1. Utekelezaji wa Masharti ya Kifungu cha 4(6) cha Sheria ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 4(6) kinataka Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwasilisha Maandiko yenye Tathmini ya Awali (Pre - Feasibility Study) kwa Waziri wa Fedha na Mipango ili ijumuishwe kwenye Mpango wa Maendeleo wa mwaka. Masharti hayo pamoja na kuwepo katika uhai wote wa Sheria hii hadi hivi sasa yamekuwa hayazingatiwi na Maafisa masuuli. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuweka utaratibu wa kikanuni utakao awalazimisha Maafisa Masuuli kufanya hivyo. Hatua hii itaongeza ushiriki wa Sekta Binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo yenye Sura ya Kibiashara.

### 3.2. Kutenga Fedha za Kutosha kwa ajili ya Mfuko wa Kuchochea Miradi ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP Facilitation Fund)

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 10A cha Sheria ya Ubia kinataka kuanzishwa kwa mfuko wa uwezeshaji wa Miradi ya PPP. Aidha, Kifungu cha 10B kifungu kodogo cha 2 kina bainisha majukumu ya mfuko huo pamoja na mengine ni kuwezesha uandaaji wa miradi ya PPP. Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kwamba mfuko huo haujaweza kutengewa fedha za kutosha ili kuchochea miradi ya Ubia. Katika mwaka wa fedha 2023/24 Mfuko huu

umetengewa **shilingi bilioni 2.8** kati ya maombi ya **shilingi bilioni 10** zilizokuwa zimeombwa**.** Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha mfuko huu una fedha za kutosha ili miradi iandaliwe na kutekelezwa kwa mfumo wa ubia. Vilevile, Wizara, Idara, Wakala na Mamlaka za Serikali za Mitaa zianzishe utaratibu wa kutenga kiasi cha fedha katika bajeti zao ambazo zitasaidia kutekeleza hatua za awali za maandalizi ya miradi ya ubia.

**3.3. Mtazamo hasi kuhusu dhana ya Utekelezaji wa Miradi kwa Njia ya Ubia**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kwamba kuna changamoto ya mtazamo hasi katika kutekeleza miradi yenye sura ya Kibiashara kwa Njia ya Ubia. Mfano ujenzi wa Stendi za Mabasi, Masoko ya Wafanyabiashara na miradi ya umwagiliaji. Mtazamo huu unatokana na ukweli kwamba Wizara, Idara na Mamlaka za Serikali zinapendelea zaidi kutumia fedha za umma kuliko kuwashirikisha Sekta Binafsi. Aidha, mtazamo huu haupo kwa Watumishi wa umma tu hata baadhi ya Wananchi kunapokuwa na ushirikishwaji wa Sekta Binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo hudhani kwamba wanaibiwa. Hivyo, kuna ulazima wa kutoa elimu ili kubadili mtazamo wa Sekta ya umma ili kuona matunda ya Utekelezaji wa Sheria hii.

**4.0. HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru wewe Mheshimiwa Dkt Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo yako wakati wa utendaji kazi wa Kamati. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika, kwa kuendelea kukusaidia kuliongoza vyema Bunge lako Tukufu. Vilevile, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao walioutoa kwa Kamati wakati wote wa kuchambua Muswada huu. Napenda kumshukuru Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango Dkt Natu Mwamba, Kamishna wa PPP Ndg. David Kafulila na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati kipindi chote cha kuchambua

Muswada huu. Kamati pia inawashukuru wadau wote kwa maoni yao kuhusu Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwapongeza Wajumbe wa Kamati kwa umahiri, wakiongozwa na Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa umahiri na ushirikiano wao katika kuchambua Muswada huu na kuweza kuuboresha hadi kufikia hatua hii. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Daniel Baran Sillo, Mb | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, Mb | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Bahati Keneth Ndingo, Mb | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Shally Josepha, Raymond, Mb | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Stella Alex Ikupa, Mb | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Jonas William Mbunda, Mb | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Zainab Katimba, Mb | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Juma Hamad Omar, Mb | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mb | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Vedastus Manyinyi Mathayo, Mb | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Omar Ali Omar, Mb | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Oran Manase Njeza, Mb | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Rashid Abdallah Rashid, Mb | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Joseph Zacharius Kamonga, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee nimshukuru pia Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndg. Michael Kadebe akishirikiana na Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Emmanuel Rhobi, Makatibu wa Kamati pamoja na

Wanasheria wa Ofisi ya Bunge kwa kuipatia Kamati ushauri wa kitaalam na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Daniel Baran Sillo,
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**
12 Juni, 2023

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa niaba ya Mwenyekiti, ahsante sana kwa kusoma vizuri. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**MUSWADA WA SHERIA YA SERIKALI**

***Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa namwita Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kabla ya kutoa maelezo kuhusu Muswada nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza miaka miwili

tangu ashike nafasi ya kuongoza nchi yetu. Katika kipindi hicho ametuongoza vyema na kupata maendeleo na mafanikio makubwa katika sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Sheria. Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na wananchi wenzangu kuendelea kumuombea Rais wetu kwa Mwenyezi Mungu amjaalie kila la kheri katika kuliongoza Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii pia kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wao mahiri katika kulitumikia Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru Mawaziri wote kwa ushirikiano wanaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kutekeleza majukumu yake. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza Mheshimiwa Spika na wewe Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri mkubwa. Ninawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuisimamia na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru pia Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Joyce Mwihambi, *ndc,* na Watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano wanaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kuwapongeza watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakiongozwa na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dkt. Evaristo Emanuel Longopa, kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ikiwemo kuandaa Muswada huu ambao ulisimamiwa kwa karibu na Bw. Honorius J. Njole, Mwandishi Mkuu wa Sheria akishirikiana na Waandishi wa Sheria wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa

Serikali. Tunatambua na tutaendelea kuhakikisha kuwa tunatekeleza majukumu yetu kwa weledi, ufanisi na kwa kuweka mbele maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie shukrani zangu kwa kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria inayoongozwa na Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba na Makamu Mwenyekiti Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia Muswada huu katika Kamati. Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Muswada huu kwa umakini na kusikiliza na kuchambua maoni yaliyowasilishwa na wadau mbalimbali walioitwa mbele ya Kamati na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu. Serikali kupitia kwa wadau wote waliohusika na sheria zinazopendekezwa kurekebishwa imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta Jedwali la Marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023)* kama ulivyowasilishwa unapendekeza marekebisho katika Sheria zifuatazo:-

(i) Sheria ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi, Sura ya 269 *(Architects and Quantity Surveyors (The Registration) Act, Cap. 269)*;

(ii) Sheria ya Huduma za Habari, Sura ya 229 *(The Media Services Act, Cap. 229);*

(iii) Sheria ya Bohari ya Dawa, Sura ya 70 *(The Medical Stores Department Act, Cap. 70)*;

(iv) Sheria ya Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa, Sura ya 419 *(The National Leaders Funerals Act, Cap. 419)*;

(v) Sheria ya Reli, Sura ya 170 *(The Railways Act, Cap. 170)*;

(vi) Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania, Sura ya 277 *(The Tanzania Forestry Research Institute Act, Cap. 277)*;

(vii) Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370 *(The Treasury Registrar (Powers and Functions) Act, Cap. 370)*; na

(viii) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148 *(The Value Added Tax Act, Cap 148)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu Tisa:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kwanza, inahusu Masharti ya Utangulizi ambayo yanajumuisha Jina la Sheria inayopendekezwa kutungwa na namna ambavyo Sheria mbalimbali zimerekebishwa katika Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Pili, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi, Sura ya 269 ambapo kifungu cha 2 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha tafsiri ya misamiati mbalimbali iliyotumika katika Sheria hiyo na kuongeza tafsiri ya baadhi ya misamiati ambayo haijatafsiriwa katika Sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 4 kinapendekezwa kurekebishwa ili kupunguza idadi ya Wajumbe wa Bodi kutoka Wajumbe 11 hadi Wajumbe tisa. Hatua hii inalenga kupunguza gharama ya uendeshaji wa Bodi na kuendana na maelekezo ya Serikali kuhusu idadi ya wajumbe inayohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 10 kinarekebishwa ili kuwajumuisha Mameneja wa Miradi katika masharti ya kifungu hicho. Lengo la marekebisho hayo ni kuhakikisha kuwa taarifa za Mameneja wa Miradi zinatunzwa katika rejesta inayotunzwa na Msajili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 12 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha masharti kuhusu sifa na vigezo na

kupanua wigo kwa ajili ya usajili wa wataalam na wahitimu katika taaluma ya ubunifu wa majengo na ukadiriaji majenzi. Marekebisho yanayopendekezwa yanalenga kupanua wigo wa fani zilizoorodheshwa na kutambua fani nyingine zinazoweza kujitokeza hapo baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 13 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza wigo wa ushiriki wa kampuni za wazawa katika miradi inayotekelezwa na kampuni za kigeni nchini. Marekebisho haya yanalenga kuongeza ubadilishanaji wa utaalam na kuwajengea uwezo wataalam wazawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 14 kinarekebishwa ili kuweka ulazima kwa mtu aliyesajiliwa nje ya nchi kutimiza vigezo vyote vya usajili vilivyoainishwa katika kifungu hicho. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha usimamizi madhubuti wa wataalam kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 18 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka masharti yanayoruhusu watalaam kutoa huduma za kitalaam kama watu binafsi ili kuongeza matumizi ya watalaam kwa umma na kuongeza fursa za ajira. Aidha, kifungu hicho kinarekebishwa pia ili kuipa Bodi mamlaka ya kutoa miongozo ya usimamizi wa huduma zitanazotolewa na watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 36 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuipa Bodi mamlaka ya kuamua na kuainisha huduma za kitaalam zinazoweza kutolewa na watalaam waliosajiliwa tofauti na zilizoainishwa katika kifungu hicho. Marekebisho haya yanalenga kutambua maendeleo ya kiuchumi na kiteknolojia yanayoweza kutokea katika fani za ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia inapendekezwa kurekebisha kifungu cha 37 ili kuweka matakwa ya ushirikishwaji wa wataalam wote katika hatua zote za utekelezaji wa miradi. Marekebisho haya yanalenga kuongeza ubora, utaalam na usalama. Aidha, kifungu hicho kinarekebishwa pia ili kuipa Bodi mamlaka ya

kusimamia na kudhibiti miradi ya ujenzi na kuondoa uwezekano wa mgongano wa kisheria katika mamlaka za utoaji wa vibali vya ujenzi wa majengo. Kifungu hicho kinavyosomeka sasa kinaashiria kuielekeza Bodi kupokea maombi ya vibali vya ujenzi wa majengo kutoka kwa watalaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 46 kinarekebishwa kwa lengo la kuoanisha kifungu hicho na sheria nyingine zinazoweka utaratibu kuhusu malipo ya Wajumbe wa Bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 53 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuipa Bodi mamlaka ya kusimamia wahitimu wa fani za ubunifu wa majengo na ukadiriaji majenzi. Kifungu kilivyo sasa kinaipa Bodi mamlaka ya kusimamia wanafunzi badala ya wahitimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada, inapendekeza marekebisho kwenye Sheria ya Huduma za Habari, Sura ya 229 ambapo kifungu cha 5 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa lengo la kumwondolea Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Habari, jukumu la uratibu wa matangazo yote ya Serikali, na pia kuiwezesha Serikali kuwa na uhuru wa kuchagua chombo cha habari itakachokitumia kwa ajili ya matangazo kwa kuzingatia nguvu ya ushindani katika soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, inapendekezwa kukifanyia marekebisho kifungu cha 38 kwa madhumuni ya kuongeza haki ya uhuru wa maoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada vile vile unapendekeza marekebisho kwenye vifungu vya 50, 51, 53, 54, 55, 63 na 64 kwa madhumuni ya kuweka adhabu tahafifu kwa makosa yatokanayo na ukiukwaji wa sheria hii, kuwafanya wanahabari kujirudi na kufurahia kazi zao. Aidha, mapendekezo ya marekebisho ya vifungu hivyo yanakusudia kuondoa adhabu kwa wamiliki wa mitambo ya uchapishaji, ambao katika hali ya kawaida, hawana uwezo wa kudhibiti maudhui yanayochapishwa katika mitambo hiyo ya uchapishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Bohari ya Dawa, Sura ya 70 ambapo kifungu cha 6 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuweka mwongozo na ufafanuzi kuhusu upatikanaji wa Wajumbe wa Bodi ya Taasisi hiyo. Mwongozo na ufafanuzi huo utasaidia kuleta ufanisi katika Bodi kwa kuleta uwiano thabiti wa Bodi na kuhakikisha utekelezaji bora na madhubuti wa Bohari ya Dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza marekebisho kwenye Sheria ya Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa, Sura ya 419 ambapo kifungu cha 6 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya kwa lengo la kuboresha masharti kuhusu mamlaka ya Rais kutoa tangazo la kifo cha Kiongozi wa Kitaifa au Kiongozi Mahsusi aliye madarakani. Marekebisho hayo pia yanampa mamlaka kiongozi mahsusi aliye madarakani kutoa tangazo la kifo cha kiongozi mahsusi mstaafu. Vilevile, marekebisho haya yanakusudia kutoa mamlaka kwa Rais kutangaza tarehe ya maziko ya Rais aliyefariki akiwa madarakani kuwa ni siku ya mapumziko. Lengo la mapendekezo haya ni kuweka bayana na kutofautisha mamlaka zinazopaswa kutoa matangazo ya vifo vya viongozi wa kitaifa na viongozi mahsusi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifungu vya 9 na 10 vinapendekezwa kurekebishwa ili kutoa mamlaka kwa kiongozi mahsusi aliye madarakani kutoa tangazo la kifo cha kiongozi mahsusi mstaafu. Lengo la marekebisho haya ni kutambua utaratibu unaotumika sasa ambapo pamoja na kwamba Sheria imemtaja Rais kama mamlaka ya kutoa tangazo la kifo cha kiongozi mahsusi mstaafu, matangazo ya aina hiyo kwa kawaida yamekuwa yakitolewa na viongozi mahsusi walio madarakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 11 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza Wajumbe katika Kamati ya Kitaifa ya Mazishi kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa mazishi ya viongozi wa kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu hii pia inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 12 ili kumtaja Waziri mwenye

dhamana na masuala ya uratibu wa shughuli za Serikali, Waziri mwenye dhamana na masuala ya Sheria na Waziri mwenye dhamana na masuala ya viongozi wastaafu kuwa Wajumbe wa Kamati ya Kitaifa ya Mazishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kifungu cha 13 cha Sheria hii kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza idadi ya Wajumbe wanaounda Kamati Tendaji. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha utendaji wa Kamati hiyo katika kushughulikia masuala yanayohusu vifo vya viongozi wa kitaifa au viongozi mahsusi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 17 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kutoa mamlaka kwa Kamati ya Mazishi ya Kitaifa kuamua muundo wa makaburi ya viongozi wa kitaifa au viongozi mahsusi. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha uwepo wa mfanano wa makaburi ya viongozi wa kitaifa au viongozi mahsusi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 18 cha Sheria kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuhamisha sehemu ambapo jeneza la kiongozi wa kitaifa litawekwa kwa ajili ya heshima za mwisho kutoka Dar es Salaam na kuwa Dodoma. Lengo la marekebisho haya ni kuoanisha masharti ya Sheria hii na Sheria nyingine zilizohamisha Makao Makuu ya Serikali na kuelekeza shughuli za Serikali kufanyika Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza marekebisho kwenye Sheria ya Reli, Sura ya 170 ambapo marekebisho ya ujumla yanapendekezwa kwa kufuta maneno "*authorized employee*" na badala yake kuweka maneno '*authorized officer*" ambayo yamekwishatafsiriwa. Sheria ilivyo sasa haina tafsiri ya maneno "*authorized employee*" hivyo, kuleta utata wa maana. Marekebisho yanapendekezwa kwa lengo la kuoanisha tafsiri zilizo katika Sheria na kuweka maana sahihi iliyokusudiwa kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa Sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada unapendekeza pia marekebisho ya jumla kwa kufuta maneno "*Railway Infrastructure Fund*" na badala yake kuweka maneno "*Railway Fund*".

Marekebisho hayo yana lengo la kupanua wigo wa Mfuko kwa kuhakikisha kwamba fedha zinazopatikana zinatumika kwa ajili ya kuendeleza Sekta ya Usafiri wa Reli kwa ujumla, tofauti na ilivyo sasa ambapo tafsiri inahusu miundombinu ya reli pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 3 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza tafsiri za baadhi ya maneno ambayo hayakuwa yametafsiriwa na kuongeza tafsiri ya misamiati mipya inayotokana na marekebisho yanayopendekezwa ili kutoa ufafanuzi wa maneno hayo kama yalivyotumika katika Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 6 cha Sheria hii kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka masharti yanayoliruhusu Shirika la Reli kuingia mikataba na makubaliano na watu na taasisi mbalimbali ili kutekeleza miradi mbalimbali ya miliki *(real estate)*. Kwa sasa, Shirika hilo halina mamlaka ya kisheria ya kutekeleza miradi ya aina hiyo. Lengo la marekebisho haya ni kulipa Shirika la Reli mamlaka ya kutekeleza miradi ya miliki na kupanua wigo wa kazi za Shirika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, inapendekezwa pia kuongezwa Vifungu vipya vya 9A, 9B na 9C kwa lengo la kuainisha masharti yanayohusu uendeshaji huria wa miundombinu ya reli *(open access)*. Chini ya utaratibu unaopendekezwa, waendeshaji binafsi *(independent operators)* watapata fursa ya kutumia miundombinu ya reli kwa ajili ya kutoa huduma za uchukuzi wa reli, ama kwa matumizi yao binafsi au kibiashara. Kwa mapendekezo haya, Shirika la Reli, kama mmiliki wa miundombinu yote ya reli nchini, litakuwa na mamlaka ya kutoa vibali kwa waendeshaji binafsi na kwa upande mwingine, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu *(LATRA)* itahusika katika usimamizi na udhibiti wa masuala yote ya kiuchukuzi ikiwemo kutoa leseni kwa waendeshaji binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mapendekezo ya kuongezwa vifungu hivi yanalenga kuondoa utaratibu wa mikataba ambao Shirika limekuwa likitumia kwa sasa, kwa kuwa umeonekana kutoleta tija stahiki. Vilevile, masharti mapya chini ya

vifungu hivyo yatasaidia kuimarisha ulinzi wa kisheria na kuendeleza Sekta ya Uchukuzi wa Reli kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 21 cha Sheria ya Reli kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza aya mpya ili kumpa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika, mamlaka ya kusimamia nidhamu kwa maafisa, watumishi na waajiriwa wengine wa Shirika la Reli. Kwa utaratibu ulivyo sasa, Bodi ya Shirika la Reli imepewa mamlaka ya kusimamia nidhamu kwa Maafisa Waandamizi *(Senior Management Officers)* wa Shirika hilo. Kwa muktadha huo, mapendekezo haya ya marekebisho, yatasaidia kuondoa ombwe la kisheria lililopo sasa ambapo Mkurugenzi Mkuu wa Shirika atakuwa na mamlaka ya kisheria ya kusimamia masuala yote ya kinidhamu ya watumishi, waajiriwa na maafisa wote ambao Sio watumishi waandamizi *(senior management employees)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada pia unapendekeza kufutwa kwa kifungu cha 22(3) cha Sheria ya Reli, kwa lengo la kuoanisha masharti ya Sheria ya Reli na masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298. Kwa hali ilivyo sasa, kifungu cha 22(3) kinaainisha kwamba, Wakurugenzi wa Idara za Shirika za Reli watatumikia Shirika hilo kwa kipindi cha miaka mitano. Hata hivyo, kwa kuzingatia kwamba Shirika la Reli ni taasisi ya umma, iliyo chini ya Sheria ya Utumishi wa Umma, kufutwa kwa kifungu kidogo cha (3) kutaondoa mkinzano wa kisheria uliopo sasa baina ya sheria hizo mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 24(1) cha Sheria kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa kuongeza maneno "*railway station or railway premises*" kwa lengo la kupanua wigo na kuimarisha ulinzi na usalama wa miundombinu ya reli. Kwa hali ilivyo sasa, Sheria ya Reli imeweka katazo la kulisha mifugo, kufanya shughuli za kilimo au ujenzi wa majengo katika hifadhi za reli bila kupata kibali cha Shirika. Hivyo, marekebisho yanayopendekezwa yanakusudia kujumuisha stesheni za reli, majengo na viwanja vya reli kama mojawapo ya maeneo ambayo shughuli zilizotajwa katika kifungu hicho hazitaruhusiwa kufanyika pasipo kibali mahsusi cha Shirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu hii ya Muswada inapendekeza kuongeza kifungu cha 24A kinachotoa fursa kwa taasisi na watu binafsi wanaohitaji kutumia hifadhi za reli au viwanja na majengo ya Shirika kufanya hivyo mara baada ya kupata vibali mahsusi kutoka kwa Shirika la Reli. Kwa hali ilivyo sasa, Sheria ya Reli haijaweka utaratibu huo na hivyo kusababisha Shirika kutumia utaratibu wa mikataba katika kutekeleza shughuli za aina hiyo. Hivyo, mapendekezo yanayokusudiwa yataweka masharti kuhusu matumizi husika ya hifadhi na majengo ya Shirika na kuimarisha kwa kiasi kikubwa utaratibu wa uendeshaji huria wa reli, ambao waendeshaji huria wa reli, watapata fursa ya kutumia reli, hifadhi za reli pamoja na majengo ya shirika kwa kuzingatia utaratibu mahsusi wa kisheria uliowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 29(2) kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka utaratibu wa mtu kuweza kupata taarifa rasmi zinazotunzwa na Shirika. Taarifa hizo, isipokuwa pale itakapohitajika nakala, hupatikana bila gharama baada ya kuwasilisha maombi kwenye Shirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kifungu cha 51 (2)(b) kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuainisha rejea sahihi ambayo masharti ya Sheria yanahusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 68 kinachohusu Mfuko wa Reli kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kupanua wigo wa matumizi ya fedha za Mfuko ili kujumuisha ununuzi wa mabehewa na vichwa vya treni pamoja na ukarabati wa mabehewa na vichwa vya treni vilivyopo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu hii pia inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 77A ambacho kinaweka katazo la kufanya shughuli za uendeshaji huria wa reli, pasipo kupata kibali cha Shirika. Aidha, kifungu hicho kimeainisha adhabu kwa wote watakaofanya shughuli za uendeshaji huria wa reli kinyume na sheria. Marekebisho hayo yanakusudia kulinda miundombinu ya reli, hususan, pale utaratibu wa uendeshaji huria wa reli unapoongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na marekebisho hayo, inapendekezwa kuongeza kifungu kipya cha 103A ambacho kina lengo la kuweka utaratibu madhubuti wa fidia kutokana na upotevu au uharibifu utakaosababishwa na ajali katika maeneo ya makutano ya reli na barabara *(railway crossing)*. Kwa kuzingatia marekebisho yanayopendekezwa, Shirika la Reli litakuwa na mamlaka ya kuamua na kurudisha gharama zote zitokanazo na uharibifu wa miundombinu ya reli au treni kufuatia ajali zitakazojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 108 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka hitaji kwa taasisi au mtu kuchangia gharama za ujenzi au ukarabati wa miundombinu katika makutano ya njia ya reli. Lengo la marekebisho hayo ni kuzitaka mamlaka na taasisi nyingine kuchangia gharama za miundombinu katika makutano ya reli ili kulipunguzia Shirika la Reli gharama ambazo si sehemu ya miundombinu ya reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania, Sura ya 277. Marekebisho katika Sheria hii yana lengo la kupanua wigo wa kisheria wa shughuli za utafiti zinazofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania *(TAFORI)* kwa kujumuisha shughuli za ufugaji wa nyuki, kama sehemu ya shughuli za utafiti zinazoshughulikiwa na Taasisi hiyo. Kwa hali ilivyo sasa, shughuli zote za utafiti zinazohusu nyuki zinasimamiwa na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania *(TAWIRI)* chini ya Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania, Sura ya 260.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia lengo hilo, Muswada unapendekeza marekebisho ya jina refu la Muswada kwa lengo la kujumuisha utafiti wa ufugaji wa nyuki katika mawanda ya Sheria hiyo. Aidha, Kifungu cha 2 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza tafsiri ya maneno mapya yanayotokana na mapendekezo ya marekebisho kama yalivyotumika kwenye Sheria. Vilevile, inapendekezwa kufanya marekebisho katika Kifungu cha 4 ili kupanua wigo wa majukumu ya Taasisi kujumuisha utafiti wa ufugaji wa nyuki na kuzingatia muundo mpya wa taasisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 5 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuakisi muundo wa sasa wa kitaasisi na pia kuliondoa Baraza *(Council)* kama mojawapo ya vyombo vyenye jukumu la kumshauri Waziri mwenye dhamana husika. Aidha, marekebisho hayo pia yana lengo la kujumuisha hifadhi za nyuki *(bee reserves)* kama sehemu ya maeneo ambayo yanaweza kutangazwa na Waziri mwenye dhamana husika kama vituo vya utafiti wa misitu nchini. Kwa sasa, Waziri ana mamlaka ya kutangaza maeneo ya misitu na hifadhi za misitu pekee kuwa vituo vya utafiti wa misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vifungu vya 8, 11 na 12 vinapendekezwa kurekebishwa ili kujumuisha shughuli za ufugaji wa nyuki kama sehemu mojawapo katika shughuli za kitafiti zinazofanywa na Taasisi. Sehemu hii pia inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 9(2) kwa lengo la kuongeza adhabu kwa makosa yanayotendwa na watu wanaojihusisha na shughuli za utafiti wa misitu au ufugaji wa nyuki. Inapendekezwa kwamba, mtu yeyote atakayeshindwa kuwasilisha taarifa zinazohusu utafiti anaoufanya atakuwa ametenda kosa la jinai na atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni mbili na isiyozidi shilingi milioni kumi au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu na kisichozidi miezi Sita au vyote kwa pamoja. Kwa hali ilivyo sasa, Sheria inaweka adhabu ya faini isiyozidi shilingi elfu tano kwa kosa linalotendwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 10 cha Sheria, ambacho kinatoa mamlaka kwa taasisi kuitisha taarifa zinazohusu tafiti za misitu au tafiti saidizi za kisayansi, kinapendekezwa kufutwa kwa kuwa maudhui ya kifungu hicho yamezingatiwa katika Kifungu cha 9. Kifungu cha 14 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kukidhi masharti ya Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370 ambapo Ofisi ya Msajili wa Hazina ndiyo taasisi stahiki inayopanga viwango vya posho za Wajumbe wa Bodi. Kwa hali ilivyo sasa, Sheria imetoa mamlaka kwa Waziri mwenye dhamana kuainisha mishahara na posho za Wajumbe wa Bodi ya *TAFORI*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 15 kinapendekezwa kufutwa ili kuondoa masharti yanayohusu mafao ya kustaafu ambayo yameainishwa katika sheria husika za Hifadhi ya Jamii. Aidha, marekebisho yanapendekezwa kwenye Kifungu cha 22(3) kwa lengo la kuoanisha kifungu hicho na utaratibu wa sasa wa Serikali ambapo shughuli za ukaguzi wa hesabu za taasisi na mashirika ya umma hufanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada pia unapendekeza marekebisho ya aya ya 1 ya Jedwali la Pili kwa lengo la kupunguza idadi ya Wajumbe wa Bodi ili kupunguza gharama za uendeshaji. Kwa hali ilivyo sasa, Bodi ya *TAFORI* inaundwa na Mwenyekiti na wajumbe wasiozidi kumi na tano. Aidha, mapendekezo haya yanakusudia kuweka bayana namna wajumbe watakavyopatikana, pia, kuhakikisha ufanisi na ushiriki wa kila mjumbe kwa ustawi wa taasisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Nane ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370 kwa kurekebisha tafsiri ya neno Waziri katika Kifungu cha 2. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwezesha masuala ya usimamizi wa mali za Serikali kusimamiwa na Waziri yeyote ambaye kwa wakati husika, atakuwa na dhamana na masuala ya mali za Serikali badala ya kujifunga kwa Wizara moja mahsusi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tisa ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148 ambapo kipengele cha 22 cha Jedwali kinarekebishwa ili kuongeza kipindi cha msamaha wa kodi kwenye huduma za kukodi ndege kwa lengo la kuruhusu sekta ya utalii kuendelea kuimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2023, ninaomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023)* kama

ilivyorekebishwa kwa mujibu wa Jedwali la Marekebisho ujadiliwe na kupitishwa katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za Nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, ahsante Mheshimiwa *AG.*

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya *PIC,* Mheshimiwa Jerry Silaa anaomba kuwatambulisha wageni wake mahsusi ambao ni wataalam wa kike wanawake ambao waliwatembelea wakati wa ziara ya Kamati mwezi wa tatu ambao ni Ndugu Mariam ambae ni fundi karakana ya Tabora, wapo madereva wa treni wawili, wapo mafundi na Wahandisi. Karibuni sana Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba kuwatangazia Wajumbe wa Kamati ya Uongozi na Kamati ya Bajeti watakutana na Serikali muda ambao tutaahirisha shughuli za Bunge leo katika Ukumbi wa Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, sasa ninamuita Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ya Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2023)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2023)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 93(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Muswada huo ulisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Bunge la 12.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136(14) na Kifungu cha 7(1)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, uliuleta Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi, kujadiliwa mapema iwezekanavyo. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada kwa kuzingatia, Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, namna Kamati Ilivyotekeleza jukumu la uchambuzi wa Muswada. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Serikali Tarehe 26 Mei, 2023 ili kupata maelezo ya Mheshimiwa Jaji Eliezer Mbuki Feleshi, Mbunge, Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu maudhui ya Muswada huo. Maelezo hayo yaliyowasilishwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro Waziri wa Katiba na Sheria, baada ya maelezo Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali, na kupata maelezo ya ufafanuzi katika Ibara mbalimbali za Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ilifanya mkutano wa kusikiliza maoni ya wadau *(Public hearing*) Tarehe 29 Mei, 2023 ili kupokea maoni yao kuhusu Muswada huu. Aidha, Kamati ilipokea maoni kwa njia ya mtandao kutoka kwa watu na makundi mbalimbali ya wadau ambao hawakuweza kufika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao. Ninawashukuru wadau wote waliotoa maoni yao ili kuuboresha Muswada huu na nichukue fursa hii kuwatambua kama ifuatavyo:-

1. *The Tanganyika Law Society,*
2. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu *(LHRC)*,
3. Jumuiya ya Kikristo Tanzania *(CCT)*,
4. Taasisi ya TWAWEZA,
5. Wanafunzi wa Sheria kutoka Vyuo Vikuu mbalimbali, na
6. Watu binafsi kutoka maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hatua hiyo, Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kwa kuzingatia maoni ya wadau. Mnamo Tarehe 01 Juni, 2023 Kamati ilikutana tena na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye alijibu hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati kuhusu Ibara mbalimbali za Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hatua hiyo, Mwenyekiti alizingatia Masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge kwa kukujulisha rasmi kwamba, Kamati imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi Wa Muswada. Kamati ilichambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2023]* ukiwa umegawanyika katika Sehemu Kuu Tisa na unapendekezwa kufanya marekebisho katika sheria Nane kwa madhumuni ya kuondoa mapungufu na kutatua changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa Sheria hizo. Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni kama ifuatavyo:-

(a) Sheria ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi, Sura ya 269.

(b) Sheria ya Huduma za Habari, Sura ya 229.

(c) Sheria ya Bohari ya Dawa, Sura ya 70.

(d) Sheria ya Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa, Sura ya 419.

(e) Sheria ya Reli, Sura ya170.

(f) Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania, Sura ya 277.

(g) Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370.

(h) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inayohusu masharti ya utangulizi, inajumuisha Ibara ya 1 inyohusu jina fupi na Ibara ya 2 inayoeleza marekebisho yanayofanyika katika sheria mbalimbali. Sheria Zinazofanyiwa Marekebisho na Maudhui yake:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi, Sura ya 269 *[The Amendment of The Architects and Quantity Surveyors (Registration) Act, (CAP. 269)]*. Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya 3 hadi Ibara ya 15 ya Muswada. Marekebisho katika sehemu hii kwa ujumla yanalenga kupanua wigo wa fani na huduma zinazotolewa katika taaluma ya ubunifu wa majengo na ukadiriaji majenzi pamoja na kuongeza fursa za ajira katika tasnia hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Huduma za Habari, Sura ya 229 *[Amendment of The Media Service Act, (CAP 229)]*. Kamati ilielezwa kuwa Marekebisho yanayopendekezwa katika sehemu hii yanalenga kumwondolea Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Habari, jukumu la uratibu wa matangazo yote ya Serikali, na pia, kuiwezesha Serikali kuwa na uhuru wa kuchagua chombo cha Habari itakachokitumia kwa ajili ya matangazo, kwa kuzingatia nguvu ya ushindani katika soko kwa kufuta aya (l) ya kifungu cha 5. Aidha, Muswada unapendekeza kufutwa kwa kifungu 38(3) cha Sheria ya Habari kilichoweka masharti ya mtu kushtakiwa kwa makosa ya Kijinai, ama madai pale anapochapisha taarifa zinazodhaniwa kuwa na uhuru usioweza kuingiliwa, (*absolutely*

*privileged*) kwa madhumuni ya kuongeza haki ya uhuru wa maoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Muswada unapendekeza marekebisho kwenye vifungu namba 50 hadi 55 na vifungu namba 63 na 64 kwa madhumuni ya kuhakikisha kwamba, wanahabari wanafurahia haki yao ya uhuru wa maoni, haki ya kupata habari na uhuru katika kazi zao za uhariri bila kuwa na uwoga wa adhabu za kijinai.

Mheshimiwa Nainu Spika, mapendekezo hayo, pamoja na mambo mengine, yanalenga kuwaondoa wanahabari katika makosa yanayohusiana na kashfa za kijinai, makosa ambayo kwa kawaida yanaangukia katika utaratibu wa mashauri ya madai. Aidha, mapendekezo ya marekebisho ya vifungu hivyo yanaenda sambamba na kuondoa adhabu kwa wamiliki wa mitambo ya uchapishaji, ambao katika hali ya kawaida hawana uwezo wa kudhibiti maudhi yanayochapishwa katika mitambo hiyo ya uchapishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Bohari ya Dawa, Sura ya 70 *[Amendment of the Medical Stores Department Act, (CAP. 70)]*. Sehemu hii inahusu ibara ya 26 na 27 ambapo Ibara ya 26 inaeleza kuwa, sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Bohari ya Dawa Sura ya 70 ambayo inajulikana kama Sheria Mama *(The Principal Act*), Ibara ya 27 inapendekeza marekebisho kwenye kifungu cha 6 kwa kufuta kifungu kidogo cha (1) ambacho kinahusu muundo wa Bodi. Marekebisho yanapendekeza muundo wa Bodi kuwa na Mwenyekiti atakayeteuliwa na Rais na Wajumbe nane watakaoteuliwa na waziri ambao wametajwa kwa mujibu wa vyeo vyao au mwakilishi wake. Lengo la marekebisho hayo ni kuleta ufanisi katika Bodi kwa kuleta uwiano thabiti wa Bodi na kuhakikisha utekelezaji bora na Madhubuti wa Bohari ya Dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tano ya Muswada inahusu marekebisho ya Sheria ya Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa, Sura ya 419 *[Amendment of The National Leaders Funeral Act,*

*(CAP. 419]*. Sehemu hii ya Muswada inahusu Ibara ya 28 hadi 37. Marekebisho haya yanalenga kuweka bayana na kutofautisha mamlaka zinazopaswa kutoa matangazo ya vifo vya Viongozi wa Kitaifa na Viongozi Mahususi. Aidha, Marekebisho haya yanapendekeza Katika Ibara ya 36 ya Muswada kuhamisha mahali pa kutolea heshima za mwisho za Kiongozi wa Kitaifa ama Kiongozi Mahsusi kutoka Uwanja wa Taifa wa Dar es Salaam na kuhamia Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Sita ya Muswada inahusu marekebisho ya Sheria ya Reli, Sura ya 170 *[Amendment of the Railways Act, (CAP. 170]*. Sehemu hii inahusu Ibara ya 38 na 52. Marekebisho haya yanalenga katika Ibara ya 46 kuweka masharti kwa mtu mwenye nia ya kutumia maeneo ya reli kuomba kibali kwa shirika na kulipa ada pamoja na gharama zinazohusiana na matumizi hayo. Ibara ya 52 inapendekeza kuongeza Kifungu cha 108(5) kinachoweka masharti kwa mtu yeyote mwenye nia ya kuomba Shirika kujenga makutano ya reli na barabara *(level crossing)* kwa matumizi binafsi au ya umma kupata kibali cha shirika na kutoa gharama za ujenzi na ukarabati kwa gharama zake mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Saba ya Muswada inahusu marekebisho ya Sheria ya Taasisi ya Utafiri wa Misitu Tanzania, Sura ya 277 *[(Amendment of the Tanzania Forestry Research Institute Act, (CAP. 277)]*. Sehemu hii inapendekeza kufanya marekebisho katika Ibara ya 53 hadi 65 ambapo Ibara ya 53 ya Muswada inaeleza kuwa Sehemu hii itasomwa kwa pamoja na Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania, Sura ya 277. Pamoja na mambo mengine katika sehemu hii, Ibara ya 58 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 8(4) cha Sheria kwa kujumuisha ufugaji wa nyuki kuwa sehemu ya shughuli za kitafiti zitakazofanywa na taasisi kwa kutungiwa kanuni na Waziri mwenye dhamana kwa kushauriana na bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Nane ya Muswada inahusu marekebisho ya Sheria ya Msajili wa Hazina (Mamlaka na Majukumu yake), Sura ya 370 *[Amendment of the Treasury Registrar (Powers and Functions) Act, (CAP. 370]*. Sehemu hii

inahusu Ibara ya 66 na 67. Ibara ya 66 inaeleza uhusiano kati ya Sheria Mama na marekebisho yanayopendekezwa kuwa marekebisho yatasomwa pamoja na Sheria Mama. Ibara ya 67 inapendekeza kufuta neno *finance* lililopo katika tafsiri ya neno *Minister* na kuweka maneno *public investments.* Lengo ni kuhamisha ofisi ya Msajili wa Hazina kutoka Wizara ya Fedha kwenda Wizara ya Uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tisa ya Muswada inahusu marekebisho ya Sheria ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148 *[Amendment of The Value Added Tax, Act (CAP. 148)]*. Sehemu hii inahusu Ibara ya 68 na 69 ambapo Ibara ya 68 inahusu uhusiano wa marekebisho yanayopendekezwa na Sheria Mama *(The principal Act)* kuwa zitasomwa pamoja. Ibara ya 69 inafanya marekebisho katika jedwali la Pili kwenye kipengele cha 22 na kufuta Tarehe 30 Disemba, 2022 na kuweka Tarehe 30 Juni, 2026 ili kuongeza kipindi cha msamaha wa kodi kwenye huduma za kukodi ndege kwa lengo la kuruhusu sekta ya utalii kuendelea kuimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuuboresha Muswada huu kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya Sheria ya Huduma za Habari, Sura ya 229. Katika Ibara zinazofuata Kamati inapendekeza adhabu zilizowekwa zinaweka ukomo wa chini wa adhabu bila kuweka ukomo wa juu wa adhabu au kuweka ukomo wa juu bila kuweka ukomo wa chini wa adhabu. Ni maoni yetu kuwa, adhabu hizi ziwekewe ukomo wa chini na wa juu ili kutunga sheria iliyo kamili badala ya kuiachia Mahakama jukumu la kuweka ukomo wa juu au wa chini wa adhabu. Kamati ilibaini kuwa katika mapendekezo ya adhabu hizo kwenye sheria hii inaweza kutumika vibaya kwa baadhi ya watu kupewa adhabu kubwa zaidi na wengine ndogo zaidi katika kosa lile lile, hivyo

kuathiri takwa la kikatiba kuhusu usawa mbele ya sheria na eneo hilo ni katika Ibara zifuatazo:-

i. Ibara ya 20(b) haijaweka ukomo wa adhabu ya juu ya kifungo.

ii. Ibara ya 21(a) aya (a) na (b) haijaweka ukomo wa juu wa faini pamoja na kifungo.

iii. Ibara ya 21(b) aya (a) na (b) hazijaweka ukomo wa adhabu ya juu isipokuwa imetaja tu ukomo wa adhabu ya chini.

iv. Ibara ya 21(f) pia haijataja ukomo wa juu wa adhabu ya faini pamoja na kifungo isipokuwa imetaja ukomo wa chini peke.

v. Ibara ya 22 imetaja ukomo wa adhabu ya chini pekee bila kutaja ukomo wa adhabu ya juu ya faini na kifungo.

vi. Ibara ya 23 imetaja ukomo wa adhabu ya chini pekee bila kutaja ukomo wa adhabu ya juu ya faini.

vii. Ibara ya 24(a) na (b) imetaja adhabu moja kwa moja bila kuwa na ukomo wa chini wala wa juu kwa faini pamoja na kifungo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika Ibara ya 25(b) ina makosa ya kiuandishi ambayo yatapoteza mantiki ya Kifungu kwa kuwa Sheria Mama imeandika adhabu isiyopungua milioni ishirini na tano wakati marekebisho yameandika milioni ishirini. Inapendekezwa Ibara ya 25(b) ifanyiwe marekebisho kwenye mstari wa tatu kutoka juu kwa kufuta maneno *twenty million shillings* na badala yake kuandika *twenty-five million shillings.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati na wamefanya mabadiliko kwa kuzingatia ushauri wa Kamati. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kufuata ushauri wa Kamati kwa kuondoa makosa dhidi ya mtu na mtu yenye sura ya madai kuondolewa kwenye orodha ya makosa ya jinai pamoja na adhabu zake, hususan kwenye Ibara ya 25 inayorekebisha kifungu cha 64 cha sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Marekebisho ya Sheria ya Bohari ya Dawa, Sura ya 70; katika Ibara ya 27 ya Muswada, ni maoni ya Kamati kuwa uwakilishi wa sekta binafsi katika bodi ni muhimu. Aidha, Kamati ilihitaji ufafanuzi utolewe katika ibara hiyo aya (f) ambayo imetaja sifa za wajumbe wengine watatu lakini haijaeleza watatoka wapi? Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati na wamefanya mabadiliko kwa kuzingatia ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Marekebisho ya Sheria ya Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa, Sura ya 419. Katika Ibara ya 29(4) ya Muswada, Kamati inapendekeza kufanya marekebisho yafuatayo: kufuta maneno "*serving President*" na kuandika maneno "*former President who died while in office*." Lengo la maboresho haya ni kukipa kifungu maana inayokusudiwa. Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati na wamefanya mabadiliko kwa kuzingatia ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia Muswada huu, naomba orodha ya majina ya Wajumbe wote wa Kamati hii yaingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Eliezer Mbuki Feleshi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali, Ndg. Onorius Njole, pamoja na watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge, Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc,* kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii. Vilevile namshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Michael Chikokoto, *ndc.* na Mkurugenzi Msaidizi, Ndg. Gerald Magili, kwa

kusimamia utendaji wa Kamati mbalimbali za Bunge ikiwemo Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, naishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria ambayo imehusika na uratibu wa shughuli zote za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii, wakiwemo Ndg. Frank Rumisha Nkya, Ndg. Praisegod Lukio, Ndg. Ganjatuni Kilemile, Ndg. Elizabeth Malogo, Ndg. Maria Mdulugu, Ndg. Evelyn Shibandiko, Ndg. Ludovick Ringia, Ndg. Nesta Kawamala, pamoja na Msaidizi wa Kamati, Ndg. Theresia Jacob.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama lilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI WA MWAKA 2023 *[THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) ACT, 2023]* – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali na Hadidu za Rejea

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2023)*.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 93 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Muswada huo ulisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Tano wa Bunge la 12.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136 (14) na Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, uliuleta Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa mapema iwezekanavyo. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba, Kamati iliuchambua na kuujadili Muswada kwa kuzingatia, Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

**1.2 Namna Kamati ilivyotekeleza Jukumu la Uchambuzi wa Muswada**

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Serikali tarehe 26 Mei, 2023 ili kupata maelezo ya Mhe. Jaji Eliezer Mbuki Feleshi (Mb) Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu maudhui ya Muswada huo. Maelezo hayo yaliyowasilishwa kwa niaba yake na Mhe. Damas D. Ndumbaro Waziri wa Katiba na Sheria. Baada ya maelezo, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali, na kupata maelezo ya ufafanuzi katika ibara mbalimbali za Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ilifanya Mkutano wa Kusikiliza Maoni ya Wadau *(Public Hearing*) tarehe 29 Mei, 2023 ili kupokea maoni yao kuhusu Muswada huu. Aidha, Kamati ilipokea maoni kwa njia ya mtandao kutoka kwa watu na makundi mbalimbali ya wadau ambao hawakuweza kufika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru wadau wote waliotoa maoni yao ili kuuboresha Muswada huu na nichukue fursa hii kuwatambua kama ifuatavyo: -

1. The Tanganyika Law Society
2. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC)

3. Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT)
4. Taasisi ya TWAWEZA
5. Wanafunzi wa Sheria kutoka Vyuo Vikuu mbalimbali; pamoja na
6. Watu binafsi kutoka maeneo mbalimbali nchini

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya muswada kwa kuzingatia maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kwa kuzingatia maoni ya wadau. Mnamo tarehe 1 Juni, 2023 Kamati ilikutana tena na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye alijibu hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati kuhusu ibara mbalimbali za Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, nilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kukujulisha rasmi kwamba Kamati imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

### 2.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilichambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2023]* ukiwa umegawanyika katika Sehemu Kuu Tisa (9) na unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria Nane (8) kwa madhumuni ya kuondoa mapungufu au kutatua changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa Sheria hizo. Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni zifuatazo: -

(a) Sheria ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi, Sura ya 269;

(b) Sheria ya Huduma za Habari, Sura ya 229;

(c) Sheria ya Bohari ya Dawa, Sura ya 70;

(d) Sheria ya Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa, Sura ya 419;

(e) Sheria ya Reli, Sura ya170;

(f) Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania, Sura ya 277;

(g) Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370; na

(h) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inayohusu masharti ya utangulizi, inajumuisha **Ibara ya 1** inyohusu jina fupi na **Ibara ya 2** inayoeleza marekebisho yanayofanyika katika sheria mbalimbali.

**2.2. Sheria Zinazofanyiwa Marekebisho na Maudhui Yake**

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi, Sura ya 269 *[The Amendment of The Architects and Quantity Surveyors (Registration) Act, (CAP. 269)]***. Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya 3 hadi Ibara ya 15 ya Muswada. Marekebisho katika sehemu hii ujumla yanalenga kupanua wigo wa fani na huduma zinazotolewa katika taaluma ya ubunifu wa majengo na ukadiriaji majenzi pamoja na kuongeza fursa za ajira katika tasnia hii.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Huduma za Habari, Sura ya 229 *[Amendment of The Media Service Act, (CAP 229)]***. Kamati ilielezwa kuwa Marekebisho yanayopendekezwa katika sehemu hii yanalenga kumwondolea Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Habari, jukumu la uratibu wa matangazo yote ya Serikali, na pia kuiwezesha Serikali kuwa na uhuru wa kuchagua chombo cha Habari itakachokitumia kwa ajili ya matangazo, kwa kuzingatia nguvu ya ushindani katika soko kwa kufuta aya (l) ya kifungu cha 5.

Aidha, Muswada unapendekeza kufutwa kwa kifungu 38(3) cha Sheria ya Habari kilichoweka masharti ya mtu kushtakiwa kwa makosa ya Kijinai ama madai pale anapochapisha taarifa

zinazodhaniwa kuwa na uhuru usioweza kuingiliwa (*absolutely priviledged*) kwa madhumuni ya kuongeza haki ya uhuru wa maoni.

**Mheshimiwa Spika**, Vilevile Muswada unapendekeza marekebisho kwenye vifungu vya 50 hadi 55 na vifungu vya 63 na 64 kwa madhumuni ya kuhakikisha kwamba wanahabari wanafurahia haki yao ya uhuru wa maoni, haki ya kupata Habari na uhuru katika kazi zao za uhariri bila kuwa na woga wa adhabu za kijinai. Mapendekezo hayo, Pamoja na mambo mengine, yanalenga kuwaondoa wanahabari katika makosa yanayohusiana na kashfa za kjinai, makosa mabayo kwa kawaida yanaangukia katika utaratibu wa mashauri ya madai. Aidha, mapendekezo ya marekebisho ya vifungu hivyo yanaenda sambamba na kuondoa adhabu kwa wamiliki wa mitambo ya uchapishaji, ambao katika hali ya kawaida hawana uwezo wa kudhibiti maudhi yanayochapishwa katika mitambo hiyo ya uchapishaji.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya **Sheria ya Bohari ya Dawa, Sura ya 70 *[Amendment of The Medical Stores Department Act, (CAP. 70)]*.** Sehemu hii inahusu ibara ya 26 na 27 ambapo Ibara ya 26 inaeleza kuwa, sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Bohari ya Dawa Sura ya 70 ambayo inajulikana kama sheria mama (*The Principal Act*), Ibara ya 27 inapendekeza marekebisho kwenye kifungu cha 6 kwa kufuta kifungu kidogo cha (1) ambacho kinahusu muundo wa Bodi. Marekebisho yanapendekeza muundo wa Bodi kuwa na mwenyekiti atakayeteuliwa na Rais na wajumbe nane watakaoteuliwa na waziri ambao wametajwa kwa mujibu wa vyeo vyao au mwakilishi wake. Lengo la marekebisho hayo ni kuleta ufanisi katika Bodi kwa kuleta uwiano thabiti wa Bodi na kuhakikisha utekelezaji bora na Madhubuti wa Bohari ya Dawa.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Tano ya Muswada inahusu marekebisho ya **Sheria ya Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa, Sura ya 419 *[Amendment of The National Leaders Funeral Act, (CAP. 419]*.** Sehemu hii ya Muswada inahusu Ibara ya 28 hadi 37. Marekebisho haya yanalenga kuweka bayana na kutofautisha mamlaka

zinazopaswa kutoa matangazo ya vifo vya Viongozi wa Kitaifa na Viongozi Mahususi. Aidha, Marekebisho haya yanapendekeza Katika Ibara ya 36 ya Muswada kuhamisha mahali pakutolea heshima za mwisho za kiongozi wa Kitaifa ama Kiongozi Mahususi kutoka Uwanja wa Taifa wa Dar es salaam na kuhamia Dodoma.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Sita ya Muswada inahusu marekebisho ya **Sheria ya Reli, Sura ya 170 *[Amendment of the Railways Act, (CAP. 170]***. Sehemu hii inahusu Ibara ya 38 na 52. Marekebisho haya yanalenga katika Ibara ya 46 kuweka sharti kwa mtu mwenye nia ya kutumia maeneo ya reli kuomba kibali kwa shirika na kulipa ada pamoja na gharama zinazohusiana na matumizi hayo, Ibara ya 52 inapendekeza kuongeza kifungu cha 108 (5) kinachoweka masharti kwa mtu yeyote mwenye nia ya kuomba Shirika kujenga makutano ya reli na barabara *(level crossing)* kwa matumizi binafsi au ya umma kupata kibali cha shirika na kutoa gharama za ujenzi na ukarabati kwa gharama zake mwenyewe.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Saba ya Muswada inahusu marekebisho ya **Sheria ya Taasisi ya Utafiri wa Misitu Tanzania, Sura ya 277 *[(Amendment of the Tanzania Forestry Research Institute Act, (CAP. 277)]***. sehemu hii inapendekeza kufanya marekebisho katika ibara ya 53 hadi 65 ambapo ibara ya 53 ya Muswada inaeleza kuwa Sehemu hii itasomwa kwa pamoja na Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania, Sura ya 277. Pamoja na mambo mengine katika sehemu hii, Ibara ya 58 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 8(4) cha Sheria kwa kujumuisha ufugaji wa nyuki kuwa sehemu ya shughuli za kitafiti zitakazofanywa na taasisi kwa kutungiwa kanuni na Waziri mwenye dhamana kwa kushauriana na Bodi.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Nane ya Muswada inahusu marekebisho ya **Sheria ya Msajili wa Hazina (Mamlaka na Majukumu Yake), Sura ya 370 *[Amendment Of the Treasury Registrar (Powers and Functions) Act, (CAP. 370]***. Sehemu hii inahusu ibara ya 66 na 67. Ibara ya 66 inaeleza uhusiano kati ya sheria mama na marekebisho yanayopendekezwa kuwa marekebisho yatasomwa pamoja na sheria mama. Ibara ya 67

inapendekeza kufuta neno" *finance*" lililopo katika tafsiri ya neno" minister" na kuweka maneno" *public investments*" lengo ni kuhamisha ofisi ya Msajili wa Hazina kutoka wizara ya Fedha kwenda wizara ya Uwekezaji

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Tisa ya Muswada inahusu marekebisho ya **Sheria ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148 *[Amendment of The Value Added Tax, Act (CAP. 148)].*** Sehemu hii inahusu ibara ya 68 na 69 ambapo ibara ya 68 inahusu uhusiano wa marekebisho yanayopendekezwa na sheria mama (The principal Act) kuwa zitasomwa pamoja. Ibara ya 69 inafanya marekebisho katika jedwali la Pili kwenye kipengele cha 22 kwa kufuta tarehe 30 Disemba,2022 na kuweka tarehe 30 Juni, 2026 ili kuongeza kipindi cha msamaha wa kodi kwenye huduma za kukodi ndege kwa lengo la kuruhusu sekta ya utalii kuendelea kuimarisha.

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Maelezo ya Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuuboresha muswada huu kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata.

### 3.2 Marekebisho ya Sheria ya Huduma za Habari, Sura ya 229 [Amendment of The Media Service Act, (CAP 229)]

**Mheshimiwa Spika**, Katika ibara zifuatazo Kamati ilipendekeza adhabu zilizowekwa zinaweka ukomo wa chini wa adhabu bila kuweka ukomo wa juu wa adhabu au kuweka ukomo wa juu bila kuweka ukomo wa chini wa adhabu. Ni maoni yetu kuwa adhabu hizi ziwekewe ukomo wa chini na wa juu ili kutunga sheria iliyo kamili na badala ya kuiachia mahakama jukumu la kuweka ukomo wa juu au wa chini wa adhabu. Kamati ilibaini kuwa katika mapendekezo ya adhabu hizo kwenye sheria hii inaweza kutumika vibaya kwa baadhi ya watu kupewa adhabu kubwa zaidi na wengine ndogo zaidi katika kosa lile lile hivyo kuathiri takwa la kikatiba kuhusu usawa mbele ya sheria, Ibara hizo ni: -

i) Ibara ya 20(b) haijaweka ukomo wa adhabu ya juu ya kifungo;

ii) Ibara ya 21(a) aya (a) na (b) haijaweka ukomo wa juu wa faini pamoja na kifungo;

iii) Ibara ya 21(b) aya (a) na (b) hazijaweka ukomo wa adhabu ya juu isipokuwa imetaja tu ukomo wa adhabu ya chini;

iv) Ibara ya 21(f) pia haijataja ukomo wa juu wa adhabu ya faini pamoja na kifungo isipokuwa imetaja ukomo wa chini peke;

v) Ibara ya 22 imetaja ukomo wa adhabu ya chini pekee bila kutaja ukomo wa adhabu ya juu ya faini na kifungo;

vi) Ibara ya 23 imetaja ukomo wa adhabu ya chini pekee bila kutaja ukomo wa adhabu ya juu ya faini;

vii) Ibara ya 24(a) na (b) zimetaja adhabu moja kwa moja bila kuwa na ukomo wa chini wala wa juu kwa faini pamoja na kifungo.

Aidha, Katika Ibara ya 25(b) ina makosa ya kiuandishi ambayo yatapoteza mantiki ya kifungu kwa kuwa sheria mama imeandika adhabu isiyopungua milioni ishirini na tano wakati marekebisho yameandika milioni ishirini. Inapendekezwa Ibara ya 25(b) ifanyiwe marekebisho kwenye mstari wa tatu kutoka juu kwa kufuta maneno "*twenty million shillings*" na badala yake kuandika "*twenty-five million shillings*".

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati na wamefanya mabadiliko Kwa kuzingatia ushauri wa Kamati. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kufuata ushauri wa Kamati kwa kuondoa makosa dhidi ya mtu na mtu yenye sura ya madai kuondolewa kwenye orodha ya makosa ya Jinai Pamoja na

adhabu zake hususan kwenye Ibara ya 25 inayorekebisha kifungu cha 64 cha Sheria.

### 3.3 Marekebisho Sheria ya Bohari ya Dawa, Sura ya 70 [Amendment of The Medical Stores Department Act, (CAP. 70)].

**Mheshimiwa Spika**, katika **Ibara ya 27** ya Muswada, Ni maoni ya Kamati kuwa uwakilishi wa sekta binafsi katika Bodi ni muhimu. Aidha, Kamati ilihitaji ufafanuzi utolewe katika ibara hiyo aya (f) ambayo imetaja sifa za wajumbe wengine watatu lakini haijaeleza watatoka wapi. Mheshimiwa Spika, Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati na wamefanya mabadiliko Kwa kuzingatia ushauri wa Kamati.

### 3.4 Marekebisho ya Sheria ya Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa, Sura ya 419 [Amendment of The National Leaders Funeral Act, (CAP. 419]

**Mheshimiwa Spika**, katika Ibara ya 29(4) ya Muswada, Kamati inapendekeza kufanya marekebisho yafuatayo, kufuta maneno "serving President" na kuandika maneno "former President who died while in office", lengo la maboresho haya ni kuipa kifungu maana inayokusudiwa. Mheshimiwa Spika, Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati na wamefanya mabadiliko Kwa kuzingatia ushauri wa Kamati.

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia muswada huu, naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb -**Makamu Mwenyekiti**
2. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb - Mjumbe
3. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb - Mjumbe

7. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Omar Issa Kombo, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Agnesra Lambert Kaiza, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Tumaini Bryceson Magessa, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Eliezer Mbuki Feleshi Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali Ndg. Onorius Njole, pamoja na watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**4.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama lilivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mhe. Joseph Kizito Mhagama (Mb)
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**
13 Juni, 2023

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa kusoma vizuri. Sasa tunaanza michango. Tunaanza na Mheshimiwa Sillo, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, anakuja Mheshimiwa Kandege, ajiandae Mheshimiwa Zedi.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Muswada huu wa Mabadiliko ya Sheria ya *PPP*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu. Nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa anayoifanya katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, Naibu Waziri, na timu nzima, kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kusimamia sera ya kifedha na ya kikodi katika nchi yetu. Vile vile nampongeza Mheshimiwa Jonas Mbunda, Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, pamoja na Wajumbe wengine wa Kamati ya Bajeti kwa kazi kubwa waliyofanya katika kuuchambua Muswada uliokuwa mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia maeneo matatu. Eneo la kwanza ni umuhimu wa miradi ya ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi. Naipongeza Serikali yetu, imeendelea kufanya kazi kubwa sana ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo pamoja na kutoa huduma za kijamii katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho haya yanayofanywa ya Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi *(PPP)* yatasaidia sana katika utekelezaji wa miradi mbalimbali, hasa miradi ya maendeleo ya kimkakati na kuipunguzia Serikali mzigo wa kibajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sekta binafsi kwa kiasi kikubwa hujihusisha na shughuli za kibiashara, hivyo ili kuipunguzia Serikali yetu mzigo wa kibajeti, basi ile miradi yote ambayo ina sura ya kibiashara ni vyema sasa sekta binafsi na sekta ya umma

ikaungana katika kutekeleza miradi yote yenye sura ya kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu ijielekeze katika ku-*finance* ile miradi ya huduma za kijamii na hii itasaidia sana kupunguza mzigo wa Serikali wa kufanya kila jambo. Kwa hiyo, kwa kuhusisha sekta binafsi, kwa maana ya miradi hii ya ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi, basi ichukue na sekta hii. Pia Serikali yetu ijielekeze kwenye miradi isiyo na mvuto au sura ya kibiashara ili ijikite zaidi katika kutoa huduma kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni bajeti ya Mfuko wa Kuchochea Miradi ya Ubia, yaani ya *PPP* ambayo ni *PPP Facilitation Fund*. Mfuko huu una jukumu kubwa sana la kuwatafuta na kuwandaa wadau watakaoshiriki katika miradi ya *PPP*. Miradi hii ya *PPP* siyo ya muda mfupi, kwa hiyo, mfuko huu lazima uwe na uwezo mkubwa ili kuandaa utaratibu mzima wa kuwapata wadau wa kushiriki katika miradi mbalimbali ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya mfuko huu kwa mwaka wa fedha huu tunaokwendanao 2023/2024, umetengewa Shilingi bilioni 2.8. Kwa kuzingatia majukumu ya mfuko huu, na kwa kuzingatia kuwa miradi mingi ya *PPP* inachukua muda mrefu, naiomba sana Serikali iongeze bajeti katika mfuko huu ili basi wapate muda wa kutosha wa kuandaa wadau mbalimbali watakaoshiriki katika miradi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Mpango wa Maendeleo ya Miaka Mitano 2021/2022 - 2025/2026, yako malengo ambayo tumeweka, kwamba miradi hii ya *PPP* iweze ku-*mobilize* asilimia 17 ambayo ni sawasawa na trilioni 21 katika kutekeleza mpango mzima wa miaka mitano. Hivyo, kuna umuhimu mkubwa sana wa Serikali kuona namna bora ya kuongeza bajeti katika mfuko huu ili iweze kupata miradi ya kutosha katika kutekeleza majukumu haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni mitaji ya miradi ya *PPP*. Kabla ya marekebisho ya sheria hii iliyoletwa leo na Serikali, kanuni za awali zilikuwa zinataka, ili mbia aweze kushiriki katika miradi ya ubia baina ya Serikali na sekta binafsi, alikuwa lazima awe na miradi *minimum* ya *20 million dollars* ambayo ni sawasawa na Shilingi bilioni 45. Kiwango hiki kilikuwa kinawatenga Watanzania wengi sana kushiriki katika miradi hii ya ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kuipongeza Serikali, katika marekebisho yaliyofanyika sasa imefanya kazi nzuri sana, kwamba sasa Mtanzania mwenye mtaji chini ya dola milioni 20 atashiriki kwenye miradi midogo ya ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi, lakini kwa miradi mikubwa basi ni kuanzia dola milioni 20 na kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni hatua kubwa sana na jambo hili litaunganisha Watanzania wengi kushiriki katika miradi hii ya ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi. Vile vile jambo hili litachangia sana katika kukuza uchumi wa Taifa letu, kukuza pato la Taifa na kupunguza matatizo ya nchi ya *balance of payment* au *balance of trade* na nchi ambazo tunafanyanazo biashara hapa duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana kwa kupata fursa. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kandege, wajiandae Mheshimiwa Zedi na Mheshimiwa Katimba.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niwe mchangiaji wa pili katika Muswada ulioletwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kunijalia afya na kuniwezesha kusimama leo nikiwa na afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee, naomba nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa maono yake na kazi kubwa anayofanya kwa Watanzania. Naomba pia niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu yote ya Wizara ya Fedha ambao hakika wametuletea Muswada huu katika kipindi ambacho ni muafaka, kipindi ambacho Tanzania tunatakiwa kukimbia. Tumetembea kwa muda mrefu, ni wajibu wetu tuanze kukimbia kama Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie katika maeneo mawili kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni hili ambalo Mheshimiwa Mwenyekiti amelisemea, nasi kama Kamati tumesema, kuhusiana na *PPP Facilitation Fund* kwa maana ya kifungu cha 10(a) na (b). Katika mpango wetu wa miaka mitano, sisi kama Taifa tunatarajia mchango kutoka katika *Private Sector* kama *engine* ya *growth of economy* isipungue Shilingi trilioni 21. Ili mchango huu uweze kupatikana kwa matarajio na matamanio yetu, ni ukweli usiopingika kwamba lazima *PPP Center* iwe na uwezo wa kufanya maandiko, kufanya *feasibility study* ili maandiko hayo yaweze kwenda kuuzwa na ndipo tutakapoweza kupata hiyo Shilingi trilioni 21 ikichangiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipongeze nia njema ya kuhakikisha kwamba kituo hiki kinakuwa kituo cha kimahiri, umahiri ambao utahakikisha maandiko yanachambuliwa vizuri, yale yote ambayo yanaonekana kwamba yana *appetite* ya kibiashara, basi ni wito niutoe kwa Watanzania, tuanzie sisi Watanzania, sekta binafsi kwa kupitia *TPSF* ni wakati muafaka baada ya marekebisho ya sheria hii. Yale yote ambayo yalikuwa yanaonekana kama makandokando, hakika Serikali ya Mheshimiwa Samia imeenda kuyaondoa, ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba tunachangamkia fursa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matarajio makubwa mchango kutoka kwenye sekta binafsi utaanza kuonekana. Ni wakati umefika kwa Watanzania, tuache kuwa watazamaji, tuhakikishe

tunachangamkia fursa ambazo Mwenyezi Mungu ameziweka katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya marekebisho ya Muswada huu ambao naamini leo Wabunge watakwenda kuupitisha kwa kishindo na utekelezaji wake uanze, naiomba Serikali kwa kushirikiana na *PPP Center,* Wizara ya Uchukuzi na Uwekezaji muanze katika maeneo yafuatayo: la kwanza, ili Bandari yetu ya Dar es Salaam iweze kufanya kazi ambayo sisi wote tunakusudia Watanzania, ni pale ambapo tuta-*address* mizigo mingi ambayo inakwenda Kongo ya *DRC* kwenda Katanga kwa kupitia Ziwa Tanganyika, kwa kupitia *Kasanga Port,* sasa mkatafute wabia ambao watakuwa tayari kujenga barabara upande wa pili wa Kongo ili twende Kongo ya Lubumbashi ambako asilimia zaidi ya 80 ya mzigo wote wa Kongo unapatikana kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mafanikio ambayo natarajia tuyapate kwa haraka ni kuanza kuchuma haya matunda ambayo ni *low hanging fruits.* Kwa utaratibu huu na maboresho ambayo yanakwenda kufanyika, naiomba Serikali, pasi na kuchelewa, Wizara ya Fedha, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, kwa kushirikiana na hiki Kituo cha *PPP Center,* twende duniani tukatafute watu ambao wana fedha kwa sababu mradi huu *economically* unaonekana kwamba ni *viable*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa malori ambayo yanalazimika kupita Zambia kwenda mpaka Kasumbalesa kule, kila yanapopita Zambia yanaacha dola 700 kwa kila *truck* moja. Sasa ni hakika kwamba tukifungua njia hii kwa kupitia Kasanga, tukichaji malori dola 300, hakika kwanza tutakuwa tumepunguza umbali kwenda huko ambako tunafuata mzigo, wakati huo huo sisi kama Taifa fedha hizi zitaingia na mradi huu unaweza kulipa kwa muda mfupi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumaliza eneo hilo ambalo nashauri tuanze nalo, ni vizuri pia Serikali mkafikiria namna ya maboresho katika reli yetu ya *TAZARA* na kipande cha kutoka Tunduma kwenda *Kasanga Border*. Naamini kuna watu

watakuwa wako tayari kuwekeza katika kipande hiki. Hakika tutakuwa tunafungua Taifa kwa ujumla, Tanzania yetu itakuwa imeunganishwa na baada ya hapo tutahamia kusini kule, nako kuna *appetite* kwa wafanyabiasra kuwekeza katika kipande hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuipongeza Serikali kwamba imeleta maboresho ya sheria hii kwa wakati muafaka, tuchangamke Watanzania, tuache kupiga maneno twende kutenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Zedi, atafuatiwa na Mheshimiwa Katimba, jiandae Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia kwenye Sheria hii ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ya Mwaka 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita kwenye Sheria ya Reli, Sura 170. Marekebisho haya ambayo yanakuja na hasa kweny,e Ibara ya 42 ya Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, kwenye Sheria ya Reli Sura 172, Muswada unapendekeza marekebisho ya Sheria ya Reli iliyopo sasa ambapo marekebisho haya yatatoa fursa kwa watu binafsi na kampuni binafsi kutumia miundombinu ya reli kutoa huduma za uchukuzi wa mizigo na abiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana ya marekebisho haya ni kwamba, kwa mfano sasa hivi kwenye sekta ya Barabara, tuna barabara ambazo ni za Serikali lakini juu ya barabara hizo yanapita mabasi ya watu binafsi, kama Ally's, Shabiby, Kimbinyiko, yanapita kwenye barabara za Serikali. Sasa sheria hii inakwenda kulileta jambo hilo kwenye miundombinu ya reli. Kwamba reli itaendelea kumilikiwa na Serikali kama miundombinu husika, lakini juu ya reli sasa sekta binafsi wanaruhusiwa kutumia fursa hiyo kutoa huduma za uchukuzi wa mizigo pamoja na abiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni fursa kubwa sana. Wote tunafahamu kwamba mwelekeo wa sera zetu za kiuchumi na kijamii, sasa ni kutoa fursa kwa sekta binafsi zishiriki kikamilfu katika uchumi wetu. Sasa hili ni eneo mojawapo. Badiliko hili la sheria linakwenda sambamba na mabadiliko hayo na mwelekeo huo wa sera zetu za kiuchumi za kuruhusu watu binafsi na sekta binafsi kushiriki katika uchumi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tutakwenda kushuhudia kwamba kwenye miundombinu ya reli hii, kwa mfano kuna Reli ya *SGR* ambayo inajengwa sasa hivi, kwa mfano, labda kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza ambapo unapita Bukene, Jimboni kwangu, tutakwenda kushuhudia kwa siku kunaweza kuwa hata na treni tatu au nne zote zinatoka Dar es Salaam kwenda Mwanza, lakini treni hizi zinamilikiwa na watu binafsi tofauti tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hii kwanza italeta ushindani wa ufanisi kwa sababu kila mwendeshaji wa treni atataka kupata abiria na mizigo ya kusafirisha. Kwa hiyo, kwa vyovyote atalazimika kuongeza ufanisi ili aweze kupata biashara. Kwa hiyo, hii ni fursa kubwa na ni badiliko kubwa sana la sheria ambalo linakwenda kusisimua uchumi hasa kwenye sekta hii ya usafirishaji, hasa kwenye sekta ya reli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo linafanyiwa mabadiliko kwenye Sheria ya Reli ni eneo ambalo kwa sheria ya sasa Shirika la Reli haruhusiwi kufanya baadhi ya shughuli za kibiashara, lakini mabadiliko haya yanakwenda kuliruhusu Shirika la Reli sasa kuinga kwenye shughuli za *real estate,* kufanya maendelezo na kuendesha miradi ambayo ina mwelekeo wa ki-*real estate*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Reli lina *nature* ya kuwa na maeneo ambayo ni stesheni kubwa katika maeneo mbalimbali. Maeneo mengine taarifa zipo, hata sisi kama Kamati tulipata fursa ya kukutana na wenzetu wa Shirika la Reli na baadhi ya mifano ni kwamba nchi nyingine unakuta mpaka kwenye asilimia 40 ya mapato ya Shirika la Reli hayatokani, na siyo lazima

yatokane na reli yenyewe, yanatokana na biashara nyingine ambazo Shirika la Reli linaruhusiwa kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi Shirika la Reli liko *limited*. Kuna baadhi ya biashara ambazo haliruhusiwi kufanya, lakini kwa sheria hii inakwenda kufungua mlango, kwamba Shirika la Reli ama lenyewe au kwa kuingia ubia na watu binafsi, linaruhusiwa sasa kutumia maeneo yake kujenga miradi kwa mfano *shopping malls,* mabenki, maduka, migahawa na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri Shirika la Reli lina maeneo ambayo ni *prime locations.* Stesheni kama za Dar es Salaam, Morogoro, Tabora, Bukene, Mwanza, ni maeneo ambayo ni *prime locations.* Kwa hiyo, Shirika la Reli kwa sheria hii sasa litaruhusiwa kuyatumia majengo haya, ama wao wenyewe kujenga hiyo miradi mikubwa. Hii itafanya sasa maeneo yetu ya stesheni kuwa *busy* muda wote, siyo lazima wakati treni inapopita tu, lakini kama kutakuwa na *shopping malls,* kama kutakuwa na ma-*godown,* kwa hiyo muda wote kutakuwa *busy* sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiunga mkono Sheria hii na ni washawishi Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa sababu kiuchumi, kijamii ni mabadiliko ambayo yanakwenda kuongeza chachu. Pale Bukene kwa hii *SGR* Bukene inakwenda kuwa *station* ambayo ni *logistic hub, station* ambayo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mizigo itashushwa na kupakuliwa pale. Kwa hiyo, naunga mkono hoja na nawashawishi kwamba mabadiliko yapokelewe, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zainab Katimba, Mheshimiwa Nusrat jiandae, Mheshimiwa Magessa atajiandaa, Mheshimiwa Ndaki, jiandae Mheshimiwa Naibu Waziri.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Marekebisho haya kimsingi yamekuja kuondoa mapungufu ambayo yalijitokeza katika utekelezaji wa Sheria hii ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi. Kimsingi masharti yaliyokuwepo kwenye Sheria ile kwa kiwango kikubwa yaliweza kuathiri ushiriki wa Sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa utaratibu wa ubiya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye ukurasa wa 13 wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020/2025, Ibara ya 18(b)(5) inasema kwamba CCM itaielekeza Serikali kuweka sera madhubuti za uchumi ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kutumia mfumo wa ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi *(Public Private Partnership) (PPP)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kimsingi suala hili ni la kuleta Muswada wa kufanya marekebisho kwenye Sheria hii ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi watu huwa wanachanganya kati ya ubinafsishaji na ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi *(Privatization* na *Public Private Partnership)* lakini vitu hivi ni viwili tofauti. Kwa mfano tukizungumzia *Public Private Partnership* yaani ubia huu kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, tuseme Serikali ina miradi mingi ya maendeleo ambayo Serikali ikisema itumie fedha zake itatumia muda mrefu sana ama inaweza ikaongeza deni la Serikali kwa maana ya kutegemea mkopo. Kwa hiyo, mkakati mbadala unaofanyika, miradi ile inatangazwa na wawekezaji wanaweza kuja na mitaji yao, uzoefu wao, wanaweza kuja na utaalam, wanaweza kuja kuwekeza kwenye ile miradi mahsusi kwa ajili ya kutoa huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hiyo inakuwa inaendeshwa na yule mwekezaji, lakini wananchi wanaweza wakawa wanatoa gharama ile ile kwa ajili ya ile huduma ambayo wangetoa kama

mradi ule ungekuwa umejengwa na Serikali. Baada ya muda fulani ambapo kwenye mkataba unakuwa umekubaliwa, mradi ule, yule mwekezaji anakuwa amepata faida yake na amerudisha mtaji wake na ule mradi sasa utakabidhiwa kwa Serikali ili uendelee kuendeshwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi hiki chote ule mradi bado unakuwa ni mradi wa umma. Unakuwa hamna hata kipindi kimoja mmiliki wa ule mradi unakuwa umetoka kwenda kwa sekta binafsi. Mradi unakuwa ni mali ya umma kwa hiyo hii ni mbinu nzuri sana ya kupata mitaji kwa ajili ya utekelezaji wa miradi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwenye Sheria ile tuliyokuwa nayo yaani *The Public Private Partnership Act* tuliyokuwa nayo ambayo sasa hivi tunaifanyia marekebisho kulikuwa na changamoto kadha wa kadha. Kwanza kwenye Sheria hii na ukienda kwenye Ibara ya 12 ya Muswada inazungumzia masuala ya utatuzi wa migogoro. Yaani Ibara ya 12 ya Muswada imeenda kufanya marekebisha kwenye kifungu cha 22 cha Sheria na sasa hapo mwanzo utatuzi wa migogoro ulikuwa haujatengenezewa sharti ya kwamba mnaweza kutumia mahakama za kimataifa lakini kwa marekebisho haya kwenye Ibara hii sasa mwekezaji atakuwa ana uhuru zaidi wa kuweza kuwekeza kwa sababu kwenye utatuzi wa migogoro atakuwa ana haki ya kutumia aidha Sheria za *arbitration* za Tanzania au Sheria zinazotambulika za *arbitration* za kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni jambo ambalo wawekezaji wengi walikuwa wanatamani kuliona lipo kwenye masharti ya Sheria hii. Kwa hiyo, ibara hii ya 12 imekwenda kuleta hayo marekebisho ambayo kimsingi yatavutia wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye Muswada huu ukienda Ibara ya 10 ya Muswada imeenda kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 18(a) cha Sheria hii ya *PPP* ambapo imeanzisha na imeweka sharti la yule mbia anayeshinda zabuni ya utekelezaji wa mradi wa *PPP* aunde Kampuni mahsusi kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa kifungu hiki au marekebisho haya ni kwamba sasa huyu mwekezaji kwa sababu atakuwa na kampuni yake achanganye mahesabu ya kampuni yake akachanganya na mapato yale yatakayokuwa yanakusanywa kwenye mradi huu wa *PPP*. Kwa hiyo, kimsingi ni kulinda maslahi ya nchi na kulinda mapato yatakayotokana na mradi huu wa *PPP*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukienda tena kwenye Ibara ya 9 ya Muswada ambayo inaenda kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 15 cha Sheria. Kifungu hiki kinafanya marekebisho na kupunguza yale masharti magumnu ya ununuzi wa mbia na hasa kwenye miradi ile ambayo inaibuliwa au inabuniwa na wabia. Kwa sababu miradi kwenye *PPP* iko miradi ya aina mbili kuna ile *solicited* ambayo imeibuliwa na Serikali lakini kuna *unsolicited* ambayo imebuniwa na mbia kutoka kwenye sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sasa kifungu hiki hapo awali kilikuwa kinaweka sharti kwenye ile miradi ambayo imeibuliwa na mwekezaji, yule mwekezaji lazima atoe asilimia 3 ya jumla ya gharama ya ule mradi anaotaka kutekeleza, aitoe kama *down payment* kitu ambacho kilikuwa kinapunguza mtaji wa mwekezaji katika kuwekeza katika huo mradi. Kwa hiyo, masharti ya ibara hii ambayo inaenda kurekebisha kifungu cha 15 imeondoa sharti hilo lakini pia imeweka masharti rahisi zaidi katika masuala ya ununuzi wa mbia katika miradi iliyobuniwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, haya mabadiliko yote kimsingi yanaenda kubadilisha eneo hili la *PPP* lakini kuvutia wawekezaji kuja kuwekeza katika miradi Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa Jumla kwa Serikali, pamoja na marekebisho haya mazuri, naiomba sana Serikali iweze kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu kwenye miradi kwa sababu *feasibility study* ndio inatengeneza msingi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, ahsante.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** …wa wawekezaji kuvutiwa na kuja kuwekeza katika miradi yetu hapa Tanzania, Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri. Haya sasa namwita Mheshimiwa Nusrati, halafu anafuatia Mheshimiwa Magessa, Mheshimiwa Ndaki, ajiandae Mheshimiwa Nape.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye marekebisho ya Sheria mbalimbali. Nitajikita kwenye Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 Sura ya 229 ambayo ndio Serikali inafanyia marekebisho. Kwanza niipongeze sana Serikali kwa kuona umuhimu wa kusikiliza maoni ya wanahabari na wadau wa tasnia ya habari lakini pia na watanzania wote ambao walipiga kelele baadhi ya vifungu kwenye Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi nakubaliana na maoni ya kamati kuhusiana na marekebisho yaliyofanywa lakini pia naunga mkono taarifa ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusiana na sehemu ambazo wamesema wamezifanyia marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda tu kwa kukazia, Serikali kwa kuona umuhimu wa maoni ya watu wamefanya marekebisho kwenye vifungu tisa ambavyo vilikuwa na utata lakini kwenye vifungu hivi tisa vifungu vitatu ndio vifungu ambavyo tumeviona kwamba ni *tangible* na nitavielezea baadae lakini vifungu sita vilivyobakia ni vifungu ambavyo vimezungumzia adhabu. Ni jambo zuri kwa Serikali kuona kwamba kulikuwa kuna nia ya kupunguza adhabu ya makosa kwenye masuala ya tasnia ya habari kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, vifungu sita vyote vinahusiana na masuala ya kupunguza adhabu ni jambo zuri na tunawapongeza. Lakini vifungu vitatu pia na vyenyewe ni

*tangible* na nitavielezea kwa sababu ya umuhimu wake kwa sababu vilipigiwa makelele na Serikali imesikia. Kuna kifungu cha tano ambacho kimemwondolea mamlaka Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Habari ambaye kimsingi alikuwa anapewa mamlaka makubwa sana. Kumwondolea Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Habari jukumu la kuratibu matangazo yote ya Serikali, kuiwezesha Serikali kuwa na uhuru wa kuchagua chombo cha Habari ambacho kitashirikiana nacho kuzingatia na ushindani wa vyombo vya habari. Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo tulilipigia kelele kwa sababu lilikuwa linampa mamlaka makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kifungu cha 64 pia kimefanyiwa marekebisho ambacho kimeondoa adhabu kwa wamiliki wa mitambo ya kuchapisha kwa sababu kwa kweli hawana mamlaka, uwezo wa moja kwa moja kuchagua nini kinachapishwa kwenye mitambo yao, kwa hiyo, ni jambo zuri na nifikiri hata watu ambao wanamiliki mitambo ya kuchapisha wamefurahi kwa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu kingine ambacho kimefanyiwa marekebisho na Serikali ni kifungu cha 38(3) ambacho kinalenga kuongeza wigo wa watanzania wote wakiwemo wanahabari kutoa maoni. Kwa sababu kuna makosa ambayo yalikuwa yanaonekana kama ni makosa, kwa hiyo, imefuta adhabu kwa mtu ambaye atachapisha taarifa ambayo ilikuwa inaonekana kwamba inaingilia uhuru usiozuilika wa watu, kwa hiyo, ni kitu kizuri tunapongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nielezee mambo ambayo naona yameachwa ambayo pengine yalitakiwa yawepo katika marekebisho haya. Jambo la kwanza ambalo limeachwa kwa kweli ambalo ni la msingi kwa ajili ya kurekebisha na kuweka mazingira mazuri kwa watu wetu wa tasnia ya habari kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo moja ambalo halijaguswa kabisa ni kuhusiana na leseni. Sheria mpaka sasa hivi ambavyo ilivyo inataka kila mwaka wamiliki wa magazeti wasajili leseni kila mwaka, *annually licensing* ya magazeti, kitu ambacho kinazuia

hawa ambao ni waandishi wa habari kufanya kazi zao wakiwa wana-*confidence* ni kama kinawondolea *confidence*. Kwa hiyo kifungu cha 5(e), 8 na 9 vyote vinalazimisha wamiliki wa magazeti kusajili kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa maoni yangu, kwanza tuondoe neno *license* badala yake tulibadilishe na *registration*. Kwa hiyo, tuwe na usajili ambao tunaweza tukakubaliana hata kama ni *five years*, au hata kama ni *ten years* lakini watu watajiwe gharama ya kusajili magazeti ili wapate uhuru wa kufanya kazi zao za uhandishi kwenye magazeti kwa muda ambao wanajua wameshafanya usajili na Serikali inajua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwaka mmiliki wa magazeti anatakiwa akasajili. Kwanza hapo kuna gharama, kuna *implication* ya *cost* ambapo kila mwaka anavyosajili analipa lakini pia hii ni sehemu moja wapo ambayo sisi tunaamini kwamba inaweza ikasababisha watu wengine ambao kwa namna moja au nyingine wataonekana wana ukali fulani wakaondolewa wakawa *fenced out.* Kwa hiyo ni kama *technique* fulani ambayo kiukweli tunashauri muone namna gani, kwa sababu kwa kweli magazeti yatapungua. Kwa sababu wangapi wata-*comply* nayo na mnajua kwamba ni vijana wengi sana wamejiajiri kwenye vyombo hivi ikiwemo magazeti. Watu wana kalamu zao wanaandika watu wanamiliki ni biashara na kimsingi tunahitaji watanzania waweze kumiliki uchumi, hii ni sehemu moja wapo ya *income* za watu na nafikiri kuna haja ya kuangalia kwa sababu hatuviziani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo limeachwa ni mamlaka ya Waziri kuzuia machapisho kutoka nje. Nchi yetu ni nchi huru kama tulivyokubaliana kwa hiyo, sioni kama ni busara kuzuia machapisho mengine yenye lengo la kujifunza kwa sababu ya *ministerial capacity* ambayo Waziri amepewa kuzuia machapisho kutoka nje. Kwa hiyo, sioni kama ni busara sana, lakini pia kitu kingine ambacho nishauri sana wakiangalie ni pamoja na hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesema waondoe ukomo wa adhabu kwa sababu, sasa hivi ilivyo ni kwamba vile vipengele sita vilivyofanyiwa marekebisho, vyote vimetaja adhabu juu na chini lakini ni bora sana. Kuna kifungu kimoja kimeandikwa vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwa sababu mwenendo wa kesi ni tofauti na sisi tunavyozungumza, ukimwekea mtoa hukumu kwenye Sheria kwamba anatakiwa atoe hukumu kwa kosa hilo kwa kutaja faini lakini pia ukamwekea kifungo kisichopungua miaka mitatu na kisichozidi miaka mitano, wakati mwingine mwenendo wa kesi unaweza kufanya ukaona kwamba hili kosa sio la miaka mitatu lakini Sheria inamlazimisha mtoa hukumu ahukumu *minimum three years.* Kwa hiyo. nashauri baada ya kusema *minimum three years* na *maximum* ni bora ikatajwa *maximum* au ikatajwa kama ilivyotajwa kwenye kifungu hiki hapa nakisoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 63(1) nina kinukuu kwa kingereza kama kilivyoandikwa na ninashauri kwa sababu kipo kwenye Sheria hii hii na Serikali ndio imekiandika, nashauri vifungu vyote vinavyohusu adhabu viandikwe hivi, *"commits an offence and upon conviction shall be liable to fine of three million shillings or five million shillings and imprisonment of five years or two years or both"* hakuna *minimum* hakuna *maximum*. Nashauri vifungu vingine vyote vinavyofanana na hivi kwenye adhabu viandikwe hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inatoa uhuru kwa anayetoa hukumu kwa sababu sio lazima kwa kuwa Sheria nyingine zimeandikwa hivi na hii iandikwe hivi, kwa sababu tunaweza kuchagua namna bora ya kuandika Sheria nyingine ambazo zikawa nzuri, sio lazima tufate vya zamani na kwa sababu hiki kifungu ni cha kwenye Sheria hii. Sasa kwanini vifungu vingine vyote vilivyotaja adhabu ambavyo niliviorodhesha hapa vingeandikwa hivi ingekuwa na picha nzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kitu kingine ambacho kimeandikwa bado kipo humu na hakijajadiliwa sio katika *amendment* ni *defamation* kwenye Sheria hii, kashfa bado ni kosa

la jinai. Kitu ambacho ni kinyume kabisa na viwango vya kimataifa vya Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 35 na 36 kwenye Sheria hii ya Huduma za Habari inaeleza kashfa kama kosa la jinai na ninashauri kiangaliwe upya. Kipitiwe kwa sababu kwanza au kiondolewe kwa sababu *internationally* kashfa ama *defamation* sio kosa la jinai ni madai kama madai mengine ambayo tutaenda tu-*battle* mahakamani huko lakini sio kosa la jinai na kwa sababu ya tasnia hii ya habari hili jambo ni pana sana kwa upana wake tunaweza tusilizungumze hapa kwa sababu wakati mwingine kitu ambacho ni ukweli kinaweza kuchukuliwa kama ni kashfa kwa sababu mwandishi wa habari ameandika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo vingine tutaendelea kushauri…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** …lakini kimsingi niwapongeze sana Serikali kwa kuona umuhimu wa kufanya *amendment* japo kuna vitu wameviacha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Magesa, Mheshimiwa Ndaki jiandae, Mheshimiwa Nape jiandae.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipatia nafasi hii ya kupitia Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa mwaka 2023. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa fursa hii ambayo anatupatia ya kujadiliana mambo makubwa ya Sheria zetu na kupitisha sheria mbalimbali na marekebisho mbalimbali ambayo tunayafanya hapa. Nimpongeze Waziri wa Fedha kwa kuja na *PPP* lakini nimpongeze Mwanasheria Mkuu kwa kutuletea Muswada huu ambao una marekebisho ya Sheria takribani nane hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Sheria ya Usajili na Ubunifu wa Majengo na Wakadiriaji wa Majengo Sura ya 269 lakini tuna Sheria ya Huduma za Habari Sura 229, Sheria ya Bohari ya Dawa Sura 70, Sheria ya Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa Sura 419, tuna Sheria ya Reli Sura 170, Sheria ya Utafiti wa Misitu Tanzania Sura 277 lakini tuna Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina Sura 370 na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura 148.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana kwamba Bunge hili, nishauri tu hata kabla sijazungumza kwamba kama Kamati tumepitia, tumechukua muda mrefu kujadiliana juu ya Miswada hii ambayo imekuja na marekebisho makubwa tumeyafanya. Niwapongeze sana Mawaziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye amekuja na tumemhoji na tumefikia mahali ambapo tumekuja na kitu ambacho sasa naamini kwamba Wabunge wenzangu niwashawishi tu kwamba tufanye mabadiliko haya ili Sheria hizi ziende kutumika kwa ajili ya maendeleo ya watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita sehemu chache katika mabadiliko au marekebisho haya. Sheria ya Huduma ya Habari Sura 229; Ukipita kwenye Sheria hii utagundua kuna marekebisho makubwa yamefanyika kama walivyosema wenzangu ya kumpunguzia madaraka au mamlaka Mkurugenzi wa Idara ya Maelezo, kumpungizia juu ya jukumu la utartibu wa matangazo yote ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana kama walivyosema wenzangu kwamba alikuwa na madaraka makubwa na hivyo matangazo yote yalitakiwa yatoke kutoka kwenye kiti hicho cha Mkurugenzi Mkuu wa Habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini cha pili, vilevile imeeleza Serikali kuwa na uhuru wa kuchagua chombo gani kinaweza kutumika kufanya matangazo. Lakini kingine ambacho kimefanyika ni kwamba Muswada umependekeza kufuta kifungu namba 38(3) kilichokuwa kimeweka masharti ya mtu kushtakiwa kwa makosa ya kijinai. Hawa waandishi wa habari walikuwa

wanashtakiwa na makosa ya kijinai au ya madai pale tu ambapo anaonekana ameshughulika kutoa taarifa zinazodhaniwa kuwa zisizoweza kuingiliwa *(absolutely privileged)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kifungu hiko kinaenda kufutwa ili kuhakikisha kwamba hawa sasa wanapata haki ya uhuru wa maoni. Kwa hiyo, niseme tu wazi kwamba kuna haki ya uhuru wa maoni inakwenda kufanyika kwenye eneo hili. Waandishi wa habari wajiandae sasa kwa sababu haki hii imepanuliwa na marekebisho ya Muswada huu. Vile vile, mapendekezo ya marekebisho ya kwenye vifungu vya 50 hadi 55 na vifungu namba 63 na 64 ambavyo vinahakikisha wanahabari wanafurahia haki ya uhuru wa maoni yao. Kwa hiyo, niseme tu wazi, kama kuna mahali wanahabari waliona kwamba walikuwa hawana uhuru na haki ya maoni sasa wanakwenda kuipata baada ya marekebisho haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, walivyokuja walikuja na maoni takribani 21 lakini nimpongeze Waziri wa Habari kwamba haya yote 21 yamefanyiwa kazi na sasa hata yale ambayo yanaonekana kwenye Sheria hayajarekebishwa yatakwenda kwenye kanuni kufanyiwa marekebisho. Kwa hiyo, nimpongeze sana Waziri kwa hili. Lakini niipongeze vile vile kuja na Sheria hii ambayo sasa inakwenda kufanya watu wetu wawe na uhuru wa kutoa maoni yao na wananchi wapate habari kama ilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho nilitaka kusema hapa ni kile ambacho na wenzangu wamekwishakisema. Mtu ana mashine zake za kudurufu kutoa matangazo. Wakati anapewa adhabu na zile mashine nazo zinakuwa zimepewa adhabu kwa sababu wanasema nazo zimefungiwa ilhali mwenye mashine hizi hawezi kujua maudhui ya kile ambacho kinakuja kuchapishwa hapa. Kwa hiyo, kwenye Sheria hii inaonesha wazi kwamba sasa mashine zile hazitakuwa zimeingizwa kwenye hilo ambalo tunalisema. Kwa mazingira hayo maana yake ni kwamba wananchi hawa na wamiliki wa mali hizi wamepewa nafasi kubwa ya kuchapisha habari yoyote wakati mashine zao hazitaweza kufungiwa.

Mheshimiwa Naibu spika, lakini kingine kimesemwa ni habari ya leseni, kwamba leseni kwa nini inakuwa ya mwaka mmoja. Tumelihoji hili kwa nini mwaka mmoja? Kuna watu wana maduka yana thamani kule Kariakoo ya karibu bilioni moja wanakata leseni kila mwaka, sasa kwa nini hawa watu wasikate leseni kila mwaka? Lakini kitaalamu tu bado hoja ya leseni vile vile inaweza kuwa ni *investment*, *initial investment*. Kwamba kama *investment* ni kubwa tunaamini kabisa huyu leseni yake inaweza kuwa inachukua muda mrefu sana. Kwa hiyo, ninaamini ziko *investments* nyingine ambazo unaweza ukaziona tulisema tu na maduka mahali fulani yanafanyika ya milioni 500 mulioni 600. Wapate hiyo *license* tuwa-*comply,* kila mwaka. Kwa hiyo, niseme wazi tu tusifikirie tu kwamba unaweza ukampatia. Magazeti ambayo mimi nazaliwa niliyakuta leo hayapo. Wangepewa leseni ya miaka 200 ingekuwaje? ingetuletea shida Kwa hiyo, naomba tu waendele kukata leseni kila mwaka ili waendelee kufanya kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumzia hii habari ya hii Sheria yetu ya habari ninaomba nijikite kidogo kwenye eneo la reli. Ukiangalia kwenye eneo la reli kwenye Sheria yetu ya leo Sura namba 170 hapa wafanyabiashara binafsi wanaingia kuanza kuchangia, kulipa kama ni ada na kulipa mchango wote ambao utatakiwa kufanyika kwenye reli tulizonazo. Ukiangalia sisi huko nyuma hatukuwa na hii kitu, reli iliyokuwa inapita ni reli ya wananchi na treni inayopita ni treni ya wananchi. Kwa hiyo, matokeo yake ni kwamba kile ambacho tulitegemea kwamba tunaweza kuwa na treni mbili kutoka Kigoma zikaja Dar es Salaam utakuta inatoka treni moja kila siku, lakini kumbe tuna uwezo wa kutoa treni tatu kama *PPP* ambayo tumeisema leo hawa watajiunga na kuingia kufanya shughuli hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Sheria ya Reli kwenye ibara namba 38 na 52 imefanya mrekebisho haya; na ibara namba 46 inawezesha sasa kama kuna mtu mwenye nia ya kutumia maeneo ya reli kuomba kibali kwa shirika na kulipa ada pamoja na gharama zinazohusiana na matumizi hayo. Kwa hiyo, tunaamini kabisa hata Waheshimiwa Wabunge ambao wanataka sasa kununua treni zao ni muda wao sasa lakini kama

Mbunge unaona huwezi kununua treni au mwananchi hawezi kununua treni, nunua mabehewa ni muda wako sasa tunataka watu wafanye biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kingine kwenye ibara namba 52 tunaongeza kifungu namba 108 (5) kinaonesha wazi kwamba kuna masharti mtu yoyote ambaye anataka kuweka kuna mahali kunaitwa *railway crossing* barabra ina-*cross* na treni; barabara na Reli na unataka kuweka hiyo, wanasema tayari kwenye mabadiliko haya ya Sheria, kazi yako wewe ni Kwenda kuomba kibali. Kibali kile kitakupa nafasi ya wewe kama unazo fedha kufanya hicho kitu kwa kulinganisha na kile ambacho unatakiwa kulipa kwa gharama ulizo nazo wewe Kwa hiyo, ninaamini kabisa kwa mazingira haya, sasa wawekezaji wetu wana nafasi kubwa ya kuchangia kwenye uchumi wetu kwa sababu reli hii tunayojenga kama ni *SGR* au reli hii ambayo tunatumia ya zamani…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Magessa kengele ya pili, ahsante kwa mchango mzuri.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, naomba kuunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni 89 wa Mheshimiwa George Simbachawene (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, hawa ni wanafunzi na walimu kutoka Shule ya Msingi Kisima, iliyoko Jimbo la Kibakwe, Wilaya ya Mpwapwa, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Mrisho Gambo, wanafunzi 32 na walimu wawili kutoka *SAUT Campus* Arusha, karubuni. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Juma Hamad Omar kutoka Zanzibar, karibu. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Florence Samizi kutoka Kibondo, karibuni. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wanafunzi 110 na walimu 10 wa Shule ya Msingi ya Martin Luther ya Jijini Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Wanfunzi 50 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)*, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wanne kutoka Kampuni ya Remo kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ndaki, ajiandae Mheshimiwa Nape.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipa nafasi na mimi niweze kusema kidogo juu ya sheria zilizoko mbele yetu. Mimi ninajikita hasa kwenye uchambuzi wa sheria mabadiliko ya mbalimbali Sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa dhamira yake ya kweli ya kushughulikia masuala na hoja za nchi yetu. Kila mmoja ni shahidi, anaona jinsi ambavyo Rais wetu anahangaika anakimbia huku na kule ili kuhakikisha tu kwamba masuala ya nchi yetu yanakwenda sawasawa. Mambo mengine na kelele zingine zinazopigwa Mawaziri wapo wazishughulikie ili Mheshimiwa Rais tumpe nafasi ya kushughulikia hoja na masuala ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze pia Mawaziri wanaohusiana na Sheria hizi tunazozijadili leo. Mheshimiwa Waziri wa Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa usikivu wao hata wakati walipokutana na kamati mablimbali. Kwa kweli tunawashukuru sana kwa sababu walikuwa wasikivu na ushauri wa kamati ulizingatiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kidogo tu juu ya huduma za habari, hasa kipengele cha mwisho alichomalizia kuchangia Mheshimiwa Nusrat. Mheshimiwa Nusrat anasema kwamba, ukomo wa juu au ukomo pia wa chini ungeachwa wazi, lakini ni vizuri kukumbuka kwamba mahakama inaendeshwa na watu. Na kwa sababu inaendeshwa na watu kwenye utoaji haki kikatiba kila mtu anakuwa yuko sawa mbele ya Sheria. Sasa tukiacha wazi namna hiyo kama ambvyo ameshauri inawezekana kabisa mtu mwingine akapewa adhabu kubwa, mtu mwingine akapewa adhabu ndogo kwa kosa lile lile moja. Kwa hiyo kuwafanya watu hawa mbele ya Sheria waonekane wanahaki tofauti tofauti. Kwa hiyo, nadhani kwa namna ambavyo Kamati sisi tulishauri lakini pia namna ambavyo sheria ilikuwa imekaa bado haina makosa au matatizo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende upande wa Bohari ya Dawa. Upande wa Bohari ya Dawa, Ibara ya 27 inapendekeza kuondoa sekta binafsi kwenye wajumbe wa bodi. Ni maoni yetu na maoni yangu kwamba sekta binafsi ndiyo inakuwa injini ya kuendesha uchumi wetu. Na kwa sababu Bohari ya Dawa ina namna mbili, inatoa huduma lakini pia lazima na yenyewe ifikirie kuendesha kibiashara; ikiwa na mjumbe mmoja wapo kutoka sekta binafsi lingekuwa ni suala ambalo lina tija sana kwenye bodi. Huyu angeleta ubunifu wa kufanya biashara, huyu angeleta uzoefu, na huyu angeleta ujuzi ambao ungewasaidia bodi kuweza kufanya taasisi hii ifikirie pia kuendeshwa kibiashara badala ya kuendesha tu kama bodi ya kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwenye Sheria hii kipengele cha (f) wametaja baadhi ya watu watakao alikwa kuja kwenye bodi lakini haisemi watu hawa wanatoka kwenye sekta ipi. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kwamba Bohari ya Dawa hasa *board members* wao mmoja wapo atoke kwenye sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika,lakini pia, kwenye Sheria ya reli Ibara ile ya 44 inafuta kifungu kidogo cha (22)(3) ambacho pia kilikuwa kinaacha wazi kuacha Wakurugenzi pamoja na Mkurugenzi Mkuu, kwamba wanaweza wakatoka kwenye sekta binafsi, kwamba sasa wanatoka kwenye mlolongo ule wa kiserikali

*per se*. Lakini lengo letu hapa pia ni kufanya reli iwe ya kibiashara zaidi. Kwa hiyo tungeacha wazi kifungu hiki pia, kwamba muendeshaji wa Shirika letu la Reli kuanzia Mkurugenzi Mkuu na Wakurugenzi wengine wanaweza wakatoka kwenye sekta binafsi au wakatoka kwenye wigo ulio nje ya Serikali badala ya kutaka kila mtumishi wa Serikali hasa Wakurugenzi mbalimbali wa idara ya reli kwamba watoke ndani ya Serikali. Hii nayo ingeweza kuongeza ujuzi na ubunifu kwenye Shirika la Reli na hivyo kufanya Shirika la Reli lifanye shughuli zake kibiashara zaidi kama ambavyo mwelekeo wa sasa ulivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, yangu yalikuwa ni hayo machache naunga mkono hoja. Ahsnate sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Nape, jiandae Naibu Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyoko mezani. Mimi nitakwenda moja kwa moja kwenye mabadiliko ya Sheria mbalimbali na hasa kwenye Sheria ya huduma za habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuthibitisha kwa vitendo uumini wake katika kuhakikisha nchi yetu inasimamia uhuru wa wanahabari. Uhuru wa watanzania kujieleza na kupata habari lakini kubwa kuliko yote muumini wa demokrasia na haki katika nchi yetu. Yeye ndiye aliyeagiza mapitio ya Sheria hii ya Huduma za Habari ya mwaka 2016. Namshukruru sana Mheshimiwa Rais kwa uwamuzi wake huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili nichukue nafasi hii kuwashukuru wafau wa sekta ya habari na hasa wanahabari kwa namna ambavyo walitoa ushirikiano baada ya maagizo haya ya Mheshimiwa Rais. Tumekuwa na vikao nao kwa karibia kipindi cha mwaka mzima. Tumekuwa na mazungumzo, tumezengumza kwa kina wameonesha uzalendo mkubwa wakati wakishirikiana kwenye maeneo haya na mpaka tukafikia kuyaleta

mependekezo haya hapa kwenye Bunge lako Tukufu na ndiyo maana unaona mambo yanakwenda sawasawa bila kelele kwa sababu tumekubaliana namna ya kusonga mbele tuijenge nchi yetu; na hapa wadau wa ndani na wadau wa nje, kwa sababu wako pia wadau wa nje ambao wameshirikiana katika kuahkikisha haya mabadiliko ya Sheria yanakidhi matakwa na hali halisi ya nchi yetu leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa niishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa namna ambavyo wametuongoza wametushauri, tumeshauriana nao kwa kina, tumekuwa na vikao nao ambavyo vimeboresha sana haya mapendekezo ambayo yako hapa. Kwa kweli tuna Kamati nzuri ina watu weledi, wazalendo wamefanya kati nzuri sana kutufikisha hapa tulipofika. Nimshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa namna ambavyo ametuongoza pamoja na Waziri mwenzangu wa Katiba na Sheria lakini na wenzangu Wizarani ambao kwa pamoja kupitia Idara ya Habari Maelezo tumeshirikiana kuifikisha sheria hapa ilipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wadau walileta mapendekezo 21 kama ilivyoelezwa hapa ambayo walitaka tuyapitie kwa pamoja. Katika mapendekezo hayo 21 yakagawanyika katika makundi manne. Hoja ambazo tulikubaliana baada ya majadiliano kwamba zibaki kama zilivyo kwenye Sheria, baada ya mazungunmzo ya muda mrefu na tukakubaliana kwa pamoja takribani hoja nane kati ya 21 tukakubaliana zibaki kama zilivyo, lakini hoja nyingine tukakubaliana zifanyiwe marekebisho ikiwemo kufutwa. Ninamshukuru sana dada yangu Nusrat, amesema hapa, kwamba Serikali ya Rais Samia Serikali ya Awamu ya Sita, Serikali sikivu katika mapendekezo takribani tisa tulikubali yafutwe, yarekebishwe ikiwemo kuondoa jinai.

Mheshimiwa Naibu Spika, na nadhani dada yangu alikuwa hajapewa yote, kwenye Sheria hii tumeondoa jinai kabisa haimo na hili ni jambo zuri litaijenga tasnia ya habari ikue na kuendelea vizuri. Kwa hiyo vipo vifungu ambavyo vimefutwa kabisa

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini baadhi ya mambo tulikubaliana kwamba yaende kurekebishwa au kufanyiwa kazi kwenye Kanuni tutakazozitunga hivi karibuni; na moja wapo ilikuwa ni suala la leseni na muda wa leseni. Tumekubaliana kwamba hili jambo likashughulikiwe kwenye kanuni na ka hiyo liko sawa sawa. Tofauti na wanavyosema kwamba Sheria inazungumza habari ya mwaka mmoja, sheria inasema ikatunge kanuni ya namna hili suala la leseni litakavyoshughulikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya mwisho ilikuwa ni hoja ambayo ni moja tu, ambayo ilikuwa haiwezi kurekebishika kwa sababu iko kwa mujibu wa sera, kwa hiyo itasubiri mapitio ya sera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wengi wanapoizungumzia Sheria hii wanazungumzia haki za wanahabari, lakini kwenye Sheria hii tumezingatia haki za walaji wa kazi za wanahabari; maana na wao wanahaki zao. Kwanza kupewa taarifa ambayo ni sahihi, na ndiyo maana kwenye Sheria hii tunataka taaluma ya habari iwe taaluma, ili waingie watu wenye ueledi wachakate taarifa vizuri, wawalishe watumiaji wa tarifa zao jambo ambalo limechakatwa kitaalamu, jambo ambalo limewatendea haki walaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kweye sheria humu kuna wajibu lakini kuna haki, haki zao zipo lakini kuna wajibu wao, na wanahabari wakitimiza wajibu wao nchi yetu itatulia kwa sababu watu watapewa taarifa kwa mujibu wa taaluma na kazi itakuwa nzuri. Kwa hiyo Sheria hii imezingatia jambo hili, na mimi ni matumaini yangu kwamba wanahabari watakwenda kufurahia Sheria hii itakwenda kukuza tasnia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, tunazo Taasisi za Kimataifa ambazo zinafanya tathmini ya hali ya demokrasia na uhuru wa Wanahabari na uhuru wa kujieleza. Sasa ni wito wangu nitumie Bunge lako hili kuziomba taasisi hizi zitumie taarifa za sasa hivi, baada ya mabadiliko haya watufanyie tathmini, maana wamekuwa wanatumia taarifa za muda mrefu na inaonekana ni kama vile hatujapiga hatua, lakini tumepiga hatua kubwa, Serikali

ya Awamu ya Sita imefanya mengi katika kurekebisha uhuru wa watu kujieleza, uhuru wa Wanahabari na kupanua wigo wa demokrasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba Wabunge tuunge mkono, tupitishe haya mabadiliko. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa fursa hii uliyonipa ili kuwa sehemu ya wachangiaji katika Muswada huu. Naomba awali ya yote kumshukuru Mwenyezi Mungu Rahim muumba wa mbingu na ardhi kwa kutujalia kuwepo hapa katika kujadili masuala ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niwapongeze sana Kamati ya bajeti, Kamati ambayo muda wote inafanya kazi kwa umakini mkubwa na uadilifu mkubwa. Naomba nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa namna anavyonielekeza na kunishauri katika utendaji wa kazi zetu za kila siku. Pia naomba kumpongeza Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa namna alivyoshiriki na kutusaidia katika kupitisha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo yote, naomba niende tu kwenye michango ambayo wametoa Waheshimiwa Wabunge na maendekezo yao. Kwanza Serikali imepokea michango na maoni ambayo yametolewa na Kamati na Wabunge wote, kwani Wabunge wamechangia kwa uzuri kabisa na kwa ufanisi mkubwa sana. Serikali tayari imepokea mapendekezo ya Kamati ambayo tayari hadi sasa imeshaanza kufanya utekelezaji wa kutoa Waraka Na.7 wa Hazina wa mwaka 2021 kwa Maafisa Masuuli kuhusu utekelezaji wa miradi kwa utaratibu wa *PPP* kwa kuhakikisha kwamba wanatenga fedha mahususi katika bajeti zao kwa ajili ya kutekeleza miradi hii ya *PPP*.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, miongoni mwa mapendekezo ya Kamati ni kutoa taaluma kwa umma. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba, taaluma hii inaendelea kutolewa na Serikali siku hadi siku kwa njia zote zinazojulikana katika kutoa taaluma. Kupitia kwako niwaombe Wabunge wenzangu na wao wawe sehemu ya kutoa taaluma kwani Wabunge walio wengi au Wabunge wote wana weledi mzuri na uelewa mzuri kuhusu umuhimu wa *PPP*.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe kwa fursa hii wote tuchukue nafasi hii kutoa taaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri, jiandae Mheshimiwa *AG*.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kutoa machache katika kuihitimisha hoja hii. Awali ya yote niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia hoja hii ambayo tumeiweka ya *PPP,* natambua mchango wa Mwenyekiti wetu wa Kamati, maoni ya Kamati yenyewe, maoni ya Wabunge wengine waliochangia akiwemo Mheshimiwa Kandege na Mheshimiwa Katimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeyapokea maoni hayo na yanaenda sambamba na hatuna haja ya kubishana nao kwa sababu hoja hizo zote ambazo wamezitaja zina mantiki na kwa kweli hilo ndio lengo mahususi ambalo Mheshimiwa Rais ameliona katika kuifanya Sheria yetu hii ya *PPP* iweze kufanya kazi kwa urahisi. Mheshimiwa Kandege ameelezea kuhusu barabara pamoja na bandari lakini na barabara ya upande wa pili kwenda *DRC,* haya ndio hasa maengo mahususi ya sheria hii kwamba tuweze kuongeza wigo wa kufanya shughuli za maendeleo kwa njia hii ya ushirikishaji wa Sekta Binafsi ikishirikiana na Sekta ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu hii imetoka mbali sana, ukichukua ulinganifu wa hata upande wa makusanyo tu kabla ya ushiriki mpana wa Sekta Binafsi na sasa pana utofauti mkubwa sana. Ukichukua wakati tuko Sekta ya Umma kufanya kazi kwa asilimia zote, chukulia mfano wakati Awamu ya Pili inaingia makusanyo kwa mwezi yalikuwa takribani bilioni 30. Bilioni 30 kwa mwezi makusanyo hayo leo hii tunaongelea ni fedha iliyo chini hata ya mgao wa Wizara moja katika fedha ambazo zinakwenda kwenye Wizara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unaweza ukaona kwamba ushiriki wa Sekta Binafsi ambapo unaenda kuongeza shughuli za uzalishaji, leo hii umeweza kuongeza makusanyo kwa kiwango kikubwa na ushiriki wa wananchi ambao wanashiriki katika shughuli za maendeleo kupitia Sekta Binafsi. Kwa hiyo Sheria hii ambayo tumeileta inaenda kupunguza kama tulivyoelezea wakati wa kutoa maelezo kupunguza yale yaliyokuwa yanakwamisha miradi kuweza kutekelezwa kwa namna hiyo. Hivyohivyo na kile ambacho Kamati imetushauri na kile ambacho Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Sillo ameelezea ni yale ambayo yanaenda kuboresha kuanzia mchakato wa ushiriki wa Sekta Binafsi lakini pia na baada ya kuwa mradi umeshaanza kutekelezwa kwa njia hizo za ubia.

Mheshimiwa Naibu Spika, yale yote ambayo yameelezewa ambayo yanaenda kuboresha zaidi utendaji, tumeyapokea na tutakapoenda kwenye utungaji wa kanuni tutazingatia ili kuweza kuleta ufanisi wa Sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kutoa hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, Mheshimiwa *AG*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa na kwa taadhima nichukue fursa hii kwa mara nyingine nikushukuru sana wewe mwenyewe kwa jinsi ambavyo umetoa fursa ya Muswada wa Serikali wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali kujadiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru sana wachangiaji sita kwa kuanza na Kamati yetu ambayo imewakilishwa hapa na Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, lakini pia Waheshimiwa Wabunge Selemani Zedi, Mheshimiwa Nusrat, Mheshimiwa Bryceson Magessa, Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki na Mheshimiwa Nape Moses Nnauye.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefarijika jinsi ambavyo tuliushughulikia mchakato wa Muswada huu. Hatua tuliyofikia ilikuwa na majadiliano ya kina na wadau wetu kabla ya kuandaliwa kwa Muswada, lakini pia mashauriano ya kina na Kamati. Kwa hiyo jedwali la marekebisho ambalo limewasilishwa limeonesha jinsi ambavyo kulikuwa na ushiriki ambao ulituleta pamoja kati ya Bunge lako Tukufu kupitia Kamati, lakini na sisi upande wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano wa maboresho na maendeleo makubwa ambayo tumekuwa nayo katika namna ya kutunga sheria zetu. Sheria ya Huduma za Habari ni mojawapo ya enao ambalo nchi yetu tumepiga hatua kubwa. Tukiangalia tangu itungwe 2016 ni Sheria ambayo ililenga kufanya huduma hizi za habari sasa kuwa za kitaaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili linadhihirishwa kwenye Sheria hiyo tuna Bodi ambayo Mwenyekiti wake wala siyo hatoki Serikalini. Majukumu yale ni makubwa, lakini vilevile tuna Baraza ambalo linahusisha Wanahabari wenyewe. Sasa ni nadra sana kupata hii, kwa hiyo nampongeza sana Mheshimiwa Rais, lakini pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri ameeleza mwenyewe ambavyo amekuwa na vikao vingi na Wanahabari na kuwa na maeneo 21 ni jinsi ambavyo yameshughulikiwa. Pia kwa sababu naelewa ushiriki wa Viongozi, Wamiliki wa Vyombo vya Habari na Wanahabari, nina kila sababu ya kupongeza viongozi wawe kutoka kwenye Bodi lakini na kwenye Baraza lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo machache ambayo yameongelewa hapa mojawapo nafikiri ni hili la leseni. La kwanza ningependa tu kumbukumbu zikae sahihi. Mheshimiwa

Waziri mwenye dhamana amelieleza vizuri, ni jambo ambalo linaendelea kujadiliwa kule. Hata hivyo, suala la leseni kwa wanataaluma huwa lina lengo la kuimarisha tasnia husika na kuifanya itende kazi zake kwa weledi na ndio maana Baraza la Wanahabari, kazi yake moja ni kuangalia mambo ya maudhui na wala halina ubaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ukiangalia tuna Wanasheria wa kujitegemea ambao ni Wanachama wa *TLS,* wana Majengo, Wana Ofisi zao, wana Maktaba za thamani, lakini kila mwaka wanahuisha leseni zao. Sasa na wala hatuwezi tukajificha hata kwenye mwamvuli wa kimataifa kwa sababu mimi mwenyewe kwa mfano ni mjumbe kwenye *International Prosecutors' Association* kwa miaka 15 na kila mwaka nahuisha uanachama wangu. Ni mjumbe kwenye *Common Wealth Magistrate and Judges' Association* ambako ninahuisha uanachama wangu kila mwaka na kulipa zile ada. Kwa hiyo jambo hili ningependa nilieleze kwamba litaendelea kujadiliwa kwa kupitia majukwaa yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunapokuja kwenye suala la adhabu ya juu au ya chini, ningependa tu kueleza kwamba tumepiga hatua kubwa, kwa sababu kwa makosa kwa mfano yale yanayohusiana na kazi zao, kabla ya mabadiliko haya, kwa mfano kima cha chini cha adhabu kama ni ya *fine* ilikuwa ni milioni tanolakini cha juu ilikuwa milioni 20. Sasa kwenye kifungu cha 50 tunaporekebisha kinashuka kuwa milioni tatu kwa *fine* kwenda milioni 10, lakini kama ni jela kabla ya sasa ilikuwa miaka mitatu mpaka mitano, sasa ni miaka miwili mpaka mitano lakini kuna mahali kwa mfano tumetoka miaka mitano mpaka mwaka mmoja. Sasa lengo lake ni lipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo lake ni kutambua kwamba wanataaluma wowote wana fursa ya kujirekebisha na kukua. Kwa hiyo nitapenda sana watakapopitia lile Jedwali la Sheria yenyewe, nafikiri watapata fursa ya kuona kwamba heshima ipi na wamezingatiwaje katika mambo ambayo yapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tujue wigo wa adhabu zote zilizowekwa ukitoa *one third remission* ambayo ni *automatic* chini ya Sheria ya Magereza, lakini vifungu vyote au adhabu hizi zinaangukia vilevile kwenye vifungo vya nje kwa yule ambaye atatimiza Sheria ile ya *Community Service*, Sheria ya *Parole* na kadhalika. Kwa hiyo, niombe sana Wanahabari kupitia mamlaka yao wendelee kushirikiana na Serikali

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko yaliyo kwenye Sheria ya Reli yakisomwa pamoja na maboresho mengine ya Sheria ya *PPP*, Sheria ya Uwekezaji, nafikiri ni kipindi cha kujitathmini kama Taifa na kuona namna ya watu kutumia fursa zilizopo sasa kwenye uwekezaji kupitia sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, niendelee tu kusema kwamba, kazi ya Ofisi yangu, kazi ya Bunge hili ni kuhakikisha tuna sheria nzuri na jambo ambalo siku zote tutaendelea ni sisi kufanya kazi kwa kushirikiana na Bunge na Kamati zake na Wabunge wote na wananchi wote. Mengine tuendelee kuwatakia heri na tumtakie heri Mheshimiwa Spika katika mbio za uchaguzi ujao. Ujumbe wangu ni mmoja tu, siyo yeye ni nchi na kwa kuwa ni nchi, ni lazima tumuunge mkono kwa gharama yoyote na jambo liwe la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA– KATIBU MEZANI:** Kamati ya Bunge Zima.

**NAIBU SPIKA:** Kamati ya Bunge Zima.

**13 JUNI, 2023**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Katibu

**NDG. BAKARI KISHOMA– KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa Mwaka 2023 *(The Public Private Partnership (Amendment) Bill, 2023)***

Kifungu cha 1

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 2

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 3
Kifungu cha 4
Kifungu cha 5
Kifungu cha 6
Kifungu cha 7
Kifungu cha 8

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 9

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 10
Kifungu cha 11
Kifungu cha 12
Kifungu cha 13

Kifungu cha 14
Kifungu cha 15
Kifungu cha 16

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. BAKARI KISHOMA– KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya marekebisho hayo, Serikali inapendekeza kifungu cha 2-16 sasa kisomeke kifungu cha 3-17.

**MWENYEKITI:** Hiyo ilikuwa ni *numbering*, inaafikiwa?

*(Mpangilio wan amba wa vifungu vilivyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima)*

**NDG. BAKARI KISHOMA– KATIBU MEZANI:** Naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Mtoa hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa 2023 (*The Public Private Partnership (Amendment) Bill, 2023]* kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba taarifa hiyo sasa ikubaliwe rasmi na Bunge Zima, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ya mwaka 2023 *[The Public Private Partnership (Amendment) Bill, 2023]*.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Wasioafiki waseme siyo (kimya) wote wameafiki.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kufanya Marekebisho Katika Sheria ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kwa Lengo la Kuondoa Mapungufu ambayo Yamebainika wakati wa Utekelezaji wa Sheria Hiyo. (*A Bill for an Act to Amend the Public Private Partnership Act in Order to Address Some Challenges which were Encountered during Its Implementation)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

*(Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa Mwaka 2023 (The Public Private Partnership (Amendment) Bill, 2023) Ulipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umeshasomwa mara tatu kwa hatua ya Bunge tumemaliza kazi yetu. Mheshimiwa Waziri hongera sana. Ninaipongeza Kamati ambayo ilishughulikia Muswada huu, Kamati ya Bajeti hongereni sana kwa kazi nzuri mliyoifanya, niwashukuru na kuwapongeza Wabunge kwa michango yenu mizuri hatimae mpaka sasa tumefikia Muswada huu wa *PPP* kukamilika na sasa unasubiri idhini ya Mheshimiwa Rais na akisharidhia tu unakuwa sheria na

utaanza kufanya kazi. Kwa kweli Muswada huu ni muhimu sana hasa kwenye dunia ya leo, ambayo sasa uchumi ndiyo mstari wa mbele. Mheshimiwa Rais amevalia njuga uchumi wa Taifa letu na mabadiliko mengi yatakuja, mabadiliko hayo ni maslahi mapana kwa Taifa letu. Nichuke nafasi hii vilevile kushukuru watendaji wote ambao wameshiriki katika kufanikisha Muswada huu kuweza kupita. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Katibu

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments Bill, 2023)***

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2
Kifungu cha 3
Kifungu cha 4
Kifungu cha 5
Kifungu cha 6
Kifungu cha 7

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 8
Kifungu cha 9
Kifungu cha 10
Kifungu cha 11
*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 12
Kifungu cha 13
Kifungu cha 14
Kifungu cha 15
Kifungu cha 16
Kifungu cha 17
Kifungu cha 18
Kifungu cha 19

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 20
Kifungu cha 21
Kifungu cha 22
Kifungu cha 23
Kifungu cha 24
Kifungu cha 25

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 26

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 27

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 28

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 29

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 30
Kifungu cha 31
Kifungu cha 32
Kifungu cha 33
Kifungu cha 34
Kifungu cha 35
Kifungu cha 36
Kifungu cha 37
Kifungu cha 38

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 39
Kifungu cha 40
Kifungu cha 41
Kifungu cha 42
Kifungu cha 43
Kifungu cha 44
Kifungu cha 45
Kifungu cha 46
Kifungu cha 47
Kifungu cha 48
Kifungu cha 49
Kifungu cha 50
Kifungu cha 51

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 52
Kifungu cha 53
Kifungu cha 54

Kifungu cha 55
Kifungu cha 56

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 57
Kifungu cha 58
Kifungu cha 59
Kifungu cha 60
Kifungu cha 61
Kifungu cha 62
Kifungu cha 63
Kifungu cha 64
Kifungu cha 65
Kifungu cha 66
Kifungu cha 67
Kifungu cha 68
Kifungu cha 69

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarudi.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Mtoa hoja.

**T A A R I F A**

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2023, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima limeupitia Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya

Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments Bill, 2023)* Ibara kwa Ibara nakuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments Bill, 2023)* kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

Sasa nitawahoji kuhusu Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments Bill, 2023)*.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali zipatazo Nane kwa lengo la kuondoa mapungufu ambayo yamejitokeza wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika sheria hizo *(A Bill for an Act to Amend Certain Written Laws in order to keep the Laws updated with some challenges observed in its/or implementation)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

*(Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023 (The Written Laws Miscellaneous Amendment Bill, 2023) Ulipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa hatua hii sasa kazi ya Bunge imekwisha, Muswada umepita na umeshasomwa kwa mara ya tatu na sasa unaeleka kwa Mamlaka ya Rais kwa idhini yake akiridhia, akishasaini Muswada huu unakuwa ni sheria na utaanza kutumika pale ambapo atakapokuwa ameshamiliza kusaini na kama kawaida yetu Bunge litajulishwa.

Nakushukuru sana Mheshimiwa *AG* kwa kazi kubwa uliofanya vilevile usingeweza kufanya pekee yako bila ushirikiano wa Kamati ya Sheria na Utawala ya Bunge kwa namna walivyoshirikiana na wewe, lakini kikubwa ni namna michango ya Wabunge ambao wameshiriki kabisa kuhakikisha Muswada huu unapita. Hii ndiyo demokrasia ya nchi kwa Bunge linakaa na Serikali, Wabunge wanaita wadau, wadau wanatoa maoni. Ninampongeze Waziri mhusika wa sekta hii vilevile kwa namna anavyoshirikiana na wadau wake na kuhakikisha kuwa uhuru wa habari unapatikana na walaji wa habari wapewe taarifa ambazo ziko sahihi. Kama vile ukiambiwa Mayele kafunga goli 17 basi iwe ni goli 17, Saido goli 17 taarifa sahihi ndiyo walaji wanataka. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninawakumbusha tena Wajumbe wa Kamati ya Uongozi na Kamati ya Bajeti watakutana na Serikali muda huu Ukumbi wa Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho Saa Tatu Asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 6.48 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 14 Juni, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*